# MAKOSA YA KISARUFI YANAYOFANYWA NA WANAFUNZI WATAITA WA SHULE ZA MSINGI WANAOJIFUNZA KISWAHILI SANIFU KATIKA KAUNTI YA TAITA / TAVETA NCHINI KENYA

**MARTINA ZIGHE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SEPTEMBA, 2021**

# UNGAMO

Ripoti hii ya utafiti ni kazi yangu asilia na haijapata kuwasilishwa popote kwa madhumuni yoyote ya shahada katika chuo chochote.

Sahihi ................................... Tarehe..................................................

**MARTINA ZIGHE**

**C50/ CE/28176/2013**

Ripoti hii ya utafiti imetolewa na kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi.

**Dkt. Jacktone Onyango**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi ………………................ Tarehe…………………………….....

**Dkt. Leonard Chacha**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi ………………………….. Tarehe………………………………

# TABARUKU

Kwa watoto wangu Faith, Doris na Martin walionivumilia nilipokosa kuwa nao ili nitekeleze masomo yangu.

Kwa mume wangu mpendwa Peter Karanja aliyenihimiza katika harakati za masomo yangu.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Maulana kwa kuniwezesha kuifanya kazi hii hadi nikaihitimisha.

Napenda kushukuru kila mtu aliyechangia kwa njia moja au nyengine katika ufanisi wa utafiti huu. Aidha, nawashukuru wenzangu wote tuliosoma nao hasa Philemona Ndinda, Eunice Wavinya na Ann Gitau kwa msaada wao.

Namshukuru mume wangu kwa kusimama nami kwa kila njia hadi nikahitimisha shahada yangu. Pia, nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Jacktone Onyango na Dkt. Chacha Leonard kwa mawaidha yote waliyonipa katika kila hatua ya kazi hii hadi tukahitimisha.Vilevile namshukuru Dkt. Peter Karanja aliyewahi kuwa msimamizi wangu alipokuwa angali mhadhiri katika Chuo kikuu cha Kenyatta.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu. Utafiti uliongozwa na nadharia za Uchanganuzi Linganuzi (UL) na Uchanganuzi Makosa (UM). UL ni nadharia ya uchanganuzi wa kiisimu unaohusisha ulinganishaji wa lugha mbili. Nadharia hii ilituwezesha kuchunguza athari za lugha ya Kitaita kwa wanafunzi Wataita wanapojifunza Kiswahili Sanifu. UM ulituwezesha kubainisha aina mbalimbali za makosa ya kisarufi ya wanafunzi na jinsi ya kuyakabili. Malengo ya utafiti huu yalikuwa: Kubainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi katika kujifunza Kiswahili Sanifu, kuainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi, kuchunguza uhusiano uliopo kati ya makosa yanayofanywa na wanafunzi Wataita na ubashiri wa UL na kubainisha mbinu mwafaka za kuyakabili makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu. Utafiti ulihusisha ukusanyaji data kupitia kwa maongezi na maandishi. Utafiti ulihusisha shule sita za msingi kutoka tarafa ya Wundanyi katika kaunti ya Taita/Taveta zilizoteuliwa kuzingatia usampulishaji. Wanafunzi walioshirikishwa ni wale wanaoongea Kitaita kama $L_1$ waliokuwa darasa la saba. Wanafunzi watano waliteuliwa kutoka kila shule kutumia njia ya sampuli nasibu, kwa jumla wakiwa wanafunzi thelathini. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni hojaji, mahojiano yaliyochochewa na usimulizi wa hadithi na ukaguzi wa insha zilizowahi kuandikwa na wanafunzi na kusahihishwa na walimu wao. Hojaji ilihusisha jaribio lililojumuisha sehemu mbili za maswali. Sehemu ya kwanza ilishirikisha maswali ya kutafsiri kauli kutoka kwa Kitaita hadi Kiswahili Sanifu na ya pili ilikuwa na maswali ya kujaza mapengo yaliyoachwa wazi katika sentensi. Maswali ya kutafsiri yalituwezesha kuchunguza ikiwa Kitaita kiliathiri wanafunzi katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu na yale ya kujaza mapengo yalitusaidia kubainisha vipengele vya kisarufi vilivyowatatiza wanafunzi. Katika kukusanya data ya maongezi iliyohusisha masimulizi ya hadithi, mtafiti alizinasa kwa kanda kisha baadaye akazinakili na kuzichunguza. Utafiti ulijikita kwa makosa yaliyohusu nomino, vivumishi na virejeshi. Data iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo ambapo majedwali yalitumika. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwepo kwa makosa ya kisarufi yaliyotokana na athari za lugha ya Kitaita. Makosa hayo yalijumuisha uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu kutoka $L_1$ hadi $L_2$ na tafsiri potofu. Makosa mengine yalikuwa ujumuishaji mno, uhamishaji wa ufundishaji na kutomakinika kwa wanafunzi katika maandishi yao ya Kiswahili Sanifu. Mikakati ya kuyashughulikia makosa haya tuliyoibainisha ni: utangamano wa mwalimu na wanafunzi, wanafunzi kushirikiana katika kukosoana, mwalimu kutambua chanzo cha kosa la mwanafunzi na kumwelekeza, mwalimu kujitayarisha vilivyo kabla ya somo, matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa, ufundishaji wa Kiswahili kwa kuzingatia mwelekeo wa UL na kutahadharisha wanafunzi dhidi ya tafsiri sisisi. Ilipendekezwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu makosa ya wanafunzi Wataita kuhusiana na vipengele kama fonolojia, semantiki na msamiati.

## ABSTRACT

This study aimed at investigating the grammatical errors among Taita students learning Kiswahili. This study was informed by two theories: Contrastive analysis and Error analysis. The former is used to compare and contrast two languages and helped to investigate the influence of Taita language among the Taita students when learning Kiswahili as their second language. The theory of error analysis was important in identification of various grammatical errors and ways of overcoming them. This study had the following objectives: To identify grammatical errors committed by primary school Taita learners when learning Kiswahili language, to categorize grammatical errors committed by primary school Taita learners when learning Kiswahili language, to find out the relationship between the actual grammatical errors committed by Taita learners of Kiswahili and those predicted by the contrastive analysis theory and lastly to device ways and means of overcoming those grammatical errors committed by Taita learners when learning Kiswahili language. Data was obtained from the learners through their spoken word as well as their writings. Data was obtained from six (6) primary schools in Wundanyi Division in Taita/Taveta County through sampling techniques. The learners used in data collection were those using Taita as their first language and all were in standard seven (7). Through simple random sampling, five (5) learners were picked from each of the primary schools totaling to thirty (30) learners. Data was collected through questionnaires and interviews, the latter coming in strongly through narration of stories. Analysis was conducted on past Kiswahili compositions submitted for marking by the learners. Questionnaires incorporated a section on translation of Taita sentences into Kiswahili as well as another on filling gaps. The first was meant to identify the influence of Taita language on the learner's acquisition of Kiswahili language while the second was to clearly identify the grammatical aspects that were a challenge to the learners. The study investigated errors related to nouns, adjectives and pronouns. Data was analysed using descriptive analysis and was displayed using tables. The study identified Kiswahili grammatical errors emanating from the influence of Taita language. The errors comprised of transfer of linguistical forms and structures from $L_1$ (Taita) to $L_2$ (Kiswahili) and wrong translations. Other errors involved overgeneralization as well as transfer of errors received from the teachers during teaching and also carelessness on the part of the learners. Among the strategies recommended to overcome the identified grammatical errors were: closer interaction between the learners and teachers cooperation and peer corrections among the learners, early identification of the learners errors by the teachers and correcting them, proper lesson preparation on the part of the teachers, use of recommended books in schools for teaching/learning, teaching Kiswahili using recommendations from the contractive analysis theory and discouraging learners from using direct translations. The areas recommended for further research include errors among Taita learners in areas of phonology, semantics and vocabulary.

# VIFUPISHO NA ISHARA

| | |
|---|---|
| § | Sehemu |
| KICD | Kenya Institute of Curriculum Development |
| KIV | Kivumishi |
| $L_1$ | Lugha ya Kwanza |
| $L_2$ | Lugha ya pili |
| LK | Lugha Kadirifu |
| LL | Lugha Lengwa |
| NACOSTI | National Commission for Science, Technology & Innovation |
| NOM | Nomino |
| TAR | Tarakimu |
| TAZ | Tazama |
| UL | Uchanganuzi Linganuzi |
| UM | Uchanganuzi Makosa |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

| | |
|---|---|
| **Kosa katika lugha** | Mfumo potofu kwa wanaojifunza lugha unaohusiana na sarufi, msamiati au matamshi ya lugha hiyo. |
| **Ngeli** | Ngeli za nomino ni kundi la majina yanayofanana kwa upatanisho wa kisarufi, na viambishi vyao vya umoja na wingi. |
| **Sarufi** | Kanuni, sheria au taratibu zinazotawala viwango mbalimbali vya lugha fulani - fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. |
| **Upatanishi wa kisarufi** | Uwiano unaopatikana baina ya nomino na maneno mengine katika sentensi. |
| **Vivumishi** | Kivumishi ni neno ambalo hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino |

# YALIYOMO

UNGAMO ........ i

TABARUKU ........ ii

SHUKRANI ........ iii

IKISIRI ........ iv

ABSTRACT ........ v

VIFUPISHO NA ISHARA ........ vi

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU ........ vii

ORODHA YA MAJEDWALI ........ viii

SURA YA KWANZA ........ 1

UTANGULIZI ........ 1

1.0 Usuli wa mada ........ 1

1.1 Suala la utafiti ........ 2

1. 2 Madhumuni ya utafiti ........ 4

1.3 Maswali ya utafiti ........ 5

1.4 Sababu za kuchagua mada ........ 5

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti ........ 8

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 9

1.7 Misingi ya Nadharia ........ 14

1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) ........ 14

1.7.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM) ........ 16

1.8 Mbinu za utafiti ........ 20
1.8.1 Muundo wa utafiti ........ 20
1.8.2 Maadili ya Utafiti ........ 20
1.8.3 Sampuli ........ 21
1.8.4 Mbinu zilizotumika kukusanya data ........ 22
1.8.4.1 Hojaji ........ 22
1.8.4.2 Mahojiano ........ 24
1.8.4.3 Ukaguzi wa insha ........ 24
1.8.5 Vifaa vilivyotumika kukusanya data ........ 24
1.8.5.1 Hojaji ........ 25
1.8.5.2 Karatasi za mazoezi ........ 25
1.8.5.3 Kinasa sauti ........ 25
1.8.5.4 Kiongozi cha mahojiano ........ 25
1.8.6 Uchanganuzi wa data ........ 26
1.8.7 Uwasilishaji wa matokeo ........ 26
1.9 Hitimisho ........ 27
SURA YA PILI ........ 28
VIPENGELE VYA KISARUFI VYA KISWAHILI NA KITAITA ........ 28
2.0 Utangulizi ........ 28
2.1 Kiswahili ........ 28
2.1.1 Dhana ya ngeli za nomino za Kiswahili ........ 29
2.1.1.1 Uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia ........ 29
2.1.1.2 Uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili kisintaksia ........ 31

2.1.2 Upatanishi wa kisarufi wa nomino na vivumishi........................................ 34

2.1.2.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa .......................................... 36

2.1.2.2 Vivumishi vimilikishi .................................................................... 37

2.1.2.3 Vivumishi viulizi ......................................................................... 38

2.1.2.4 Vivumishi vya ‘- a’ unganifu ................................................................... 39

2.1.2.5 Vivumishi vya pekee.................................................................... 39

2.1.2.6 Vivumishi vya idadi (Tarakimu)............................................................. 40

2.1.3 Urejeshi katika Kiswahili............................................................... 41

2.1.3.1 Urejeshi wa kileksia ....................................................................... 42

2.1.3.2 Urejeshi unaodhihirishwa na viambishi................................................... 42

2.1.3.3 Virejeshi awali ............................................................................ 42

2.1.3.4 Virejeshi tamati ............................................................................ 43

2.2 Kitaita.................................................................................................... 43

2.2.1 Ngeli za nomino katika Kitaita .............................................................. 44

2.2.1.1 Ngeli za nomino za Kitaita kimofolojia.................................................. 44

2.2.1.2 Ngeli za nomino za Kitaita kisintaksia .................................................... 46

2.2.2 Upatanishi wa kisarufi wa nomino na vivumishi........................................ 49

2.2.2.1 Upatanishi wa nomino na vivumishi vya sifa .......................................... 49

2.2.2.2 Vivumishi vimilikishi .................................................................... 51

2.2.2.3 Vivumishi viulizi ......................................................................... 52

2.2.2.4 Vivumishi vya ‘A’ unganifu .................................................................. 53

2.2.2.5 Vivumishi vya pekee.................................................................... 54

2.2.2.6 Vivumishi vya idadi ....................................................................... 55

2.2.3 Urejeshi katika Kitaita .......................................................................... 57

2.3 Ulinganishaji wa vipengele vya kisarufi vya Kiswahili naKitaita.................. 57

2.3.1 Mfanano katika Kiswahili na Kitaita .......................................................... 58

2.3.2 Tofauti katika Kiswahili na Kitaita............................................................. 61

2.4 Ubashiri wa nadharia yaUL ............................................................................ 63

2.5 Hitimisho......................................................................................................... 65

SURA YA TATU .................................................................................................. 66

UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KISARUFI............................................ 66

3.0 Utangulizi......................................................................................................... 66

3.1 Mifano ya makosa mbalimbali ya kisarufi...................................................... 67

3.1.1 Makosa yanayohusiana na upatanishi wa nomino na kivumishi ................. 67

3.1.1.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa ........................................... 68

3.1.1.2 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha kumiliki ................................... 72

3.1.1.3 Upatanishi wa nomino na kivumishi kiashiria.......................................... 74

3.1.1.4 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi /Tarakimu ....................... 76

3.1.1.5 Upatanishi wa nomino na kivumishi kiulizi ............................................. 79

3.1.1.6 Upatanishi wa nomino na vivumishi vya pekee ....................................... 80

3.1.1.7 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha ‘-a’ unganifu............................ 82

3.1.2 Makosa yanayohusu urejeshi wa nomino katika vitenzi.............................. 83

3.2 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa .............................................. 87

3.2.1 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa katika insha ....................... 87

3.2.2 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa katika masimulizi.............. 89

3.3 Aina mbalimbali za Makosa ya kisarufi katika kazi za wanafunzi................. 91

3.3.1 Matumizi ya viambishi vipatanishi vya ngeli visivyofaa ............................ 92

3.3.2 Uongezaji vipashio au sauti pasipostahili ................................................. 93

3.3.3 Udondoshaji wa vitamkwa au maneno katika tungo ................................... 94

3.3.4 Mpangilio potofu wa vipashio katika sentensi........................................... 95

3.3.5 Kuchanganya vipashio .................................................................................. 96

3.3.6 Uakifishaji wenye makosa ........................................................................... 96

3.3.7 Urudiaji wa vipashio ..................................................................................... 98

3.4 Hitimisho........................................................................................................ 99

SURA YA NNE ................................................................................................. 100

CHANZO CHA MAKOSA YA KISARUFI YA WANAFUNZI NA MIKAKATI YA KUYASHUGHULIKIA.............................................................. 100

4.0 Utangulizi....................................................................................................... 100

4.1 Chanzo cha makosa ya kisarufi ya wanafunzi ............................................ 100

4.1.1 Uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu............................................. 101

4.1.2 Ujumuishaji mno......................................................................................... 104

4.1.3 Uhamishaji wa ufundishaji .......................................................................... 105

4.1.4 Tafsiri............................................................................................................ 108

4.1.5 Kutomakinika kwa wanafunzi ..................................................................... 110

4.2 Mikakati ya kuyashughulikia makosa ya kisarufi ya wanafunzi .................. 112

4.2.1 Utangamano wa mwalimu na wanafunzi.................................................... 113

4.2.2 Wanafunzi kushirikishwa katika kukosoana............................................... 114

4.2.3 Mwalimu kutambua chanzo cha kosa la mwanafunzi na kumwelekeza.... 114

4.2.4 Mwalimu kujitayarisha vilivyo kabla ya somo .......................................... 115

4.2.5 Matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa ...................................................... 118

4.2.6 Ufundishaji wa Kiswahili kwa mwelekeo wa Uchanganuzi Linganuzi .... 120

4.2.7 Kutahadharisha wanafunzi dhidi ya tafsiri sisisi kutoka $L_1$ hadi $L_2$ .......... 120
4.3 Hitimisho.......... 121
SURA YA TANO.......... 122
HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.......... 122
5.0 Utangulizi.......... 122
5.1 Muhtasari wa Utafiti .......... 122
5.2 Matokeo ya Utafiti .......... 124
5.3 Changamoto za utafiti .......... 126
5.4 Mapendekezo .......... 127
5.5 Hitimisho.......... 128
Marejeleo .......... 129
Kiambatisho 1: Hojaji ya wanafunzi.......... 134
Kambatisho 2: Jaribio la wanafunzi.......... 135
Kiambatisho 3: Kiongozi cha mahojiano ya wanafunzi .......... 138
Kiambatisho 4: Kiongozi cha mahojiano na walimu.......... 139
Kiambatisho 5: Barua ya shule ya kuidhinisha utafiti .......... 140
Kiambatisho 6: Kibali cha NACOSTI .......... 141

## ORODHA YA MAJEDWALI

1.1 Matokeo ya somo la Kiswahili ya Kaunti ya Taita /Taveta (KCPE 2011- 2015) ………………………………...........................3

2.1 Ngeli za nomino za Kiswahili Kimofolojia.............................................30

2.2 Ngeli za nomino za Kiswahili kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi......33

2.3 Vivumishi vimilikishi...................................................................................37

2.4 Vivumishi vya pekee ...................................................................................39

2.5 Vivumishi vya idadi ....................................................................................41

2.6 Ngeli za nomino za Kitaita kimofolojia ..................................................45

2.7 Ngeli za nomino za Kitaita Kisintaksia....................................................47

2.8 Vivumishi vya sifa .......................................................................................50

2.9 Vivumishi vimilikishi...................................................................................51

2.10 Vivumishi viulizi ....................................................................................52

2.11 Vivumishi vya ‘A’ Unganifu .................................................................54

2.12 Vivumishi vya pekee ...................................................................................55

2.13 Vivumishi vya idadi ....................................................................................56

2.14 Ngeli za nomino kimofolojia katika Kiswahili na Kitaita.........................59

2.15 Vipatanishi vya ngeli za nomino za Kiswahili na Kitaita ........................60

3.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa ..........................................69

3.2 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha kumiliki ..................................72

3.3 Nomino na kivumishi kiashiria..............................................................75

3.4 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi ........................................77

3.5 Upatanishi wa nomino na kiulizi ............................................................80

3.6 Nomino na vivumishi vya pekee ............................................................81
3.7 Urejeshi wa nomino katika vitenzi...........................................................84
3.8 Viwango vya makosa katika insha ..........................................................88
3.9 Viwango vya makosa ya wanafunzi katika masimulizi............................89
4.1 Kauli potofu za wanafunzi zilizotokana na uhamishaji wa vipengele vya kisarufi .........................................................................................101
4.2 Makosa ya kisarufi yaliyokosa kuangaziwa katika usahihishaji..............106
4.3 Kauli za wanafunzi zilizotafsiriwa kutoka $L_1$ ........................................108
4.4 Wanafunzi waliofanya makosa ya uakifishaji .......................................110
4.5 Upotofu wa kisarufi unaotokana na athari za kukaribiana kimaumbo kwa vipengele vya kisarufi vya $L_1$ na $L_2$ ...............................................113
4.6 Aina za vitabu vilivyotumiwa na walimu katika maandalizi ya ufundishaji wa sarufi ...................................................................116
4.7 Maoni ya walimu kuhusu kitabu cha Kiswahili Kwa darasa la Saba......117
4.8 Mchango wa walimu kwa vitabu vya wanafunzi vya ziada..................119

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli wa mada

Kiswahili kimekuwa lugha muhimu sana tangu enzi za ukoloni katika kuendeleza mawasiliano. Baada ya uhuru, kutokana na maoni na mapendekezo ya tume mbalimbali za elimu zilizowahi kuundwa nchini Kenya, Kiswahili kimepewa dhima ya kufundishwa na kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya darasa la nane (KCPE) na kidato cha nne (KCSE) kama somo la lazima. Aidha, Kiswahili kinafunzwa na kutahiniwa katika mataifa mbalimbali ya Afrika Mashariki.

Mbali na matumizi haya ya Kiswahili katika uwanja wa elimu, Kiswahili pia kimeidhinishwa kikatiba kama lugha ya taifa na lugha rasmi katika taifa la Kenya na Tanzania. Aidha, Kiswahili ni lugha ya kimataifa ambayo inatumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa watu wa mataifa mbalimbali. Isitoshe, hutumika katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, biashara, kortini na katika vyombo vya habari. Pia, vyuo vingi barani Afrika, Ulaya, Asia na Marekani vinafundisha somo la Kiswahili.

Kulingana na Odeo na Maina (2008), Kiswahili ni lugha yenye lahaja nyingi ijapokuwa hakuna makubaliano kamili kuhusu idadi ya lahaja za Kiswahili na mipaka yake. Kiswahili Sanifu kimetokana na lahaja ya Kiunguja. Kwa kuzingatia hili, kuna haja ya kufunza Kiswahili Sanifu ili kuweze kuwepo na

maelewano ya kimawasiliano miongoni mwa watumizi wake mbalimbali. Jambo hili ndilo lililotupa mchocheo wa kuchunguza juu ya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita ambao wanajifunza Kiswahili Sanifu.

Ijapokuwa lugha ya kwanza ($L_1$) ya Wataita ni Kitaita, watoto wengi Wataita huongea lugha ya Kiswahili sambamba na Kitaita katika mazingira ya nyumbani; hasa katika hali ya kubadilisha msimbo. Hata hivyo, Kiswahili Sanifu ni lugha ya pili kwao. Mara nyingi wanafunzi wanaosoma Kiswahili Sanifu hukumbwa na matatizo wanapokizungumza na kukitumia na hufanya makosa mathalani ya kimatamshi, kisarufi na kimsamiati. Norrish (1983) anafafanua kosa katika lugha kama mfumo potofu kwa wanaojifunza lugha unaohusiana na sarufi, msamiati au matamshi ya lugha hiyo. Hata hivyo anadai kuwa kosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili ni sehemu muhimu katika kujifunza lugha hiyo. Naye Lado (1957) anashikilia kuwa makosa ya ujifunzaji lugha huashiria matatizo waliyo nayo wanaojifunza lugha kuhusiana na vipengele fulani vya lugha hiyo mathalani sarufi, matamshi na msamiati. Kwa kuzingatia haya, uchunguzi wetu ulichunguza chanzo cha makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu.

### 1.1 Suala la utafiti

Utafiti huu ulichochewa na matokeo yasiyoridhisha katika utendaji wa somo la Kiswahili katika kaunti ya Taita / Taveta kama inavyodhihirika katika mitihani ya

kitaifa (KCPE). Hili linabainika wazi katika Jedwali lifuatalo linaloonyesha matokeo ya miaka mitano mtawalia.

**Jedwali 1.1: Matokeo ya somo la Kiswahili ya Kaunti la Taita/Taveta (KCPE 2011-2015)**

| Mwaka | Alama ya wastani |
|---|---|
| 2011 | 52.76 |
| 2012 | 47.47 |
| 2013 | 48.01 |
| 2014 | 44.75 |
| 2015 | 47.16 |

Asili: Afisi ya Wizara ya Elimu, Kaunti ya Taita/Taveta, 2016

Kwa kuzingatia matokeo haya, ni dhahiri kuwa kuanzia 2012 - 2015 alama ya wastani katika somo la Kiswahili ilikuwa chini ya 50. Hii inamaanisha kuwa kumekuwa na wanafunzi wengi sana ambao wamekuwa wakipata alama za chini ya asilimia 50 ikilinganishwa na waliopata asilimia 50 kwenda juu. Bila shaka kutokana na matokeo haya ni wazi kuwa kuna makosa ambayo wanafunzi hufanya katika mtihani wao yanayochangia matokeo haya yasiyoridhisha kwa mfano, ya hijai, kimsamiati na ya kisarufi.

Utafiti ulilenga kimaksudi kuchunguza makosa ya kisarufi ambayo wanafunzi Wataita hufanya wanapojifunza Kiswahili Sanifu.Tulichunguza chanzo cha makosa haya na hasa iwapo lugha ya Kitaita inachangia kutokea kwa makosa hayo – $L_1$ ya wanafunzi inaweza kuwa na athari hasi au chanya katika ujifunzaji

wa $L_2$. Makosa ya kisarufi katika ujifunzaji wa $L_2$ yanaweza kusababishwa na uvunjaji wa kanuni za kisarufi zinazohusiana na vipengele vyake mbalimbali yaani, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki.

Utafiti ulidhamiria kuchunguza chanzo cha ugumu wa wanafunzi hawa katika kujifunza Kiswahili Sanifu. Maoni yanatolewa kwamba si rahisi kukadiria viwango vya ugumu katika kujifunza vipengele mbalimbali vya lugha kwani, ugumu hutegemea mtazamo na uwezo wa mwanafunzi husika. Ugumu huo hauwezi kukadiriwa kwa kuzirejelea tu zile tofauti za kiisimu zinazojitokeza kati ya $L_1$ na $L_2$. Littlewood (1984:19) anashikilia kwamba 'tofauti za kiisimu' na 'ugumu wa kujifunza' si dhana zinazofanana. Anasema, dhana ya kwanza inatokana na maelezo ya kiisimu na ya pili na mifanyiko ya kisaikolojia. Kwa hivyo, hakuna sababu yoyote ya kuonyesha kwamba dhana hizi zinalingana. Kwa kuzingatia hili, utafiti wetu ulilenga pia kuchunguza vyanzo tofauti vya makosa yao ya kisarufi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali.

## 1. 2 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:

1. Kubainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi katika kujifunza Kiswahili Sanifu.
2. Kuainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi.

3. Kuchunguza uhusiano uliopo kati ya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita na ya ubashiri wa UL.
4. Kubaini mbinu mwafaka za kuyakabili makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

1. Ni makosa gani ya kisarufi yanayobainika katika data za utumizi wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa wanafunzi Wataita?
2. Ni aina gani za makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi wanapojifunza Kiswahili Sanifu?
3. Je, kuna uhusiano gani kati ya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita na yale yanayobashiriwa na UL?
4. Je, ni mbinu zipi zinazoweza kutumika ili kushughulikia makosa hayo?

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Kiswahili ni lugha yenye dhima na umuhimu mkubwa katika kuunganisha watu kutoka jamii mbalimbali. Ikiwa lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya, kuna haja ya kila mwananchi kuweza kuitumia kwa njia sahihi ili kuwasiliana na wengine bila kuvuruga ujumbe. Ili watumizi wake waweze kufanikisha mawasiliano yao bila tashwishi yoyote lazima kanuni zote za kisarufi za lugha hii ziweze kuzingatiwa. Hivyo basi ni muhimu kufanya uchunguzi kabambe kuhusu

matatizo yoyote ya kisarufi ambayo huenda yakawakabili watumizi wake kwani Kiswahili Sanifu ni $L_2$ ya watu wengi.

Corder (1981) ameeleza sababu mbili zinazofanya uchanganuzi wa matatizo ya wanafunzi wa $L_2$ kuwa muhimu: Sababu za kiufundishaji zinazohusu uelewaji mzuri wa aina za matatizo yanayowakabili kabla ya kutafiti mbinu za kuyaondoa na sababu za kinadharia zinazopendekeza kuwa uchunguzi wa matatizo ya mwanafunzi ni sehemu ya utaratibu wa kuchunguza lugha ya mwanafunzi; jambo ambalo ni muhimu katika kuelewa mchakato wa ujifunzaji wa $L_2$. Hivyo basi, utafiti huu ulidhamiria kuchanganua aina mbalimbali za makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wanapojifunza Kiswahili Sanifu.Hili lingesaidia kupendekeza mbinu mwafaka za kuyakabili.

Sababu nyingine ya kuichagua mada hii ilikuwa ni kuchunguza ikiwa ubashiri wa Uchanganuzi Linganuzi (UL) kuhusu matatizo ya wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu, ulikuwa wa kweli. Hii ni kutokana na madai ya Corder (1967) aliyenukuliwa na James (1971) akisema kuwa UL inaelekea kubashiri matatizo mengine ambayo hayapo. Utafiti huu basi ulilenga kuchunguza ikiwa Kitaita huchangia kwa vyovyote makosa ya kisarufi kwa wanafunzi Wataita kwani licha ya kuwa lugha hizi zote ni za Kibantu, zina upekee fulani. Uainishaji wa Guthrie (1948) ulikiweka Kiswahili katika kundi la G la lugha za Kibantu na Kitaita kikawekwa katika lile la E.

Matokeo ya uchunguzi yalinuiwa kutumika kutoa maelekezo mwafaka kwa walimu kuhusu matatizo ya kisarufi yanayowakabili wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu na jinsi ya kuyasuluhisha. Aidha, uchunguzi ungewaelekeza kutambua mbinu zinazofaa kutumika katika ufundishaji wa vipengele mbalimbali vya lugha hii.

Kwa upande wa wanafunzi ambao hasa ndio waathiriwa, ungewasaidia kuelewa ni matatizo ya aina gani wanayoweza kukumbana nayo katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu kama $L_2$ na hivyo kuweza kukabiliana nayo. Wakijua matatizo yanayowakabili, bila shaka watamakinika zaidi katika maongezi au maandishi yao ya Kiswahili Sanifu.

Aidha, matokeo na mapendekezo ya utafiti huu yamenuiwa kutoa maelekezi kwa washikadau mbalimbali wa elimu katika jimbo la Taita/Taveta. Yamelenga kuwawezesha kujua ni vipengele gani vya kisarufi vingepaswa kushughulikiwa kuboresha matokeo ya Kiswahili hasa wanapoandaa warsha za walimu wa Kiswahili.

Sababu nyingine ya kutaka kushughulikia mada hii ni kuwa japo tafiti nyingi zimefanywa kuchunguza matatizo ya wanafunzi kutoka jamii mbalimbali wanaojifunza Kiswahili Sanifu kama; $L_2$ marejeleo ya maandishi mbalimbali yaliyofanywa, hayakuthibitisha kuwepo kwa utafiti wowote ambao ulilenga hasa

wanafunzi wa jamii ya Wataita. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo. Matokeo yake yalinuiwa kuwafaidi wanajamii husika na hasa wanafunzi katika kurekebisha makosa ya kisarufi wanayofanya.

## 1.5 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu umo katika taaluma ya isimu tumikizi ambayo ni taaluma inayohusisha nadharia na mbinu mbalimbali za kiisimu katika kutatua matatizo yanayojitokeza katika ufafanuzi wa lugha, hasa katika ufundishaji wa lugha za kigeni (Massamba, 2004). Kwa kuzingatia mada ya utafiti, dhana ya sarufi imefafanuliwa kama kanuni, sheria au taratibu zinazotawala viwango mbalimbali vya lugha fulani - fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Hivyo basi kulingana na maelezo haya, makosa yalitambuliwa kutokana na ukiukaji wa kanuni za kisarufi katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Utafiti huu ulichunguza makosa yanayohusu kategoria zifuatazo za kisarufi: nomino, vivumishi na virejeshi. Kategoria hizi ziliteuliwa kimaksudi ili kukidhi matakwa ya mhimili wa Nadharia ya UL unaopendekeza kuteuliwa kwa kategoria za lugha zitakazolinganishwa.

Utafiti nyanjani ulifanywa katika taarafa ya Wundanyi katika Kaunti ya Taita/Taveta. Eneo hili liliteuliwa kimaksudi kwani ni makazi asilia ya Wataita kwa hivyo ilikuwa rahisi kupata sampuli faafu ya utafiti. Utafiti ulihusisha

wanafunzi wa shule za msingi wa darasa la saba ambao wanachukuliwa kuwa na umilisi wa kutosha wa Kiswahili. Shule zilizoshirikishwa katika uchunguzi zilihusisha za umma na moja ya kibinafsi. Shule zote zilikuwa za mseto na za kutwa. Hii ni kwa sababu hakukuwa na shule yoyote ya jinsia moja au ya bweni. Lahaja ya Kitaita iliyotumiwa katika utafiti huu ni ya Kiwerugha.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Usomaji wa vitabu na tasnifu zilizowahi kuandikwa ulidhihirisha kuwa tafiti nyingi zimefanywa zinazohusiana na ujifunzaji wa $L_{2.}$ Hata hivyo, kwa vile ambavyo uwanja wa lugha ulivyo mpana, mambo yanayosisitizwa katika utafiti mmoja hutofautiana kwa njia moja au nyingine na yale yaliyoshughulikiwa katika kazi nyingine. Aidha, watafiti mbalimbali hutumia mielekeo na mikabala tofauti kutekeleza kazi zao. Kwa sababu hii kuna maeneo ambayo bado yanahitaji kushughulikiwa ili kukamilisha kazi zilizotangulia utafiti huu. Baadhi ya tafiti hizi zililenga kuonyesha maingiliano ya lugha kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya lugha mathalani fonolojia, mofolojia, sintaksia na kadhalika. Sehemu hii ilishughulikia kazi zilizoandikwa kuhusiana na ujifunzaji wa $L_2$ kwa jumla na zile zilizoshughulikia ujifunzaji wa Kiswahili kama $L_2$. Lengo kuu likiwa ni kuangazia uhusiano uliopo kati ya kazi hii na zilizotangulia.

Lado (1957) akizungumzia nadharia ya Uchanagnuzi Linganuzi alionyesha kuwa katika kuchunguza ujifunzaji wa $L_{2,}$ ni muhimu kuangazia miundo fanani na ile

inayotofautiana kati ya $L_1$ na $L_2$. Ni lazima miundo ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na ya kitamaduni ichunguzwe ili kuweza kubashiri miundo inayoweza kurahisisha au kutatiza ujifunzaji wa $L_2$. Anaendelea kusema kuwa inafaa kukabiliana na tatizo la uhamishaji. Kwa sababu hii, anahimiza walimu kuweza kufundisha vipengele vinavyotofautiana kwani ndio chanzo cha makosa yanayojitokeza katika $L_2$. Kwa maoni yake, matatizo ya wanafunzi yanatofautiana kadri lugha zao za kwanza zinavyotofautiana. Utafiti huu umetufaa kwa kutuelekeza kinadharia.

Utafiti mwingine uliotuelekeza kinadharia ni wa Ellis (1985, 1994) aliyejadili kwa kina nadharia mbalimbali za ujifunzaji wa $L_2$ na kutoa maelezo ya kimsingi ya kuzingatiwa katika ujifunzaji wa $L_2$. Katika utafiti huu, kazi hii ilitufaa zaidi katika kutupa mwelekeo wa kinadharia na kubainisha mipaka ya utafiti huu.

Mbaabu (1985) alishughulikia maingiliano ya lugha ya kwanza katika Kiswahili bila kulenga kikundi cha wanafunzi. Alichunguza athari za lugha za Kiluo, Kiluhya, Kikamba, Kimeru, Kikalenjin, Kikuria na Kikuyu kama $L_1$ katika ujifunzaji wa Kiswahili. Aliona maingiliano ya lugha hizi huathiri wanaojifunza Kiswahili. Utafiti huu ni tofauti kwani ulihusu wanafunzi na tulijikita katika jamii mahususi ya Wataita.

Musau (1993) alishughulikia ujifunzaji wa kifonolojia kwa wanafunzi Wanandi, Wakamba, Wakikuyu, Wabukusu, Wasomali, Wamasai na Waluo wa shule za msingi nchini Kenya na kubainisha makosa yanayojitokeza kwa makundi hayo tofauti. Utafiti huu ulibainisha kuwa wanafunzi hawa wanapojifunza fonolojia ya Kiswahili wanatatizika kutokana na msingi walio nao wa $L_1$ na hili linaleta uhamishaji na ujumuishaji miongoni mwao ili kujiundia lugha kadirifu au fonolojia ya kati ya lugha za mama na Kiswahili. Tofauti kubwa kati ya tafiti hizi mbili ni kuwa, wa Musau ulizingatia uchunguzi wa makosa ya kifonolojia na huu ulihusu makosa ya kisarufi.

Mudhune (1994) alifanya uchanganuzi linganuzi wa mofosintaksia ya Kiswahili kwa wanafunzi Wajaluo na kudhihirisha kwamba tofauti za kisarufi kati ya Kiswahili na Kiluo ndicho chanzo cha makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi hao. Utafiti huo unalingana na huu kinadharia kwa kiasi fulani kwani zote zinaendeshwa na nadharia ya UL ila zinatofautiana kwa $L_1$ zinazozingatia.

Vilevile, Mbaabu (1995) alijishughulisha na usahihishaji wa makosa yatokeayo mara kwa mara miongoni mwa wanaojaribu kuzungumza Kiswahili Sanifu. Alibainisha kuwa makosa yanayofanywa huweza kuwa ya kimatamshi, kisarufi, kisemantiki na kimofolojia. Aliangazia makosa ya kisarufi yanayohusu kuchanganya viambishi vya ngeli tofauti na yale yatokanayo na virejeshi. Nayo makosa ya kisemantiki yanatokana na upungufu wa msamiati pamoja na athari za

$L_l$. Utafiti huu unahusiana na huu kwani ulichunguza makosa yatokanayo na ukiukaji wa matumizi ya viambishi vya ngeli za nomino na yale yatokanayo na virejeshi. Tofauti ni kuwa huu ulijikita katika matatizo ya kisarufi kwa wanafunzi wa jamii mahususi ya Wataita.

Hali kadhalika, Onyango (1997) alifanya utafiti kuhusu uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wa Kinyala ambapo alibainisha tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa tofauti hizi ndizo chanzo cha makosa ya wanafunzi wa Kinyala katika kujifunza Kiswahili Sanifu kama $L_2$. Kazi hizi zinahusiana kinadharia.

Mwaliwa (2000) pia alifanya utafiti kuhusu ulinganishi wa mofolojia ya Kiswahili na Kitaita. Katika utafiti huu aliweza kutofautisha fonimu na ngeli za Kitaita na za Kiswahili. Utafiti huu ulifaa kwani ulishughulikia lugha ya Kitaita sawa na huu ijapokuwa zinatofautiana kimada.

Naye Chepkwony (2011) katika utafiti wake juu ya matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kikipsigis wanaojifunza Kiswahili Sanifu, alibainisha kuwa utaratibu wa muundo wa sentensi za Kiswahili na ule wa Kikipsigis ni tofauti kwani lugha hii si lugha ya Kibantu. Kwa hivyo, alionyesha kuwa makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wengi hutokana na athari za lugha ya kwanza. Utafiti huu ulizingatia nadharia za UL na Lugha Kadirifu (LK). Kwa

hivyo, unatofautiana na huu kinadharia, kwani ulitumia LK na huu umetumia UM.

Obara (2014) alichanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayodhihirika katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wanaozungumza lugha ya Ekegusi kama $L_1$. Katika utafiti wake alishughulikia mchango wa lugha ya Ekegusii kwa makosa hayo. Kwa mujibu wa utafiti huu, Lugha ya Ekegusii ilichangia kutokea kwa makosa haya. Utafiti huu unahusiana na huu kinadharia kwani zote zimetumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UL). Tofauti kati yao ni kuwa huu ulishirikisha pia nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) ilhali huo ulitumia nadharia ya Lugha Kadirifu. Isitoshe, zinatofautiana kuzingatia $L_1$ zilizohusishwa.

Utafiti mwingine unaohusiana na huu ni ule uliofanywa na Ntawiyanga (2015) kuhusu Changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Kupitia kazi hii, makundi saba ya makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi yalidhihirishwa: makosa ya uchopekaji wa vipashio katika tungo, udondoshaji wa vipashio katika tungo, mchanganyiko wa viambishi na matumizi ya viambishi visivyofaa, mchanganyiko wa aina mbalimbali za maneno, uradidi wa vipashio usiofaa katika tungo, uhamishaji wa vipashio, mpangilio mbaya wa maneno katika tungo na uundaji wa sentensi ndefu. Utafiti huu ulifaa kazi hii kwani zote zinahusiana na makosa ya kisarufi.

Tofauti ni kuwa uliongozwa na nadharia za UM na LK ilhali huu uliongozwa na UL na UM.

Kwa mujibu wa marejeleo yaliyofanywa kuhusiana na yaliyoandikwa kuhusu mada, ilikuwa dhahiri kuwa kulikuwa na pengo kwani hakukuwa na ithibati ya utafiti wowote uliofanywa kuchunguza chanzo cha makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi Wataita. Aidha, utafiti huu unatofautiana na nyingine kwani hawa wanafunzi waliolengwa licha ya kuwa Kiswahili ni $L_2$ kwao, aghalabu hukizungumza sambamba na $L_1$ katika mazingira yao ya nyumbani. Kwa hivyo, wao huwa wana umilisi wa Kiswahili wa kiwango fulani hata kabla hawajajiunga na shule. Hata hivyo, Kiswahili kwao si $L_1$ bali ni $L_2$.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto: Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) na nadharia ya Uchanganuzi makosa (UM). Nadharia UL ilisaidia kubainisha ikiwa kutofautiana na kufanana kiisimu baina ya Kiswahili Sanifu na Kitaita kulichangia makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi. Nayo ya UM ilitumika kubainisha makosa mbalimbali ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi na vyanzo vyao, na mikakati ya kuyakabili.

### 1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL)

Nadharia hii ya UL imeshughulikiwa na wanaisimu mbalimbali wakiwemo Lado (1957), James (1980), Van Els na wengine (1984), Ellis (1985) miongoni mwa

wengine. Kwa mujibu wa James (1980), UL ni uchanganuzi wa kiisimu unaohusisha ulinganishaji wa lugha mbili. UL hujihusisha na kuchunguza lugha kibinafsi na pia dhana ya lugha kijumla.

Nadharia hii inahusu upekee wa lugha na ulinganishaji wa lugha hasa kwa kuchunguza zile tofauti zilizoko kati ya lugha badala ya vile lugha husika zinavyofanana. Isitoshe, UL huchunguza lugha vile ilivyo katika kipindi fulani cha wakati. Katika kuchunguza lugha kihistoria, UL huchunguza vile mtu anavyojifunza $L_2$ kiwakati. Kawaida UL huchunguza kwa kuhusisha lugha mbili kwani huchukulia kuwa lugha zinaweza kulinganishwa. Hii ina maana kuwa UL huchunguza lugha katika kiwango cha mtu binafsi kwa kuchunguza jinsi mzungumzaji anavyoendelea kuimudu $L_2$.

Uchanganuzi wa UL pia unahusisha maswala ya kisaikolojia kwani huchunguza dhana ya mwingiliano wa kimatamshi, kisarufi na kadhalika. Athari hizi husababishwa na mzungumzaji kuingiza sauti na maneno ya lugha nyingine. Hivyo basi, UL inahusu namna $L_1$ inavyomwathiri mwanafunzi wa $L_2$ kimatamshi, kisarufi na kisemantiki. Athari hizo zinaweza kutatiza au kurahisisha jitihada zake za kujifunza $L_2$.

Kwa mujibu wa Mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi Utaratibu unaofuatwa katika kuchanganua vipashio vya lugha ni kuzilinganisha na

kuzitofautisha ili kudhihirisha namna zinavyofanana na kutofautiana. Ellis (1985) amezitambua hatua nne zinazozingatiwa katika utaratibu wa UL kama ifuatavyo:

1. Maelezo mwafaka ya lugha mbili husika.
2. Uamuzi kuhusu vipengele vya lugha vitakavyolinganishwa.
3. Kuvifananisha na kuvitofautisha vipengele hivyo katika lugha hizo mbili.
4. Ubashiri wa sehemu fulani za lugha ambazo huenda zikasababisha makosa.

Kwa vile ambavyo nadharia ya UL haiwezi kubashiri na kuyaeleza makosa yote ya mwanafunzi, utafiti huu ulizingatia pia nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM). Nadharia hii ilituwezesha kuyatambua makosa mengine ambayo hayatokani na $L_1$ na hata kuweza kueleza maumbo yao halisi. Vilevile UM ilituelekeza kujua ni jinsi gani matatizo ya kisarufi yanayowakabili wanafunzi husika yanaweza kushughulikiwa.

### 1.7.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM)

Nadharia hii ya UM katika ujifunzaji wa $L_2$ ilizungumziwa na Corder (1971). Inajumuisha seti za kanuni zinazotumiwa kuyatambua, kuyakinisha na kufafanua makosa ya wanafunzi katika maandishi na uzungumzaji wa $L_2$.

Pia inaeleza ni jinsi gani makosa yanaweza kushughulikiwa. Nadharia ya UM inasistiza mbinu za kuichunguza lugha ya mwanafunzi. Katika nadharia ya UM,

makosa huchukuliwa kama ishara kuwa mwanafunzi anajaribu kujifunza na kuelewa mfumo wa lugha lengwa (LL). Kwa hivyo, nadharia ya UM inampatia mwanafunzi nafasi ya kutosha katika ujifunzaji kwa kuchunguza makosa anayoyafanya katika ujifunzaji wake.

UM inaelekeza ni kwa jinsi gani makosa ya wanafunzi yanavyoweza kushughulikiwa. Nadharia hii ya UM inadai kuwa baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza $L_2$ hutokana na athari ya $L_1$. Makosa hayo yanaweza kuainishwa kulingana na kiwango cha lugha na kwa hivyo kuna makosa kama vile ya kifonolojia, kimsamiati au kileksia, kisintaksia na kimofolojia. Aidha, makosa hayo yanaweza kuchunguzwa kulingana na kiasi kinachoweza kutatiza mawasiliano. Kuna yale yanaweza na yale yasiyoweza kukwamisha mawasiliano. Nadharia ya UM inaweza kutoa picha ya aina ya matatizo yanayowakumba wanafunzi (Norrish, 1983). Utafiti kama huo ukifanywa unaweza kusaidia katika kuandika miongozo ya masomo. Pia, UM inatoa mwangaza kuhusu mbinu anazotumia mwanafunzi ili kuyaepuka matatizo hayo katika kujifunza lugha ya pili (Corder, 1974).

Utafiti wetu ulizingatia mihimili mitano ifuatayo ya nadharia ya UM kama inavyofafanuliwa na Ellis (1994):

1. Ukusanyaji wa data. Katika hatua hii data hukusanywa kupitia njia ya maandishi na masimulizi kwani makosa ya kimasimulizi na yale ya

kimaandishi huweza kutofautiana ikizingatiwa kuwa watu mara nyingi huwa makini hasa wanapoandika kuliko wanavyoweza kufanya wanapozungumza.

2. Kubainisha makosa: Hapa mtafiti huyabainisha makosa baada ya kupata data kutoka kwa lugha ya mwanafunzi. Ubainishaji wa data humwezesha mtafiti kuamua mapema mambo muhimu au sifa zinazoyabainisha makosa ya mwanafunzi. Pili, mtafiti huweza kujiwekea kanuni za kuzingatia katika uchunguzi wake wa kuyabainisha makosa. Tatu, uamuzi hufanywa kwa kuzingatia makosa yaliyo bayana na yale yasiyo bayana. Hayo ya kwanza hutokea pale ambapo mwanafunzi anafanya makosa ya kiumilisi na hayo ya pili huhusu fani zinazodhihirishwa kama makosa lakini zikawa tofauti na kile kilichomo bongoni au akilini mwa mwanafunzi.
3. Kufafanua makosa. Kulingana na Ellis (1994), maelezo kuhusu makosa ya mwanafunzi yanaleta ulinganishaji wa semi za mwanafunzi na miundo inayopaswa kuzingatiwa katika lugha lengwa. Mara nyingi hali hii huambatana sana na uainishaji wa makosa yaliyobainishwa katika hatua iliyotangulia. Ufafanuzi wa makosa huambatana na uainishaji wake pale ambapo makosa hupangwa katika kategoria tofaufi kulingana na vigezo alivyojiwekea mtafiti. Vilevile, katika hali hii ya ufafanuzi wa makosa ya mwanafunzi ndipo mtafiti huweza kuonyesha pia kiwango cha makosa hayo ili kukifanyia uchunguzi wa kina katika hatua inayofuata.

4. Kueleza makosa. Hatua hii inahusisha kueleza makosa yaliyobainishwa na kufafanuliwa. Ellis (1994) anadhihirisha kuwa kuyaeleza makosa kunachangia sana katika kuonyesha chanzo cha makosa hayo. Kwa hivyo, uchanganuzi makosa unaleta uwezo mkubwa wa kupata maelezo ya makosa ya mwanafunzi wa $L_2$ hasa kwa kuzingatia vipengele viwili: kipengele cha maswala ya ndani ya lugha mahususi na cha maingiliano ya lugha. Kwa kuzingatia mwingiliano wa lugha, makosa yanaweza kutokana na lugha ya kwanza kwani yanahusisha mifumo ya lugha tofauti. Nayo makosa ya maswala ya ndani ya lugha hujitokeza wakati yanapotokana na lugha yenyewe inayofunzwa au inayochunguzwa kama vile kosa la ujumuishaji wa baadhi ya kanuni za kisarufi anazozimudu mwanafunzi.
5. Kutathmini makosa. Hatua hii ya kutathmini makosa ni jambo linalohusiana na kuchunguza athari za makosa kwa mwanafunzi anayetafitiwa kwa ajili ya kuboresha mikakati ya ufundishaji wa lugha. Kwa hivyo, ni lazima kuangalia upande wa mwanafunzi anayejifunza lugha hiyo ili kujua kama ni mzawa wa lugha hiyo au la. Vilevile, umahiri wa wanaohusika katika ufunzaji kama vile walimu unazingatiwa na hali kadhalika kuchunguza ikiwa maamuzi yanayofanywa yanalenga kiini au kiwango cha makosa husika. Isitoshe, sababu za utokeaji wa makosa fulani zinaangaliwa pia ili kutambua uzito wa makosa fulani yakilinganishwa na makosa yote yaliyobainishwa. Hapa ndipo tunapata kuwa njia za kuepuka makosa hayo huweza kupendekezwa kama

suluhisho kwa makosa yaliyobainishwa. Hatua hizi zinadhihirisha kwamba, nadharia ya UM huweza kuangazia kuhusu aina ya matatizo yanayowakumba wanafunzi wa $L_2$.

**1.8 Mbinu za utafiti**

Uchunguzi wetu nyanjani ulijumuisha vipengele mbalimbali ikiwa ni pamoja na vya usampulishaji, maadili ya utafiti, muundo wa utafiti, vifaa vya utafiti, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Data zilizokusanywa nyanjani zilitumika kubainisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi Wataita katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu.

**1.8.1 Muundo wa utafiti**

Muundo wa utafiti, kulingana na Orodho (2009), ni ile mikakati inayotumika kuzua au kujibu maswali kuhusu maswala ya utafiti. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ambao hutumia mbinu ya kuuliza maswali katika ukusanyaji data.

**1.8.2 Maadili ya Utafiti**

Utafiti nyanjani ulitekelezwa baada ya mtafiti kupata barua ya kuidhinisha utafiti

kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na shirika la Nacosti. Utafiti ulifanywa kwa kuzingatia maadili ya utafiti ili kuepusha wote walioshirikishwa na athari zozote hasi ambazo zingeweza kutokana na shughuli za ukusanyaji data. Kwa kuzingatia hili, watafitiwa walihakikishiwa kuwa habari zote ambazo wangetoa

hazingetumika kuwaharibia majina au mahusianao yao na watu wengine. Habari walizotoa ziliwekwa kuwa siri kati yao na mtafiti.

Maadili ya utafiti yalizingatiwa pia wakati wa kukusanya data kwa kutumia hojaji na karatasi za mazoezi ambapo wanafunzi waliagizwa wasiandike majina yao. Aidha, wakati wa masimulizi wanafunzi walishauriwa wasiwachekelee na kuwadhihaki wenzao ambao walikuwa na shida katika kujieleza labda kwa kukosa ujasiri au kuharibu sarufi. Lengo hasa lilikuwa ni kutowavunja moyo na kutowafanya wahisi kudunishwa.

### 1.8.3 Sampuli

Kulingana na Orodho na Kombo (2002), usampulishaji ni utaratibu anaotumia mtafiti kuteua watu, mahali na vitu vya kufanyia utafiti. Katika utafiti huu, sampuli yetu ilihusisha uteuzi wa eneo la utafiti, shule na wanafunzi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka shule za msingi za Kaunti ndogo ya Wundanyi katika Kaunti ya Taita/Taveta. Sehemu hii ilichaguliwa kimaksudi kwa kuzingatia kuwa ni makazi asilia ya Wataita kwa hivyo, ilikuwa rahisi kuteua sampuli ya utafiti yenye sifa zilizotakikana.

Utafiti ulihusisha shule sita za msingi (A, B, C, D, E na F) zilizoteuliwa kutoka maeneo matatu yaliyo katika Kaunti ndogo ya Wundanyi kuzingatia kipengele

cha usampulishaji. Shule mbili ziliteuliwa kimaksudi kutoka kila eneo kwa kuzingatia utendaji wao katika somo la Kiswahili katika mtihani wa KCPE. Shule ya kwanza na ya mwisho kimatokeo kutoka kila eneo, ziliteuliwa. Lengo likiwa ni kuweza kuwa na matokeo ya uchunguzi ya kutegemewa.

Wanafunzi walioshirikishwa ni wale wanaoongea Kitaita kama $L_1$ waliokuwa darasa la saba ambao walichukuliwa kuwa na umilisi wa kutosha wa Kiswahili Sanifu. Jumla ya wanafunzi watano waliteuliwa kutoka kila shule. Idadi hii iliteuliwa kimaksudi.Wanafunzi hawa watano kutoka kila shule waliteuliwa kutumia njia ya sampuli nasibu ili kumpa kila mwanafunzi uwezekano sawa wa kuteuliwa kushiriki katika utafiti. Ili kuteua wanafunzi walioshirikishwa, karatasi tano ziliandikwa nambari moja (1) na nambari mbili (2) ikapewa karatasi nyingine kulingana na idadi ya wanafunzi waliobaki. Waliopata nambari moja ndio walioshirikishwa katika utafiti.

### 1.8.4 Mbinu zilizotumika kukusanya data

Katika utafiti huu, mbinu zilizotumiwa kuzikusanya data zetu ni pamoja na hojaji, masimulizi na ukaguzi wa insha za wanafunzi kama ifuatavyo.

#### 1.8.4.1 Hojaji

Seale (2012) anasema kuwa hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafitiwa hupewa muda wa kukaa peke yake na kujibu maswali atakayoulizwa mwenyewe.

Katika kukusanya data kutoka kwa wanafunzi, mtafiti alijumuika na watafitiwa na kuwaeleza malengo yake ya utafiti. Aliwaeleza vile ambavyo matokeo ya utafiti alionuia kufanya yangewanufaisha wote.

Vilevile aliwafahamisha kuhusu maagizo ya hojaji ambazo walijaza kama vile, kutoandika majina yao. Hatua iliyofuata ilikuwa kuwapa hojaji wajaze. Hojaji ya kwanza ilihusisha maswali ya kibinafsi kumhusu mwanafunzi. Baadhi ya maswali katika sehemu hii yalikuwa funge na mengine wazi. Maswali funge yalisaidia kupata kauli ambazo zingeaminika kumhusu mtafitiwa. Nayo wazi yangempa uhuru wa kujieleza. Hojaji ya pili ilihusisha zoezi fupi lililohusisha vipengele vya kisarufi ambavyo vilichunguzwa. Katika sehemu ya kwanza ya maswali ya zoezi hili, wanafunzi walipewa sentensi za Kitaita wazitafsiri kwa Kiswahili. Sehemu ya pili ya maswali ilijumuisha sentensi za Kiswahili ambapo walitakiwa kuzikamilisha kwa kutumia maneno au viambishi mwafaka vya upatanishi wa kisarufi. Mtafiti aliwafahamisha kuwa mazoezi ambayo walifanya hayakuwa mtihani.

Maswali ya zoezi hili yaliwezesha mtafiti kujua kiwango chao cha uhamishaji kutoka $L_l$. Aidha, ilisaidia kujua kiwango cha matumizi yao ya kanuni za sarufi ya Kiswahili walizojifunza darasani kuhusiana na upatanishiji wa kisarufi wa nomino na vitenzi, vivumishi na virejeshi.

#### 1.8.4.2 Mahojiano

Kulingana na Mugenda na Mugenda (2012), mahojiano hushirikisha mtafiti kuuliza maswali naye mhojiwa kutoa majibu. Katika utafiti huu, wahojiwa walihusishwa katika mahojiano kupitia kwa masimulizi ya hadithi. Kila mwanafunzi alipewa fursa ya kuwasimulia wengine hadithi fupi ambapo mtafiti aliuliza hadhira maswali kuhusiana na hadithi zilizosimuliwa. Jambo hili lilichochea mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa na hili lilimwezesha mtafiti kupata data ambayo alihitaji. Hadithi na mazungumzo hayo yalirekodiwa na baadaye kunakiliwa na mtafiti ili aweze kuyachunguza. Masimulizi ya hadithi yalitupatia data ya utendaji wa kimazungumzo.

#### 1.8.4.3 Ukaguzi wa insha

Ukaguzi uliofanywa ulihusisha insha ambazo wanafunzi walikuwa wamewahi kuandika na zikasahihishwa na mwalimu wao. Insha moja iliteuliwa kimaksudi kutoka kwa daftari la kila mtafitiwa na kuzipiga chapa. Baadaye, alizitumia kuchunguza aina mbalimbali za makosa. Hili lilimwezesha mtafiti kutambua makosa ambayo yalifanywa na wanafunzi katika uandishi wao kwani mara nyingi mtu huandika kwa namna tofauti na vile anavyozungumza.

### 1.8.5 Vifaa vilivyotumika kukusanya data

Utafiti huu ulitumia vifaa mbalimbali vya kukusanyia data ya utafiti ikiwa ni pamoja na hojaji, karatasi za mazoezi, kiongozi cha mahojiano na kinasa sauti.

#### 1.8.5.1 Hojaji

Katika utafiti huu, wanafunzi waliohusishwa walipewa hojaji ambapo walihitajika kutoa habari zao za kibinafsi. Maswali funge pamoja na wazi yalitumika. Maswali wazi yalitumika ili kumpa mtafitiwa uhuru wa kuandika jawabu ambalo angetaka.

#### 1.8.5.2 Karatasi za mazoezi

Karatasi hizi zilikuwa na sehemu mbili: sehemu ya maswali ya kutafsiri sentensi kutoka kwa lugha ya Kitaita hadi ya Kiswahili na ile ya kujaza nafasi zilizoachwa kwa viambishi au maneno mwafaka.

#### 1.8.5.3 Kinasa sauti

IIi kufanikisha utafiti huu, kinasa sauti kilitumika kurekodi mahojiano na kunasa hadithi ambazo zilisimuliwa na wanafunzi. Baadaye, tulinukuu mahojiano na hadithi hizo na kuzichanganua.

#### 1.8.5.4 Kiongozi cha mahojiano

Hiki kilijumuisha maswali yaliyoulizwa wanafunzi wakati wa mahojiano kuhusu hadithi zilizosimuliwa. Maswali yaliyohusika yalilenga kuchochea mjadala miongoni mwa wanafunzi ili kupata data iliyohitajika. Aidha, kulikuwa na kiongozi cha mahojiano ambacho kilijumuisha maswali mbalimbali yaliyoulizwa walimu.

### 1.8.6 Uchanganuzi wa data

Kuhusu suala la uchanganuzi wa data, Mugenda na Mugenda (2012) wanashikilia kuwa mtafiti anatakiwa kwanza kupanga data yake kwa utaratibu unaomwezesha kupata maana ya habari alizo nazo. Katika kazi hii, data ilichanganuliwa kuhusiana na makosa ya kisarufi ya wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifi na mikakati ya kuyashughulikia tukiongozwa na malengo yetu na nadharia za utafiti. Kwa hivyo, uchanganuzi wa data ulizingatia hatua zifuatazo: Kwanza, makosa yalinukuliwa kwa utaratibu maalum kisha makosa hayo yalibainishwa kwa kuzingatia kategoria za kisarufi zilizoathirika na viwango mbalimbali vya utokeaji wake kiasilimia.

Hatua ya tatu ilihusisha kuyafafanua makosa hayo na kuyaainisha. Uainishaji ulijumuisha kuweka makosa katika kategoria mbalimbali. Nayo hatua ya nne, ilihusisha kuchunguza vyanzo vya makosa na kuvitolea maelezo. Aidha, tuliyatambua yale makosa yaliyobashiriwa kwa kuzingatia nadharia ya UL. Hatua ya mwisho ilihusisha kutathmini utokeaji wa makosa na kuchunguza mikakati ya kuzingatiwa na walimu ili kuyapunguza makosa hayo ndio mapendekezo mwafaka yatolewe.

### 1.8.7 Uwasilishaji wa matokeo

Uwasilishaji wa matokeo katika utafiti huu ulifanywa kwa njia ya maelezo. Majedwali yalitumika kurekodia na kufafanulia maelezo yetu kwa kuonyesha

kiwango cha utokeaji wa makosa na idadi ya wanafunzi waliofanya makosa hayo kiasilimia. Matokeo ya data yaliwasilishwa kwa kujumuisha matokeo ya mazoezi yote ya utafiti kwa pamoja.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imejikita na utangulizi wa uchunguzi huu. Hapa tulibainisha yale mambo muhimu yaliyozingatiwa katika kuichagua mada na pia kuangazia namna utafiti ungekabiliwa ili kuyafikia madhumuni yake. Kwa jumla tumedhihirisha na kufafanua usuli wa mada ya uchunguzi, suala la utafiti, sababu zilizotufanya kuichagua mada husika, upeo na mipaka ya utafiti wetu, marejeleo kuhusu mada, nadharia zilizotuongoza na zile mbinu zilizotumika kufanyia utafiti huu.

# SURA YA PILI

## VIPENGELE VYA KISARUFI VYA KISWAHILI NA KITAITA

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, vipengele mbalimbali vya kisarufi katika lugha za Kiswahili Sanifu na Kitaita vilichunguzwaa ili kuonyesha vinavyofanana na kutofautiana kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL). Ngeli za nomino za Kiswahili na Kitaita zilibainishwa kwa kuonyesha zinavyoleta upatanishi wa kisarufi katika sentensi zitumiwapo na kategoria nyingine za maneno.

Hili lilitokana na kisio kwamba makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi hutokana na sarufi miundo fanani na tofauti iliyopo kati ya mfumo wa ngeli za nomino za Kiswahili na za Kitaita ambapo maswala ya kimofolojia, ya kisintaksia na kisemantiki huingiliana na kukamilishana kimatumizi kiasi cha kumkanganya mwanafunzi. Ulinganishaji wa vipengele hivi vya kisarufi ulisaidia katika kufanya ubashiri wa matatizo ya kisarufi ambayo yangewakumba wanafunzi Wataita katika utumizi wao wa Kiswahili Sanifu. Vipengele mbalimbali vya kisarufi katika Kiswahili na Kitaita vilivyotumiwa katika uchunguzi vilibainishwa kama ifuatavyo.

### 2.1 Kiswahili

Lugha ya Kiswahili huzungumzwa na wenyeji wa mwambao wa Afrika Mashariki kuanzia Somalia mpaka kwenye visiwa vya Komoro. Hivi sasa Kiswahili

kimeenea hadi sehemu za Bara kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Kongo Kinshasa na Jamhuri ya Kongo. Kiswahili ni lugha ya mawasiliano barani Afrika. Kiswahili kina lahaja mbalimbali ambapo Kiswahili Sanifu kimetokana na lahaja ya Kiunguja. Utafiti wetu ulizingatia Kiswahili Sanifu. Kiswahili ni mojawapo wa lugha za Kibantu na kwa hivyo, inahusisha mpangilio wa nomino katika ngeli mabalimbali kama inavyobainika katika 2.1.1.

### 2.1.1 Dhana ya ngeli za nomino za Kiswahili

Istilahi 'ngeli' imechukuliwa kutoka kabila la Kihaya (Tanzania) ambapo ina maana ya aina ya kitu. TUKI (1990) wanaeleza ngeli ya nomino kuwa, ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana. Kwa mujibu wa fasili hii, ngeli za nomino ni jumla ya majina yanayofanana kwa upatanisho wa kisarufi, na viambishi vyao vya umoja na wingi. Ngeli za Kiswahili zinaweza kuainishwa kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki (Taz. § 2.1.1.1 - 2.1.1.2).

#### 2.1.1.1 Uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia

Kulingana na Katamba (1993), mofolojia ni tawi la kiisimu linaloshughulikia miundo ya ndani au maumbo ya maneno. Kinachozingatiwa katika uainishaji huu ni viambishi awali vya nomino katika umoja na wingi. Ngeli za nomino kimofolojia huhusisha kundi moja la nomino zilizo na viambishi awali vya umoja na/au vya wingi vinavyofanana. Aidha, nomino zisizo na kiambishi awali

hata kimoja huwa na ngeli zao. Uainishaji wa ngeli kwa kuzingatia kipengele hiki cha kimofolojia umeshughulikwa na wanaisimu mbalimbali wakiwemo Kraph (1850), Steer (1865), Ashton (1944), Habwe na Karanja (2004) Polome (1967), Myachina (1981), Mbaabu (1978, 1985), Mgullu (1999), na Mohammed (2001). Jedwali 2.1 linaonyesha makundi ya ngeli za Kiswahili kwa kuzingatia utaratibu wa viambishi na tarakimu kwa mujibu wa Mbaabu (1995).

**Jedwali 2.1 Ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia**

| **Tarakimu ya ngeli** | **Viambishi (mianzo ya nomino)** | **Mifano katika sentensi** |
|---|---|---|
| 1 | M | Mtoto anakimbia.<br>Mwalimu amefika.<br>Muuguzi amefika. |
| 2 | WA | Watoto wanakimbia. |
| 3 | M | Mti tulianguka.<br>Mwembe umekatwa.<br>Muungu umekauka. |
| 4 | MI | Miti itaanguka. |
| 5 | JI | Jicho lake linaauma. |
| 6 | MA | Macho yao yanauma. |
| 7 | KI | Kiti kimenunuliwa. |
| 8 | VI | Viti vimenunuliwa. |
| 9 | N | Nguo imeshonwa. |
| 10 | N | Nguo zimeshonwa. |
| 12 | U | Utambi umekatika. |
| 13 | N | Tambi zimekatika.<br>Mbeleko zimepotea. |
| 14 | U | Ulevi unaudhi. |
| 15 | KU | Kucheza kunafaa. |
| 16 | PA/PO | Hapo pamesafishwa. |
| 17 | KU/KO | Huko kumesafishwa. |
| 18 | MU/MO | Humo mumesafishwa. |

Asili: Mbaabu (1995)

Kulingana na Jedwali 2.1, muainisho huu wa ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia huzingatia viambishi vya nomino. Baadhi ya ngeli zina alomofu zaidi ya moja kwa mfano,

a) Ngeli ya 1 ina alomofu {m, mw na mu}.

   *(2.1) mtoto {m}, mwalimu {mw} na muuguzi (mu)*

b) Ngeli ya 3 ina alomofu {m, mw na mu}

   *(2.2) mti {m}, mwembe {mw}, muungu {mu}*

c) Ngeli ya 13 ina maumbo {n} na {m}.

   *(2.3) nyuzi {n} na mbeleko {m}*

Mabadiliko haya ya kifonolojia katika ngeli ya 1 na 3 yanasababishwa na mifanyiko ya kifonolojia mathalan ya uyeyushaji na udondoshaji kwa kuzingatia aina ya sauti inayotangulia shina la nomino inayohusika. Hili linadhihirika pia katika ngeli ya 13 ya (N), inapojitokeza kwa maumbo {n} na {m} kutokana na usimilisho wa nazali ambapo nazali huathiriwa na konsonanti inayoifuata kulingana na mahali pa kuitamkia. Hivyo basi {n} itatumiwa kwenye majina yenye mashina yanayoanza kwa konsonanti ghuna kama vile {d, j na g} kama vile ndoto, njia na ngano.  Nayo alomofu {m}, hutumika kwenye majina yenye mizizi inayotanguliwa na konsonanti ghuna {b} na {v} kwa mfano, mbao na mvua.

#### 2.1.1.2 Uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili kisintaksia

Wataalamu mbalimbali wameweza kuibua taratibu tofauti tofauti za kuainisha ngeli za Kiswahili kisintaksia. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), uainishaji wa ngeli

kisintaksia huzingatia uhusiano uliopo baina ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Muainisho huu huzingatia vipatanishi vya kisarufi vya nomino vinavyowekwa kwenye vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Aidha Kapinga (1983), kufuatia kuwapo kwa matatizo yaliyodhihirika katika uainishaji wa ngeli kwa kutumia kigezo cha umoja na wingi, aliainisha ngeli kwa kuzingatia kiambishi cha upatanishi wa kisarufi. Yeye alichagua kutumia kiambishi cha upatanishi wa kisarufi ambacho huambishwa kwenye kitenzi. Jedwali 2.2 linaonyesha makundi mbalimbali ya ngeli za nomino za Kiswahili kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi.

**Jedwali 2.2 Ngeli za nomino za Kiswahili kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi**

| **Ngeli** | | **Vipatanishi** | **mifano ya nomino** | **Mifano ya sentensi** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Umoja** | **Wingi** |
| 1 | YU/A–WA | a-wa | mtu/watu,mtume/ mitume, kipofu/ vipofu, nzi/nzi, bawabu/mabawabu | Mtu (yule) **a**nakuja. | Watu (wale) wanakuja. |
| 2 | U-I | u-i | mti/miti, mwembe/miembe, mkono/mikono, | Mti (ule) umekatwa. | Miti (ile) imekatwa. |
| 3 | KI – VI | ki-vi | kikapu/vikapu, choo/vyoo, kiti/ viti | Kisu kimenolewa. | Visu vimenolewa |
| 4 | LI – YA | li-ya | duka/maduka, jicho/macho | Jicho linauma. | Macho yanauma. |
| 5 | I – ZI | i-zi | nyumba/nyumba, nguo/nguo, njia/ njia | Nyumba imebomoka. | Nyumba zimebomoka. |
| 6 | I | i-i | sukari/sukari, mvua/mvua | Sukari imemwagika. | Sukari imemwagika. |
| 7 | U-ZI | u-zi | uzi/nyuzi, ufa/nyufa | Ufa umezibwa. | Nyufa zimezibwa. |
| 8 | U | u-u | uchoyo, udaku, werevu | Udaku unaudhi. | Udaku unaudhi. |
| 9 | U-YA | u-ya | ugonjwa /magonjwa, uovu/maovu | Ugonjwa umepona. | Magonjwa yamepona. |
| 10 | YA | ya-ya | maji,maziwa | Maji yameisha. | Maji yameisha. |
| 11 | KU | Ku | kusoma, kuimba | Kusoma kunapendeza. | Kusoma kunapendeza. |
| 12 | PA | Pa | Pahali | Pahali panapendeza. | Pahali panapendeza. |
| | KU | Ku | Mahali | Mahali kunapendeza. | Mahali kunapendeza. |
| | MU | Mu | Mahali | Mahali mnapendeza. | Mahali mnapendeza. |

Asili: Kapinga (1983)

Kwa mujibu wa Jedwali hili, ni wazi kuwa kiambishi kinachopatanisha nomino na kitenzi huwa kinafanana ikiwa majina yamo katika ngeli moja kama inavyobainika katika mifano 2.4.

*(2.4)*

a. *Mtoto analala / Watoto wanalala.*
b. *Ng'ombe amekufa / Ng'ombe wamekufa.*
c. *Kipofu amefika / Vipofu wamefika.*
d. *Mti umekatwa / Miti imekatwa.*
e. *Mkono unauma / mikono inauma.*
f. *Kiatu kimeraruka /Viatu vimeraruka.*
g. *Choo kimejengwa / Vyoo vimejengwa.*
h. *Duka limefungwa / Maduka yamefungwa.*
i. *Jicho linauma /Macho yanauma.*
j. *Ubao umenunuliwa / Mbao zimenunuliwa.*
k. *Uzi umekatika / Nyuzi zimekatika.*

Mifano 2.4 (a, b na c), imo katika ngeli ya A/WA, (d) na (e) katika ngeli ya U/I huku (f) na (g) ikiwa katika ngeli ya KI/VI. Aidha mifano 2.4 (h, i) ni ya ngeli ya LI/YA na (j) na (k) ya ngeli U/ZI.

Ni dhahiri kuwa katika ngeli ya A/WA, majina yanayoanza na viambishi tofauti katika umoja na wingi yameingizwa katika kundi moja kwa kuzingatia kipatanishi *a* (umoja) na *wa* (wingi). Utaratibu wa uainishaji wa ngeli za Kiswahili kwa kuzingatia kipengele hiki cha kisintaksia kwa kiasi kikubwa umechukuliwa kuwa unakidhi haja hasa ukilinganishwa na zile nyingine.

### 2.1.2 Upatanishi wa kisarufi wa nomino na vivumishi

Upatanishi wa kisarufi ulihusu kuoanisha nomino na kategoria nyingine za

maneno katika sentensi. Nomino ndiyo inayotawala maneno mengine yote katika sentensi. Ikiwa mtu anaelewa ngeli ya nomino inayohusika, ni rahisi kuipatanisha na maneno yale mengine. Hili linarahisisha uundaji wa sentensi zilizo sahihi kisarufi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili.

Vivumishi ni mojawapo ya vipengele vya kisarufi vilivyolengwa kuchunguzwa (Taz. § 1.6). Kwa mujibu wa Steere (1969), kivumishi hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino hiyo. Vivumishi huwekwa baada ya jina linalovumishwa na huundwa kwa msingi unaoleta ukubalifu wa viambishi awali vya nomino na vile vya vivumishi vyenyewe. Kwa kuzingatia maelezo haya kuna aina zifuatazo za vivumishi: vivumishi vya sifa, vivumishi vimilikishi, vya kuuliza, vya idadi, vionyeshi/viashiria na vya pekee (-enye, -enyewe, -ote, -o-ote, -ingine na ingineo).

Ufafanuzi mwingine wa vivumishi tofauti na huu unatolewa na Karingi (2012) ambaye anaeleza vivumishi kwa kuzingatia mtazamo wa sintaksia finyizi. Kwa mujibu wa maelezo yake, kivumishi ni neno linalotoa sifa zaidi kuhusu nomino na linachangia maana ya nomino.Yeye ametofautisha vibainishi na vivumishi ambapo kulingana naye kategoria za vivumishi zinajumuisha tu maneno yanayotoa sifa mbalimbali kuhusu nomino - vivumishi vya tabia (mfano: mkali, mcheshi), vya umbo (kwa mfano: mdogo, mnono, mrefu) na vya hali (-eupe, bichi, -zuri). Katika kueleza vibainishi, anashikilia kuwa hili ni neno linalotoa

taarifa zaidi kuhusu nomino bila kuhusika na maana ya nomino inayorejelewa. Anaainisha makundi yafuatayo ya vibainishi: vibainishi viashiria, vibainishi vimilikishi, vya idadi, viulizi na vya pronomino.

Utafiti huu haukuzingatia uainishaji wa vivumishi unaopendekezwa na Karingi bali ulizingatia ule wa Steer. Huu ndio unaozingatiwa na mtaala wa Kiswahili wa shule za msingi na hautofautishi vivumishi na vibainishi. Sababu ya kuzingatia uainishaji huu ni kuwa mtihani wa KCPE unaofanywa na wanafunzi huzingatia yaliyomo katika silabasi.

#### 2.1.2.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa

Kwa mujibu wa Steere (1865), viambishi awali vya vivumishi vya sifa katika Kiswahili vinafanana na vile vya nomino isipokuwa ngeli ya U katika umoja. Aidha, kuna vile ambavyo havichukui viambishi vya nomino mathalani bora, rahisi, safi, hodari, kamili, lazima, ghali, haba, imara, maarufu, halali, hafifu, dhahiri, laini, haramu, dhaifu. Mifano ifuatayo inabainisha vivumishi hivi:

(2.5)

a. *Msichana mrefu, mbwa mkali, kiatu kizuri, mtoto mnene, mti mrefu.*
b. *Ukuta mchafu, ubao mweusi.*
c. *Mtoto safi, nguo rahisi, mwanafunzi hodari, bidhaa ghali, ngozi laini.*

Katika mifano 2.5(a), tunaona vile vivumishi vinavyochukua viambishi awali vya nomino ilhali mifano ya 2.5(b) inaonyesha vivumishi vinapotumika pamoja na

nomino za ngeli ya U (umoja) ambapo havichukui kiambishi cha nomino. Aidha mifano ya 2.5(c) inajumuisha vivumishi ambavyo havichukui vianzio vya nomino asilani.

#### 2.1.2.2 Vivumishi vimilikishi

Vimilikishi ni maneno yanayoonyesha nomino inamiliki kitu fulani. Mizizi ya vivumishi hivi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali (-angu, -ako, -ake/-etu, -enu, -ao). Kwa kuwa vimilikishi si maneno kamili, sharti vitumiwe vikiwa vimeambatishwa na viambishi awali vya nomino za ngeli husika kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 2.3.

**Jedwali 2.3: Vivumishi vimilikishi**

| | **Kimilikishi** | | |
|---|---|---|---|
| **Nomino** | **Nafsi 1 umoja– wingi** | **Nafsi 2 umoja– wingi** | **Nafsi 3 umoja- wingi** |
| mtoto / watoto | wangu – wetu | wako – wenu | wake – wao |
| mkate / mikate | wangu – wetu | wako – wenu | wake – wao |
| jicho / macho | langu – yetu | lako – yenu | lake – yao |
| kiti / viti | changu– vyetu | chako – vyenu | chake – vyao |
| Nyumba | yangu – yetu | yako – yenu | yake – yao |
| Pahali | pangu – petu | pako – penu | pake – pao |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Jedwali la 2.3 linadhihirisha wazi kuwa mizizi ya vivumishi vimilikishi vya nafsi mbalimbali huchukua viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya ngeli za nomino husika ili kuwa maneno kamili. Mifanyiko ya kifonolojia inafanya sauti mbalimbali zinazofuatana katika maumbo ya maneno yanayozalishwa kuathiriana

kwa njia fulani na hivyo kuchukua umbo maalum kama inavyobainika katika mifano ifuatayo.

(2.6)

a. *Mtoto (wa +-angu) wangu (a moja inadondoshwa)*
b. *Watoto (wa +-etu) wetu*
c. *Kiti ( cha + -angu) changu*
d. *Viti (vi +-etu) vyetu*

**2.1.2.3 Vivumishi viulizi**

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza swali kuhusu nomino husika. Baadhi ya vivumishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli kwa mfano, -ngapi, -pi?

(2.7)

a. *Ni watoto wangapi wamefukuzwa? ( - kuulizia idadi)*
b. *Je, ni dawati lipi lenye funguo zangu?*
c. *Ni mtoto yupi aliyetuzwa?*
d. *Mama alinunua milango ipi?*
e. *Umefua nguo zipi?*
f. *Umenunua vitabu vingapi?*
g. *Amekata miti mingapi?*

Kunavyo vivumishi viulizi vingine ambavyo havichukui viambishi vyovyote. Kwa mfano, gan*i*? nini?

(2.8)

a. *Unazungumza kuhusu kipindi gani?*
b. *Amenunua vitabu gani?*
c. *Je, amekuambia nini?*

Kulingana na mifano hii, vivumishi viulizi ‘gani’ na ‘nini’ havionyeshi kiambishi chochote cha jina linalovumishwa. Navyo vivumishi viulizi ‘-pi’ na‘-ngapi’ huchukua umbo wakilishi la nomino inayovivumisha.

### 2.1.2.4 Vivumishi vya '- a' unganifu

Vivumishi hivi hutueleza zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha kitu kinachomiliki nomino hiyo. Hivi huundwa kwa kuambatisha kiambishi ngeli pamoja na kiambishi '–a' cha 'A'-unganifu, kisha nomino kwa mfano: cha, la, kwa, za na ya kama inavyobainika katika mifano 2.9.

(2.9)

a. *Watoto **wa mwalimu** mkuu wana tabia nzuri.*
b. *Chai **ya daktari** imemwagika.*
c. *Kitabu **cha mwalimu** kimepotea.*
d. *Duka **la mama** limefungwa.*
e. *Nyumba **ya nyanya** ni safi.*

### 2.1.2.5 Vivumishi vya pekee

Vivumishi hivi vinaundwa na mizizi ifuatayo: -enye, -ote, - o-ote, -enyewe na -ingine. Miundo ya vivumishi vinavyoundwa na mizizi hii hutegemea viambishi vya ngeli. Jedwali 2.4 linaonyesha mifano ya miundo tofauti ya vivumishi hivi kwa kuzingatia nomino za ngeli mbalimbali.

**Jedwali 2.4: Vivumishi vya pekee**

| **Nomino** | **Vivumishi** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **-enye** | **-enyewe** | **-ote** | **-o-ote** | **-ingine** |
| Mtoto | mwenye | mwenyewe | yeyote | - | mwingine |
| Watoto | wenye | wenyewe | wowote | wote | wengine |
| Mti | wenye | wenyewe | Wote | wowote | mwingine |
| Miti | yenye | yenyewe | Yote | yoyote | mingine |
| Gari | lenye | lenyewe | Lote | lolote | linguine |
| Magari | yenye | yenyewe | Yote | yoyote | mengine |
| Kikombe | chenye | chenyewe | Chote | chochote | kingine |
| Vikombe | vyenye | vyenyewe | Vyote | vyovyote | vingine |
| Pahali | penye | penyewe | Pote | popote | pengine |

Matumizi ya vivumishi hivi vya pekee katika kutoa habari zaidi kuhusu nomino yanatofautiana:

-enye (kumiliki)

-enyewe (kusistiza)

-ote (ujumla)

-o-ote (bila kubagua)

-ingine (ziada au badala ya)

*(2.10)*

a. *Mzee mwenye gari ndiye huyu.*
b. *Kitabu chenyewe ndicho hiki.*
c. *Pahali pote pamejaa.*
d. *Kikombe chochote kinafaa.*
e. *Nyumba nyingine imejengwa. (ziada)*
f. *Chungwa hili halijaiva, nipe lingine. (badala ya)*

### 2.1.2.6 Vivumishi vya idadi (Tarakimu)

Haya ni maneno yanayowakilisha idadi. Maneno haya huwakilisha vivumishi vya idadi yanapotumika kueleza zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna vivumishi vya idadi kamili na vya idadi isiyodhihirika. Vivumishi vya idadi kamili hutumia nambari (tarakimu) kueleza idadi ya nomino kama vile moja, mbili na tatu. Navyo vivumishi vya idadi isiyodhihirika huelezea idadi ya nomino kwa ujumla kama vile chache, nyingi na kidogo. Kuna vivumishi vya idadi vinavyokubali viambishi awali na vile visivyokubali kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.5.

**Jedwali 2.5: Vivumishi vya idadi**

| Nom. | Vivumishi vya idadi | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **moja** | **mbili** | **tatu** | **nne** | **tano** | **Sita** | **saba** | **nane** | **tisa** | **kumi** | **-ingi** | **-chache** |
| Mtu | mmoja | | | | | | | | | | | |
| Watu | | wawili | watatu | wanne | watano | Sita | saba | wanane | tisa | kumi | wengi | wachache |
| Mti | mmoja | | | | | | | | | | | |
| Miti | | miwili | mitatu | minne | mitano | Sita | saba | minane | tisa | kumi | mingi | michache |
| Jiwe | moja | | | | | | | | | | | |
| Mawe | | mawili | matatu | manne | matano | Sita | saba | nane | tisa | kumi | mengi | machache |
| Kiti | kimoja | | | | | | | | | | | |
| Viti | | viwili | vitatu | vinne | vitano | Sita | saba | vinane | tisa | kumi | vingi | vichache |
| Nguo | moja | | | | | | | | | | | |
| Nguo | | mbili | tatu | nne | tano | Sita | saba | nane | tisa | kumi | nyingi | chache |
| Uzi | mmoja | mbili | tatu | nne | tano | Sita | saba | nane | tisa | kumi | nyingi | chache |
| Nyuzi | | mbili | tatu | nne | tano | Sita | saba | nane | tisa | kumi | nyingi | chache |

Kwa mujibu wa Jedwali 2.5, tarakimu 1, 2, 3, 4, 5 na 8 zinachukua viambishi vya ngeli za nomino husika ilhali 6, 7, 9 na 10 hazichukui. Vilevile vivumishi vya idadi isiyodhihirika huchukua viambishi vya ngeli.

Kulingana na Polome (1967) na Myachina (1981), tarakimu 6, 7 na 9 ni za asili ya Kiarabu. Kumi (10) ni ya asili ya Kibantu hata kama haichukui viambishi vya nomino.

### 2.1.3 Urejeshi katika Kiswahili

Virejeshi ni viambishi au vipashio vya maneno vinavyorejelea nomino, viwakilishi au vivumishi kwenye maneno. Dhana ya urejeshi katika Kiswahili ni pana sana na inaweza kuonyeshwa kwa kutumia ama umbo la kileksia au kiambishi kinachoambishwa kwenye kitenzi (Taz. § 2.1.3.1 -2.1.3.4).

#### 2.1.3.1 Urejeshi wa kileksia

a. Yeye = kiwakilishi nafsi ya tatu umoja kinachosimama kwa ngeli ya YU/A – WA.

   Kwa mfano, Yeye ameenda

b. Mwenyewe = Kipashio cha urejeshi kinachomaanisha ‘huyo hasa’. Kwa mfano, Mama mwenyewe amefika.

c. Mwenye = Kipashio cha urejeshi kinachomaanisha ‘aliye na’. Kwa mfano, Tajiri mwenye gari ndi**ye** huyu.

#### 2.1.3.2 Urejeshi unaodhihirishwa na viambishi

a. ji - : Watoto wamejichafua.
b. -O- : Watoto waliojichafua wameadhibiwa.
c. -ye- : Mtoto aliyejipaka rangi amependeza.
d. Ndi- : Mwalimu ndiye aliyenipa kitabu hiki.

Mbaabu (1995) anafafanua kwamba katika Kiswahili, nomino huweza kurejelewa katika kitenzi kwa kutumia virejeshi vya ngeli vya kati na virejeshi vya mwisho kulingana na mahali kiambishi kinachorejelea nomino hizo hujitokeza.

#### 2.1.3.3 Virejeshi awali

Hivi ni viambishi vinavyojitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi vinapotumiwa kurejelea nomino mtenda au mtendwa. Muundo wa viambishi hivi hutegemea ngeli ya nomino hiyo inayorejelewa kama inavyobainika katika mfano 2.11.

*(2.11)*
*a) Mama anapika chakula / vyakula.*
*b) Mama ana**ki**pika chakula / ana**vi**pika / vyakula.*

Kulingana na mifano hii (2.11), sentensi ya (a) ni sawa na ya (b). Katika sentensi ya (b), viambishi {ki/vi} ndivyo virejeshi awali; yaani viambishi vinavyorejelea nomino mtendwa (chakula / vyakula) katika ngeli za KI/VI.

Aidha, Kiswahili kinatumia aina nyingine ya kirejeshi awali {o} kinachorejelea nomino ambayo imetajwa kabla ya kitenzi chenyewe kutajwa. Mgullu (1999) anaeleza kuwa katika kundi hili pia ndimo tunakuta mofu rejeshi ya namna vi + o {vyo} kama tunavyopata katika mfano, 'namna alivyocheza'. Aidha, mofu rejeshi hizi ndizo huandamana na matumizi ya shina 'amba'' katika kuunda kiwakilishi cha nomino iliyotajwa. Kwa mfano: Ua ambalo limekatwa /lililokatwa, nyumba ambazo zimejengwa/zilizojengwa, mti ambao umeanguka /ulioanguka.

### 2.1.3.4 Virejeshi tamati

Hivi hupatikana mwishoni mwa kitenzi (baada ya mzizi) ili kurejelelea nomino iliyokwisha kutajwa.

*(2.12)*
a. *Mti ukatwa**o** ni wa mama.*
b. *Chakula kipikwa**cho** ni cha mgeni*
c. *Nyumba ijengwa**yo** ni yetu*

## 2.2 Kitaita

Kitaita pia hujulikana kama Kidawida na ni lugha ya Kibantu. Lugha hii

huzungumzwa na Wataita (Wadawida) ambao ni jamii mojawapo nchini Kenya, ya watu wanaokaa katika Wilaya ya Taita/Taveta. Kitaita kina lahaja mbalimbali. Kulingana na Mwaliwa (2000), hizi ni pamoja na Kiwerugha, lahaja inayotumiwa na wazungumzaji - wazaliwa wa Mghange, Werugha na Wundanyi. Lahaja ya Kimwanda inayotumiwa na wazungumzaji - wazaliwa wa Mwanda na Kibura (lahaja ya Wabura), Kishamba (ya Wakishamba), Kirong'e (Warong'e) na Kimbololo (Wambololo). Lahaja iliyotumiwa katika utafiti wetu ni Kiwerugha. Vipengele mbalimbali vya kisarufi kuhusu lugha hii ni kama inavyodhihirika katika §2.2.1 - 2.2.3.

### 2.2.1 Ngeli za nomino katika Kitaita

Kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, Kitaita pia kinatumia mfumo wa ngeli. Ngeli hizi ndizo hutawala mahusiano yote kati ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Ngeli hizi zinaweza kuainishwa kimofolojia na kisintaksia kama ifuatavyo.

#### 2.2.1.1 Ngeli za nomino za Kitaita kimofolojia

Mwaliwa (2000) ameshughulikia ngeli za Kitaita kwa kuzingatia kipengele cha kimofolojia cha nomino. Ameainisha jumla ya ngeli kumi na nane kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.6.

**Jedwali 2.6: Ngeli za nomino za Kitaita kimofolojia**

| Ngeli | | Mifano ya nomino | Mfano wa sentensi |
|---|---|---|---|
| 1 | MU (nomino za binadamu) | Mundu (mtu), mwai (msichana), mwana (mtoto), mka (mke) | Mundu mlacha wacha (Mtu mrefu amefika). |
| 2 | WA (βA) (wingi wa ngeli ya kwanza ) | wandu (watu), wai (wasichana) wana (watoto), waka (wake) | Wandu walacha wacha (Watu warefu wamefika). |
| 3 | MU (majina ya miti, viungo vya mwili) | mudi (mti), mkonu (mkono), muembe (muembe) | Mudi mlacha gwademwa (Mti mrefu umekatwa). |
| 4 | MI (wingi wa ngeli ya 3) | midi (miti), mikonu (mikono), miembe (miembe) | Midi milacha yademwa (Miti mirefu imekatwa). |
| 5 | I | igho (jiwe), ikaji (kiazi), isaka (kichaka) iriso (jicho), ighi (yai) | Igho ibaa jabarwa (Jiwe kubwa limevunjwa). |
| 6 | MA (wingi wa ya 5) | magho (mawe), masaka(vichaka), meso (macho), maghi (mayai) | Magho mabaa ghabarwa. (Mawe makubwa yamevunjwa). |
| 7 | KI (Nomino za ngeli hii huchukua kiambishi {Ki} | kidasi (kikapu), kichula (chura), kifumbi (kiti), kitungure (kipofu) | Kidasi kiwishi chalaghaya. (Kikapu kipya kimepotea) |
| 8 | VI (Nomino za wingi wa ngeli ya 7) | vidasi (vikapu), vichula (vyura), vifumbi (viti), vitungure (vipofu), | Vidasi viwishi valaghaya (Vikapu vipya vimepotea). |
| 9 | N (nomino zinazoanza kwa kiambishi {N} | nguwo (nguo), ng'ombe (ng'ombe), ngarai (karai), njala (njaa), mburi (mbuzi), | Ng'ombe mbaa yafwa. (Ng'ombe mkubwa amekufa). |
| 10 | N (Nomino za wingi wa ngeli ya 9) | Nguwo (nguo), ng'ombe (ng'ombe), nguku (kuku), mburi(mbuzi) | Nguwo yarashuka. (Nguo imeraruka) |
| 11 | LU (Nomino za ngeli hii huanza kwa kiambishi {Lu}) | Lufu (upanga), lungo (uteo), luki (ukuni), lunyasi ( unyasi) | Lufu luwishi lwalaghaya (Upanga mpya umepotea). |
| 12 | CHU (tʃu) (ngeli ya nomino za wingi wa ngeli ya 11) | Chufu (panga), chungo (teo), chuki (kuni) | Chufu mbishi ralaghaya (Panga mpya zimepotea). |
| 13 | KA (ngeli ya Nomino za udogo) | Kamwana (kitoto), kamoda (kijito), kamghondi (kilima) | Kamoda aka kawaoma (Kijito hiki kinakauka). |
| 14 | WU (βU) (ngeli Nomino za dhahania) | Wutoi (wizi), wukelu (ujinga) wuda(vita), wukongo (ugonjwa) | Wutoi gwazidi (Wizi umezidi) |
| 15 | KU (ngeli ya nomino za vitenzi – jina) | kubora (kuimba), kusarigha (kucheza), kushoma (kusoma) | Kubora kwapoie (Kuimba ni kuzuri). |
| 16 | AHA (Mahali karibu/dhahiri) | Andu (mahali) | Andu aha kwafwagilwa (Mahali hapa pamefagiliwa). |
| 17 | AHO (Mahali mbali wastani/ndani 'ya') | Andu (mahali) | Aho niko mbewa yangia (Humo ndimo panya alimoingia). |
| 18 | AJA (Mahali mbali /kusiko dhahiri) | Andu ( mahali) | Andu aja kwaelie (Mahali kule ni safi). |

Asili: Mwaliwa (2000)

Kwa mujibu wa muainisho huu wa Jedwali 2.6, majina yenye vianzio sawa yamewekwa katika ngeli moja na kuna jumla ya ngeli 18. Ngeli ya kwanza na ya

pili *(MU/WA)* zinajumuisha majina yanayorejelea binadamu pekee ambayo huanza na mu (umoja) na wa (wingi). Hapa tunaona kuwa majina ya viumbe wenye uhai hayamo katika ngeli moja. Nomino za viumbe wengine wenye uhai zimo katika ngeli za 7 na 8 *(KI/VI)* kwa mfano, *kichula* (chura) na *kishushe* (nge), *kitungure* (kipofu) na kadhalika. Majina mengine yote yanayoanza kwa viambishi ki (umoja) na vi (wingi) pia yamo katika ngeli ya *KI/VI*. Aidha, kuna majina mengine ya viumbe wenye uhai yaliyo katika ngeli za 9 na10 mathalan, *ng'ombe*, *nguku* (kuku), *choka* (nyoka) na kadhalika.

Ngeli za 3 na 4 *(MU /MI)* ni za majina yanayoanza kwa kiambishi mu (umoja) na mi (wingi). Nazo ngeli za 5 na 6 ni za majina yanayoanza kwa kiambishi i (umoja) na ma (wingi).

Ngeli za 11/12 {*LU / CHU (tʃu)*} nazo zinajumuisha majina yanayoanza kwa *lu* (umoja) na *chu* (wingi). Ngeli ya 16, 17 na 18 ni za nomino ya mahali. Hizi zinawakilishwa na *AHA*, *AHO* na *AJA* mtawalia. Ngeli ya 16 *(AHA)* hutumiwa kurejelea mahali karibu na ambapo ni dhahiri, ya 17 *(AHO)* ni ya kuwakilisha mahali kuliko umbali wa wastani na vilevile huleta dhana ya 'ndani ya' mahali fulani nayo ya 18 *(AJA)* ni ya mahali mbali, pasipo dhahiri.

#### 2.2.1.2 Ngeli za nomino za Kitaita kisintaksia

Nomino za Kitaita zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia viambishi vya upatanishi

wa kisarufi vinavyotumika kuoanisha nomino na kategoria nyingine za maneno. Nomino zenye viambishi sawa vya upatanishi wa kisarufi zinawekwa katika ngeli moja. Jedwali lifuatalo (2.7) linaonyesha muainisho wa ngeli nomino za Kitaita Kisintaksia kwa kuzingatia viambishi vya upatanishi wa kisarufi

**Jedwali 2.7: Ngeli za nomino za Kitaita kisintaksia**

| **Ngeli** | | **Vipatanishi** | **Mfano wa sentensi** |
|---|---|---|---|
| 1 | WA/ (βA) WA | wa | Mundu mlacha wacha (Mtu mrefu amefika). |
| | | wa | Wandu walacha wacha (Watu warefu wamefika. |
| 2 | GWA/RA(YA) | gwa | Mudi mlacha gwademwa (Mti mrefu umekatwa). |
| | | ya/ra | Midi milacha yademwa (Miti mirefu imekatwa). |
| 3 | JA/GHA | ja | Igho ibaa jabarwa (Jiwe kubwa limevunjwa). |
| | | gha | Magho mabaa ghabarwa. (Mawe makubwa yamevunjwa). |
| 4 | CHA /VA | cha | Kidasi kiwishi chalaghaya. (Kikapu kipya kimepotea). |
| | | va | Vidasi viwishi valaghaya (Vikapu vipya vimepotea). |
| 5 | YA/RA | ya | Ng’ombe mbaa yafwa. (Ng’ombe mkubwa amekufa). |
| | | ra | Ng’ombe rafwa (Ng’ombe wamekufa). |
| 6 | LWA/RA | lwa | Lufu luwishi lwalaghaya (Upanga mpya umepotea). |
| | | ra | Chufu mbishi ralaghaya (Panga mpya zimepotea. |
| 7 | KA | ka | Kamoda aka kawaoma (Kijito hiki kinakauka). |
| 8 | GHA | gha | Machi ghasia (Maji yameisha). |
| 9 | WU (βU) | gwa | Wutoi gwazidi (Wizi umezidi). |
| 10 | YA/YA | ya | Sukari yasia (Sukari imeisha). |
| 11 | CHA | cha | Chai chasia (Chai imeisha). |
| 12 | KU | ku | Kubora kwapoie (kuimba ni kuzuri). |
| 13 | AHA | aha | Andu aha kwafwagilwa (mahali hapa pamefagiliwa). |
| | AHO | aho | Aho niko mbewa yangia (humo ndimo panya alimoingia). |
| | AJA | aja | Andu aja kwaelie (Mahali kule ni safi). |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Katika Jedwali 2.7 tunaona kuwa kuna jumla ya ngeli 13 za nomino za Kitaita kwa kuzingatia muainisho wa kisintaksia unaotumia viambishi vinavyopatanisha nomino na kategoria mbalimbali za maneno katika sentensi. Kuna ngeli zenye vipatanishi vya umoja na vya wingi ambazo ni pamoja na *WA/ βA (WA), JA/CHA, CHA/VA, GWA/RA (YA), YA/RA* na *LWA/RA.* Ngeli ya *WA/ (βA) WA* inajumuisha nomino zinazotumia vipatanishi *wa* (umoja) na *wa* (wingi). Nomino zote zinazorejelea binadamu zimo katika ngeli hii kama vile *mundu* (mtu), *mwai* (msichana) na *musawi* (mchawi). Ngeli ya *GWA/RA (YA)* ina vipatanishi *gwa* (umoja) na *ra/ya* (wingi). Viambishi vya wingi ni viwili na hutumika kwa ubadalia. Mifano ya nomino za ngeli hii ni *mudi* (mti), *muchungwa* (mchungwa) na *mufereji* (mfereji).

Aidha, kuna ngeli ambazo zina kipatanishi sawa katika umoja na wingi. Ngeli hizi ni za *KA, GHA, WU, YA, CHA, KU* na *AHA/AHO/AJA.* Ngeli ya *KA* inajumuisha nomino za udogo zikiwa katika umoja na hupatanishwa na kipatanishi *[ka]*. Nayo ngeli ya *YA* inajumuisha nomino zinazopatanishwa na *[ya]* katika (umoja) na wingi. Nomino hizi hazibadiliki katika umoja na wingi. Mifano ni *sukari* na *sumu*. Ngeli ya *YA* ni ya nomino kama vile *chai* zinazopatanishwa kwa *[cha]*. Ngeli ya *AHA/AHO/AJA* inajumuisha nomino, mahali. Viambishi hivi hutumika kwa ubadalia kuleta dhana zifuatazo kuhusu mahali: Kiambishi *[aha]* hurejelea mahali

karibu /dhahiri, *[aho]* mahali mbali wa wastani / ndani ya na *[aja]* mahali mbali sana / kusiko dhahiri.

### 2.2.2 Upatanishi wa kisarufi wa nomino na vivumishi

Upatanishi wa kisarufi ni kipengele muhimu sana kinachozingatiwa katika sarufi ya lugha ya Kitaita. Upatanishi wa kisarufi katika Kitaita huegemea zaidi kipengele cha kimofolojia cha majina husika badala ya sifa za kisemantiki za nomino zenyewe. Kategoria nyingine za maneno huchukua viambishi vya ngeli ya nomino husika kama inavyoonyeshwa katika § 2.2.2.1 - §2.2.2.6).

#### 2.2.2.1 Upatanishi wa nomino na vivumishi vya sifa

Vivumishi vya sifa katika Kitaita si maneno kamili. Mizizi ya vivumishi hivi vya sifa ni kama vile–*poie* (-zuri), -*lue* (chafu), -*elie* (-safi), *bandie* (nono/nene), chilu *(-eusi)*, -*chokwa* (-eupe), -*lacha* (-refu), -*ghokie* (-rembo), -*zamie* (-baya), -*birie* (-kali), -*tini* (-dogo), -*vui* (fupi) na -*singie* (tamu). Jedwali 2.8 linatupa mifano ya vivumishi kwa kuzingatia nomino kutoka ngeli mbalimbali.

**Jedwali 2.8: Vivumishi vya sifa**

| Ngeli | Nomino | Vivumishi | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **-poie (-zuri)** | **-bandie (nenepa / nono)** | **-zamie (-baya)** |
| MU | mwai (msichana) | Upoie | ubandie | uzamie |
| WA | wai (wasichana) | Wipoie | wibandie | wizamie |
| MU | mudi (mti) | Ghupoie | ghubandie | ghuzamie |
| MI | midi (miti) | i /(ri) poie | ri/(i) bandie | ri/(i)zamie |
| I | ikaji (kiazi) | ji-poie | jibandie | jizamie |
| MA | makaji (viazi) | Ghipoie | ghibandie | ghizamie |
| KI | kidu (kinu) | Chipoie | - | chizamie |
| VI | vidu (vinu) | Vipoie | - | vizamie |
| N | nguwo (nguo) | Ipoie | - | izamie |
| N | nguwo (nguo) | Ripoie | - | rizamie |
| LU | luki (ukuni) | Lupoie | lubandie | luzamie |
| CHU | chuki (kuni) | Ripoie | ribandie | rizamie |
| AHA/AHO /AJA | andu (mahali) | Kupoie | - | kuzamie |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kwa mujibu wa Jedwali 2.8 ni bayana kuwa mizizi ya vivumishi vya sifa huambishwa viambishi awali vya ngeli za nomino husika kwa kuwa si maneno kamili kama tunavyoona katika 2.14 (a), (b), (c) wingi na (d) wingi. Hata hivyo katika baadhi ya ngeli, vivumishi vya sifa havichukui kipatanishi cha ngeli bali huchukua umbo wakilishi la nomino husika mathalani katika mifano ya 2.14 (c) umoja na (d) umoja.

(2.14)

| | **Umoja** | **wingi** |
|---|---|---|
| a. | *Mudi ghupoie* (Mti mzuri). | *Midi ipoie* /ripoie (Miti mizuri). |
| b. | *Kidu chipoie* (Kinu kizuri). | *Vidu vipoie* (Vinu vizuri). |
| c. | *Mwai upoie* (Msichana mzuri). | *Wai wipoie* (Wasichana wazuri). |
| d. | *Nguwo ipoie* (Nguo nzuri). | *Nguwo ripoie* (Nguo nzuri). |

### 2.2.2.2 Vivumishi vimilikishi

Mizizi ya vivumishi vimilikishi vya Kitaita ni: nafsi 1 *(-apo/-edu)*, nafsi 2 *(-ako/-enyu)* na nafsi 3 *(-ake/-awo)*. Kwa vile si maneno kamili inabidi viambishwe viambishi vingine ili kuvikamilisha. Jedwali 2.9 linaonyesha mifano ya vivumishi vimilikishi.

**Jedwali 2.9 Vivumishi vimilikishi**

| **Ngeli** | **Nomino umoja / wingi** | **Nafsi 1 (-apo / -edu) Umoja / wingi** | **Nafsi 2 (-ako / -enyu) Umoja / wingi** | **Nafsi 3 -ake / -awo Umoja / wingi** |
|---|---|---|---|---|
| MU/βA(WA) | mwana / wana | wapo / wedu | wako / wenyu | wake / wawo |
| MU / MI | mudi / midi | gwapo / redu (yedu) | gwako / renyu | gwake / gwawo |
| I / MA | ikoti / makoti | japo / ghedu | jako / ghenyu | ghake / ghawo |
| KI / VI | chuo / vuo | chapo / chedu | chako / venyu | chake / chawo |
| N | ng’ombe /ng’ombe | yapo / redu | yako / renyu | yake / rawo |
| LU / CHU | luki / chuki | lwapo / redu | lwako / renyu | lwake / rawo |
| KA | kamwana | kapo / edu | kako / kenyu | kake / kawo |
| AHA / AHO/ AJA | andu | kwapo / kodu | kwako / konyu | kwake / kwawo |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na Jedwali 2.9, mizizi ya vivumishi vimilikishi inaambishwa vipatanishi vya kisarufi vya ngeli za nomino husika ili vikamilike kwa mfano,

(2.15)

| | | **umoja** | **wingi** |
|---|---|---|---|
| a) | Nafsi 1 | *Ikoti ( ja +apo) = japo* (Koti langu) | *Makoti (gha + edu) = ghedu* (Makoti yetu) |
| b) | Nafsi 2 | *Chuo (cha+ako) = chako* (Kitabu chako) | *Vuo (va+enyu) = venyu* (Vitabu vyenu) |
| c) | Nafsi 3 | *Andu ( ku+ake) = kwake* (Mahali kwake) | *Andu ku+ awo = kwawo* (Mahali kwao) |

Mifanyiko ya kimofolojia inahusika katika uzalishaji wa maumbo mbalimbali ya vivumishi hivi vimilikishi.

### 2.2.2.3 Vivumishi viulizi

Mizizi ya viulizi inayotumika ni *'–ao'* (-pi) na *'-linga'* (-ngapi). Jedwali 2.10 linaonyesha mifano ya vivumishi viulizi vinavyorejelea nomino kutoka ngeli mbalimbali.

**Jedwali 2.10: Vivumishi viulizi**

| **Ngeli** | **Nomino** | **Viulizi** | |
|---|---|---|---|
| | | **-ao (-pi)** | **-linga ( ngapi)** |
| MU | mka (mwanamke) | uao | - |
| WA | waka (wanawake) | wiao | walinga |
| MU | mchungwa (mchungwa) | ghuao | - |
| MI | Michungwa | iao | ilinga |
| I | idirisha (dirisha) | jiao | - |
| MA | madirisha (madirisha) | ghiao | alinga |
| KI | kidasi (kikapu) | chiao | - |
| VI | vidasi (vikapu) | viao | vilinga |
| N | ng'ombe | iao | - |
| N | ng'ombe | riao | ilinga |
| LU | Lungo | luao | - |
| CHU | Chungo | riao | ilinga |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na mifano iliyoko katika Jedwali 2.10 ni wazi kuwa mizizi ya viulizi inaambishwa viambishi vipatanishi vya ngeli za nomino husika katika baadhi ya nomino kama vile katika mfano 2.16 (a) na (b) -umoja. Kwingineko mizizi huchukua viwakilishi vya nomino mathalani katika mfano 2.16 (a) na (b) wingi.

(2.16)

| | **Umoja** | **wingi** |
|---|---|---|
| a) | *Muchungwa (ghu) + (-ao) =ghuao* | *Michungwa (i) + (-linga) = ilinga* |
| | *Mchungwa upi?* | *Michungwa mingapi?* |
| b) | *Idirisha (ji) + (-ao) = jiao* | *Madirisha (a) + (-linga) = alinga* |
| | *Dirisha lipi?* | *Madirisha yapi?* |

Mifano ya matumizi ya viulizi hivi katika sentensi ni kama ifuatavyo:

(2.17)

| | **Kitaita** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| a) | *Ni mka uao wakuduma?* | *Ni mwanamke yupi / gani aliyekutuma?* |
| b) | *Ni waka walinga wavika?* | *Ni wanawake wangapi wamefika?* |
| c) | *Ni mdi ghuao ghwademwa?* | *Ni mti upi/gani umekatwa?* |
| d) | *Mao waghua kidasi chiao?* | *Mama amenunua kikapu kipi/gani?* |
| e) | *Apa wauza ng'ombe ilinga?* | *Baba ameuza ngo'mbe wangapi?* |

#### 2.2.2.4 Vivumishi vya 'A' unganifu

Vivumishi vya '-A' unganifu hutokana na kuambisha viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya ngeli ya nomino husika kwenye mzizi '-a' kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.11.

**Jedwali 2.11: Vivumishi vya 'A' Unganifu**

| Ngeli | Nomino | kivumishi 'A'unganifu | mfano wa sentensi |
|---|---|---|---|
| MU | mwana (mtoto) | wa | Mwana wa mao walala. (Mtoto wa mama amelala) |
| βA (WA) | wana (watoto) | wa | Wana wa mao walala. (Watoto wa mama wamelala) |
| MU | muchungwa (mchungwa) | ghwa | Muchungwa ghwa wawa ghooma. (Mchungwa wa nyanya umekauka) |
| MI | michungwa | ya | Michungwa ra/ya wawa yeoma. (Michungwa ya nyanya imekauka) |
| I | igare (gari) | ja | Igare ja apa jalua. (Gari la baba limechafuka) |
| MA | magare (magari) | gha | Magare gha apa ghalua. (Magari ya baba yamechafuka) |
| KI | kidasi (kikapu) | cha | Kidasi cha mao chalaghaya. (Kikapu cha mama kimepotea) |
| VI | vidasi (vikapi) | ya | Vidasi va mao valaghaya. (Vikapu vya mama vimepotea) |
| N | ng'ombe | ya | Ng'ombe ya Mwakio yafwa. (Ng'ombe wa Mwakio amekufa.) |
| N | ng'ombe | ra | Ng'ombe ra Mwakio rafwa. (Ng'ombe wa Mwakio wamekufa) |
| LU | luki | lwa | Luki lwa mao lwaiwa. (Ukuni wa mama umeibwa. |
| CHU | chungo | ra | Chuki ra mao raiwa. (Kuni za mama zimeibwa) |

Asili: Utafiti wetu (2018)

### 2.2.2.5 Vivumishi vya pekee

Mizizi ya kusimamia vivumishi vya pekee katika Kitaita ni pamoja na *-eni* (-enyewe), *-ose* (-ote), *-o-ose* (-o-o-te) na *–mu* (-ingine). Kwa vile haya si maneno kamili inabidi viambishi vya ngeli ya nomino husika viambishwe mwanzoni ili kuyakamilisha. Mifano ya matumizi yao katika ngeli mbalimbali ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 2.12.

**Jedwali 2.12 Vivumishi vya pekee**

| Ngeli | Nomino | Vivumishi | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | -eni (-enyewe) | -ose (-ote) | -o-o-se (-o-ote) | -mu (-ingine) |
| MU | mka (mwanamke) | moni | wose | uowose | umu |
| WA | waka (wanawake) | weni | wose | awowose | wamu |
| MU | mchungwa (mchungwa) | ghoni | ghose | ughoghose | ghumu |
| MI | michungwa | cheni | yose | iyoyose/ irorose | imu |
| I | idirisha (dirisha) | jeni | jose | jojose | jimu |
| MA | madirisha (madirisha) | gheni | ghose | aghoghose | ghamu |
| KI | kidasi (kikapu) | cheni | chose | ichochose | chimu |
| VI | vidasi (vikapu) | veni | vose | ivovose | vimu |
| N | ng’ombe | cheni | yose | iyoyose | imu |
| N | ng’ombe | reni | rose | irorose | rimu |
| LU | lungo | loni | Lose | ulolose | lumu |
| CHU | chungo | reni | rose | irorose | rimu |
| AHA/ AHO/ AJA | andu | koni | kose | ukokose | kumu |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na Jedwali 2.12, maumbo mbalimbali ya vivumishi vya pekee yanaundwa kwa kuzingatia nomino husika.Viambishi viwakilishi vya nomino hizi ndivyo vinavyoambishwa mwanzoni mwa mizizi ya vivumishi hivi.

### 2.2.2.6 Vivumishi vya idadi

Maneno ya kuwakilisha idadi mbalimbali katika Kitaita ni kama ifuatavyo:

1. *imweri* (moja)
2. *iwi* (mbili)
3. *idadu* (tatu)
6. *irandadu* (sita)
7. *mfungade* (saba)
8. *wunyanya* (nane)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | *inya* (nne) | 9. | *ikenda* (tisa) |
| 5. | *isanu* (tano) | 10. | *ikumi* (kumi) |

Baadhi ya vivumishi hivi vya idadi huchukua viambishi vya upatanishi awali vya ngeli ilhali vingine havichukui kama inavyobainika katika Jedwali 2.13.

**Jedwali 2.13 Vivumishi vya idadi**

| **Ngeli** | **nomino** | **kivumishi cha idadi** | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** |
| MU | mwana | umweri | | | | | | | | | |
| WA | wana | | wawi | wadadu | bana | wasanu | warandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |
| MU | mudi | ghumweri | | | | | | | | | |
| MI | midi | | iwi | Idadu | inya | Isanu | irandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |
| I | igho | jimweri | | | | | | | | | |
| MA | magho | | awi | adadu | ana | masanu | arandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |
| KI | kidasi | chimweri | | | | | | | | | |
| VI | vidasi | | viwi | vidadu | vina | visanu | virandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |
| N | nguwo | imweri | iwi | idadi | inya | isanu | irandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |
| LU | lufu | lumweri | | | | | | | | | |
| CHU | chufu | | iwi | idadu | inya | isanu | irandadu | mfungade | wunyanya | ikenda | ikumi |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na Jedwali 2.13, vivumishi vya idadi, moja hadi sita, vinachukua viambishi awali vya ngeli. Navyo vivumishi visivyochukua viambishi vya ngeli ni pamoja na saba *(mfungade)*, nane *(wunyanya)*, tisa *(ikenda)* na kumi *(ikumi)*. Ni wazi kuwa kuna tofauti kati ya Kiswahili na Kitaita kuhusu vivumishi vya idadi visivyochukua viambishi vya ngeli kwani vya Kiswahili ni sita, saba, tisa na kumi ilhali vya Kitaita ni saba, nane, tisa na kumi.

### 2.2.3 Urejeshi katika Kitaita

Katika Kitaita, urejeshi huonyeshwa kama ilivyo katika mifano ifuatayo.

(2.17)

| | Kitaita | Kiswahili |
|---|---|---|
| a. | *Mwana uhu nio udumiloghe.* | *Mtoto huyu ndiye aliyetumwa.* |
| b. | *Vadu ivi nivo vighuioghe.* | *Viatu hivi ndivyo vilivyonunuliwa.* |
| c. | *Nyumba ija niyo yaweaghwa.* | *Nyumba ile ndiyo inayojengwa.* |
| d. | *Mao nio wadeka vindo.* | *Mama ndiye aliyepika chakula.* |
| e. | *Mka uja ucheghe asubuhi ni uao?* | *Mwanamke ambaye alikuja asubuhi ni yupi / Mwanamke aliyekuja asubuhi ni yupi?* |
| f. | *Luki uluja luomie ni ulu.* | *Ukuni ambao umekauka ni huu / Ukuni uliokauka ni huu.* |
| g. | *Mudi ughuja ghudemwagha ni ughu.* | *Mti tulikaokatwa ni huu / Mti ambao ulikatwa ni huu.* |
| h. | *Kidasi ichija chighuloghe ni ichi.* | *Kikapu kilichonunuliwa ni hiki / ambacho kilinunuliwa ni hiki.* |

Kutokana na mifano hii tunaona kuwa katika Kitaita kiambishi *'ni-'* cha urejeshi ni sawa na 'ndi-' ya urejeshi katika Kiswahili (mifano a-d). Mifano (e-h) inaonyesha urejeshi ambao ni sawa na wa 'amba-' rejeshi na 'o' rejeshi katika Kiswahili. Hata hivyo si tafsiri ya moja kwa moja kwani katika Kitaita kuna matumizi ya viashiria vya mbali vinavyotangulia kitenzi kinachohusishwa na nomino inayorejelewa. Viashiria hivi katika mifano yetu ni uja (yule), uluja (ule), ughuja (ule) na ichija (kile).

### 2.3 Ulinganishaji wa vipengele vya kisarufi vya Kiswahili naKitaita

Ubainishaji katika § 2.1- 2.2.3 kuhusu vipengele mbalimbali vya kisarufi katika lugha za Kiswahili na Kitaita, ulituwezesha kuona zinavyotofautiana na kushahabiana. Lugha hizi zote zikiwa ni za Kibantu, zina sifa fulani ambazo

zinafanana katika baadhi ya vipengele vyao vya kisarufi. Hata hivyo kwa kiwango fulani, kuna pia tofauti kati yazo zinazodhihirika katika vipengele hivyo kama ifuatavyo.

### 2.3.1 Mfanano katika Kiswahili na Kitaita

Ngeli za lugha zote kwa kuzingatia muainisho wa kimofolojia zinafanana kwa kiwango fulani kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.14.

**Jedwali 2.14: Ngeli za Kimofolojia katika Kiswahili na Kitaita**

| Tar. | Kiswahili | | Kitaita | |
|---|---|---|---|---|
| | **Ngeli** | **Mifano** | **Ngeli** | **Mifano** |
| 1 | M | mtu, msichana | MU | mundu (mtu), mwana (mtoto), mka (mke) |
| 2 | WA | watoto, wasichana | WA (βA) | wandu (watu), wana (watoto), waka (wake) |
| 3 | M | mti mwembe muungu | MU | mudi (mti), mkonu (mkono), muembe (muembe), mwaka |
| 4 | MI | miti, mikono, miembe | MI | midi (miti) miembe (miembe), miaka (miaka) |
| 5 | JI | jicho, jino, jiko | I | igho (jiwe), ikaji (kiazi), isaka (kichaka) |
| 6 | MA | macho, mawe meko | MA | magho (mawe), masaka (vichaka), maghi (mayai) |
| 7 | KI | kiti, kikapu, kitabu | KI | kidasi (kikapu), kichula (chura) |
| 8 | VI | viti , vikapu, vitabu | VI | vidasi (vikapu), vichula (vyura), |
| 9 | N | nguo,nyumba nyasi | N | nguwo (nguo), ng'ombe (ng'ombe), ngarai (karai), |
| 10 | N | nguo, nyumba nyasi | N | nguwo (nguo), ng'ombe (ng'ombe) |
| 11 | U | utambi, ubeleko, ubao | LU | lufu (upanga), lungo (uteo), lunyasi (unyasi) |
| 12 | N | tambi, mbeleko, mbao | CHU (tʃu) | chufu (panga), chungo (teo), chuki (kuni), |
| 13 | - | - | KA | kamwana (kitoto), kamoda (kijito) |
| 14 | U | ulevi , wizi, ujinga | WU (βU) | wutoi (wizi), wukelu (ujinga) wuda (vita), wukongo (ugonjwa) |
| 15 | KU | kucheza, kusoma | KU | kubora (kuimba), kusarigha (kucheza) |
| 16 | PA | Pahali hapo | AHA | Andu aha (mahali hapa) |
| 17 | KU | Mahali huku | AHO | Andu aho (mahali humo) |
| 18 | MU | Mahali humu | AJA | Andu aja (mahali kule) |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na Jedwali 2.14, katika lugha zote mbili maumbo mengi ya ngeli za nomino zao yanafanana. Uchunguzi wa vipatanishi vyao vya kisarufi unadhihirisha mshahabiano wa kiwango fulani katika baadhi ya ngeli kama inavyodhihirika katika Jedwali lifuatalo 2.15.

**Jedwali 2.15: Vipatanishi vya ngeli za nomino za Kiswahili na Kitaita**

| **Kiswahili** | | **Kitaita** | |
|---|---|---|---|
| **Ngeli** | **Vipatanishi** | **Ngeli** | **Vipatanishi** |
| YU/A-WA | a- wa | WA /WA(βA) | wa-wa |
| U-I | u-i | MU/MI | gwa- ra/ya |
| LI-YA | li-ya | I/ MA | ja/gha |
| KI-VI | ki-v- | CHA / VA | ya/ra |
| I-ZI | i-zi | N/N | ya/ra |
| I | i-i | - | - |
| U-ZI | u-zi | LWA / RA | lwa |
| YA/YA | ya-ya | GHA | gha |
| U | u | GWA | gwa |
| U-YA | u-ya | GWA / GHA | gwa/gwa |
| - | - | KA | ka |
| KU | ku | KU | ku |
| PA | pa | HA | aha |
| KU | ku | HO | aho |
| MU | mu | JA | aja |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na Jedwali 2.15, vipatanishi vya kisarufi vya baadhi ya ngeli katika lugha hizi vinafanana. Kwa mfano, Kiswahili hutumia viambishi {a/wa} katika ngeli ya 1 huku Kitaita pia kikitumia *{a/wa (βa)}* katika ngeli yake ya 1.

Aidha, ngeli ya KU katika lugha hizi mbili hutumia kiambishi {ku). Uchunguzi pia unadhihirisha kuwa lugha zote mbili zina viambishi vitatu vya ngeli ya mahali. Katika Kiswahili viambishi hivi vikiwa ni {pa, ku, mu} na Kitaita *{ha, ho, ja}* kama tunavyoona katika Jedwali 2.15.

### 2.3.2 Tofauti katika Kiswahili na Kitaita

Kulingana na Jedwali 2.14 katika ngeli ya 1 na ya 3 Kiswahili kina alomofu {mu, mw na m} ilhali Kitaita kina alomofu *{mu}* na *{mw}*. Vilevile umbo ngeli ya 13, *(KA)* inayojumuisha nomino za udogo katika Kitaita haliko katika Kiswahili. Nomino za udogo katika Kiswahili ziko katika ngeli ya KI/VI.

Aidha, kuna maumbo yasiyofanana kama vile ngeli za 5, 11, 12, 14, 16-17 ambapo Kiswahili hutumia maumbo {ji, u, n, u, pa, ku, mu} bali Kitaita hutumia *{i, lu, chu, wu, aha, aho, na aja}*. Vilevile ngeli ya pili ya Kitaita ambayo ni sawa na ya pili katika Kiswahili ina viambishi viwili vya wingi *(ra/ya)* huku Kiswahili kikiwa na kimoja tu (i).

Kwa mujibu wa Jedwali 2.14, katika Kitaita majina yanayojumuishwa katika ngeli za *MU/WA*, (1 na 2) ni yale yenye viambishi ngeli *m*u (umoja) na *wa* (wingi). Mifano ni kama vile *mundu* (mtu), *mwana* (mtoto), *mwai* (msichana) na kadhalika. Kwa upande wa Kiswahili, nomino za ngeli ya M/WA hazina viambishi ngeli vinavyofanana bali zina upatanishi sawa wa kisarufi. Majina yote ya viumbe vyenye uhai yamo katika ngeli hii kwa mfano mtu, nzi, kiroboto na ng’ombe.

Ngeli ya mahali katika lugha zote ina viambishi vitatu ambavyo ni {pa, ku, mu} katika Kiswahili na *{aha, aho aja}* katika Kitaita. Hata, hivyo zinatofautiana

kwani katika Kitaita kiambishi cha upatanisho wa kisarufi cha ngeli hii ni kimoja kikiwa ni *{ku}* ilhali katika Kiswahili ni {pa, ku na mu} kama tunavyoona katika Jedwali 2.15.

Aidha, uchunguzi umebainisha kuwa katika Kitaita vivumishi vya idadi, moja hadi sita, vinachukua viambishi awali vya ngeli. Navyo vivumishi visivyochukua viambishi vya ngeli ni pamoja na saba *(mfungade)*, nane *(wunyanya)*, tisa *(ikenda)* na kumi *(ikumi)*. Katika Kiswahili tarakimu zisizochukua viambishi vya nomino ni sita, saba, tisa na kumi.

Urejeshi katika lugha hizi mbili pia hutofautiana kwa kiasi fulani. Katika Kiswahili urejeshi huweza kufanywa mwanzoni au mwishoni mwa kitenzi ilhali katika Kitaita hufanyika tu mwishoni mwa kitenzi. Urejeshi wa Kitaita pia hutumia kiashiria cha mbali kinachotangulia kitenzi kinachooanishwa na nomino inayorejelewa. Aidha, kiwakilishi 'amba' hutumiwa pia katika Kiswahili kurejelea nomino kiima.

*(2.18)*

| | **Kitaita** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| *a.* | *Mwana uja udumiloghe ni uhu.* | *Mtoto aliyetumwa ni huyu/*<br>*Mtoto atumwaye ni huyu.* |
| *b.* | *Vadu ivija vighuiloghe ni ivi.* | *Viatu vilivyonunuliwa ni hivi.* |
| *c.* | *Mka uja ucheghe asubuhi ni uao?* | *Mwanamke aliyekuja asubuhi ni yupi?* |
| *d.* | *Mudi ughuja gudemeloghe ni ugu.* | *Mti ambao umekatwa ni huu.* |

## 2.4 Ubashiri wa nadharia ya UL

Kutokana na tofauti na mfanano ulioko katika vipengele mbalimbali vya kisarufi vya lugha ya Kiswahili na Kitaita, ilitarajiwa wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu waweze kukumbwa na matatizo mbalimbali. Matatizo haya hayatokani tu na zile tofauti zilizoko kati ya vipengele vya lugha hizi bali hata mfanano ambao unaweza kusababisha uhamishaji usiofaa.

Kwanza ilibashiriwa kuwa wanafunzi huenda wangetatizika kupatanisha baadhi ya nomino za ngeli ya A-WA na kategoria nyingine za maneno. Hii hasa ilitarajiwa kutokea kwa zile nomino zisizo na viambishi awali M-WA bali ziko na N, KI/VI na JI/MA kwa mfano, bondia - mabondia, kiwete, viwete na ng'ombe. Katika Kiswahili viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya nomino za viumbe vyenye uhai ni 'a' (umoja) na 'wa' (wingi). Hiki ni kinyume cha ilivyo katika Kitaita ambapo nomino za viumbe wenye uhai huchukua kiambishi cha ngeli zilizomo.

Aidha, mwanafunzi alitarajiwa kupata shida katika upatanishi wa kisarufi unaohusu nomino za udogo. Ilibashiriwa kuwa huenda angefanya kosa. Hii ni kutokana na hali kuwa katika Kitaita nomino za udogo zimo katika ngeli ya *KA* ilhali katika Kiswahili zimo katika ngeli za KI/VI (Taz. § 2.1.1; § 2.2.1). Kuhusu ukubwa wa nomino, mwanafunzi huenda pia angetatizika kwani nomino hazina ukubwa katika Kitaita.

Isitoshe, mwanafunzi huenda angetatizwa na upatanishi wa nomino na vivumishi vya idadi / tarakimu hasa 6 na 8. Katika Kitaita, tarakimu 7, 8, 9 na 10 hazichukui viambishi vya ngeli ilhali katika Kiswahili ni 6, 7, 9 na 10 zisizochukua viambishi vya ngeli. Hali hii huenda ingesababisha tatizo kwa mwanafunzi. (Taz. § 2.1.2.5; § 2.2.2.5).

Tatizo jingine lililobashirika ni kuhusu upatanishaji wa nomino na viulizi. Vivumishi viulizi vyote vya Kitaita si maneno kamili ilhali katika Kiswahili kuna kile ambacho ni neno kamili kisichohitaji kiambishi cha ngeli (-gani). Mwanafunzi alitarajiwa kutatizika anapotumia kiulizi 'gani' kwani amezoea kuambisha viambishi vya ngeli kwenye viulizi vyote katika Kitaita.

Mbali na matatizo ya upatanishi kuhusiana na vivumishi viulizi, ilitarajiwa pia kuwa wanafunzi wangetatizika kupatanisha baadhi ya vivumishi vya sifa na nomino mbalimbali. Hivi hasa ni vile vivumishi vya sifa visivyochukua kiambishi cha ngeli ilhali katika Kitaita havimo (Taz. §2.1.2.1; §2.2.2.2).

Hali kadhalika, tatizo lilitarajiwa kubainika kwenye urejeshi. Matumizi ya kiashiria cha mbali kuonyesha urejeshi wa 'amba' na 'O' rejeshi katika Kitaita huenda ungemchanganya mwanafunzi ambaye angeweza kuhamisha sifa hii na kuitumia katika Kiswahili.

Ilibashirika pia kuwa huenda mwanafunzi angetatizwa na matumizi ya kivumishi cha pekee '-enye' kwani dhana ya kivumishi 'enye' katika Kitaita, ikitafsiriwa itakuwa 'aliye na' kwa mfano,

*(2.19)*

| ***Kitaita*** | ***Kiswahili*** |
|---|---|
| *Muka uko na mwana wacha.* | *Mama (aliye na) mtoto amekuja – tafsiri sisi* |

**2.5 Hitimisho**

Katika sura hii tulichunguza vipengele mbalimbali vya kisarufi katika lugha za Kitaita na Kiswahili – ngeli za nomino, vivumishi, tarakimu na urejeshi. Kwa kushughulikia vipengele mbalimbali vya kisarufi katika lugha hizi mbili tuliona kwamba kwa kiasi kikubwa lugha hizi mbili zina sifa zinazofanana licha ya kuwa kuna pia zile zinazotofautiana.Ufahamu huu uliwezesha ubashiri kufanywa kuhusu baadhi ya matatizo yaliyotarajiwa kuwakumba wanafunzi Wataita wanapojifunza Kiswahili Sanifu. Kwa hivyo, sura inayofuata itaangazia makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafuzi hawa wanapojifunza Kiswahili Sanifu kwa kuchunguza data mbalimbali zilizokusanywa nyanjani.

# SURA YA TATU

## UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KISARUFI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ilihusisha uchunguzi wa majibu ambayo wanafunzi walikuwa wameyatoa katika hojaji, insha na hadithi na kuyatolea maelezo yakiongozwa na nadharia za uchunguzi: Uchanganuzi Linganuzi (UL) na Uchanganuzi Makosa (UM). Kulingana na nadharia ya UM, baada ya kukusanya data makosa ya mwanafunzi hustahili kudhihirishwa kwanza; kisha kufafanuliwa na kuainishwa katika hatua ya tatu. Kinachofuata katika hatua ya nne, ni kuyaeleza makosa hayo ili kuonyesha chanzo chao kwa mujibu wa Ellis (1994). Hivyo basi, tulibainisha makosa ya wanafunzi kama yalivyodhihirika katika data mbalimbali - majibu ya maswali ya hojaji, insha na masimulizi ya hadithi, kisha tukayafafanua na kuyaainisha tukiongozwa na nadharia ya UL.

Odeo na Geofrey (2008) wanasema kuwa makosa ya lugha hutokea pale ambapo mtumiaji wa lugha hutamka au kuandika maneno bila kuzingatia sarufi ya lugha. Makosa ya kisarufi hutokea pale ambapo kauli hazijaandikwa kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi. Upatanishi wa kisarufi ni uwiano uliopo kati ya nomino na maneno mengine yaliyo katika sentensi. Makosa yaliyoyabainishwa yalifafanuliwa kwa kulinganisha kauli za wanafunzi na miundo sahihi inayopaswa kuzingatiwa katika Kiswahili Sanifu kwa mujibu wa Ellis (1994). Majedwali yalitumika kuwasilisha idadi ya wanafunzi waliofanya aina mbalimbali za makosa

na asilimia ya makosa katika kila kategoria iliyohusishwa. Matokeo yalipangwa kwa kuzingatia kategoria mbalimbali za makosa yaliyobainishwa katika mazoezi mbalimbali ya uchunguzi yaliyotumika.

### 3.1 Mifano ya makosa mbalimbali ya kisarufi

Kwa vile ambavyo Kiswahili ni lugha ambishi bainishi, kuna mwingiliano wa kiasi kikubwa cha mofolojia na sintaksia yake. Kuingiliana huku kunadhihirika bayana kwenye upatanishi wa kisarufi kati ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Kimsingi, nomino ndio huamua viambishi vya upatanishi katika sentensi. Uteuzi wa vipatanishi vya ngeli vinavyotumika kuoanisha nomino na maneno mengine katika sentensi hutegemea uainishaji wa nomino husika. Uchunguzi wetu ulijikita katika makosa yaliyohusiana na nomino, vivumishi na virejeshi kulingana na upeo na mipaka ya utafiti wetu kama inavyobainika katika § 3.1.1 – 3.1.2.

#### 3.1.1 Makosa yanayohusiana na upatanishi wa nomino na kivumishi

Katika sentensi, vivumishi hutumika pamoja na nomino kuunda kikundi nomino. Mofolojia ya vivumishi hivi huathiriwa na ile aina ya nomino inayohusika kwani huchukua viambishi vya nomino hiyo. Hata hivyo, kuna baadhi ya vivumishi hasa vile vilivyokopwa visivyochukua viambishi vyovyote. Kwa kuzingatia majibu ya wanafunzi katika maswali ya hojaji, insha na masimulizi tuliweza kuchunguza

vile walivyopatanisha nomino na vivumishi vya aina mbalimbali. Tulibainisha miundo iliyo sahihi na potofu, iliyoashiria vile vivumishi vilivyowatatiza zaidi wanafunzi kama inavyoonyeshwa katika sehemu §3.1.1.1 - § 3.1.1.7.

#### 3.1.1.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa

Katika uchunguzi uliotumia hojaji, kauli zifuatazo nne zilitumika kufanyia uchunguzi kuona vile wanafunzi walipatanisha vivumishi vya sifa safi, -eusi, -zuri na –refu. Matokeo ya majibu yao yamewasilishwa katika Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa**

| Ngeli | Kauli | Majibu ya wanafunzi | Idadi ya wanafunzi | % ya wanafunzi | Jumla ya makosa | % ya makosa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Mtoto –safi ametuzwa | *Mtoto msafi angetuzwa.<br>Mtoto safi ametuzwa. | 29<br>1 | 96.6<br>3.33 | 29 | 96.6 |
| “ | b) Ng’ombe ya chilu yawekamwa (Ng’ombe mweusi anakamuliwa) | Ng’ombe mweusi anakamuliwa<br>*Ng’ombe nyeusi inakamuliwa | 10<br>20 | 33.33<br>66.66 | 20 | 66.6 |
| LI/YA | c) Gari –ke ni -zuri | Gari lake ni zuri<br>*gari yake ni nzuri<br>*Gari lake ni lizuri | 7<br>15<br>8 | 23.33<br>50<br>23 | 23 | 76.6 |
| I/ZI | d) Kamba ndacha yadumbuka. (Kamba ndefu imekatika.) | Kamba ndefu imekatika<br>*Kamba mrefu imekatika | 14<br>16 | 14.66<br>53.3 | 16 | 53.3 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Sentensi za Jedwali 3.1(a) na (c) ni za kujaza mapengo na (b) na (d) ni za kutafsiri. Matokeo ya utafiti wa Jedwali 3.1 yanabainisha kuwa upatanishaji wa nomino za ngeli ya LI/YA uliwatatiza wanafunzi wengi kwani waliotoa jibu lisilo sahihi walikuwa asilimia 76.66. Baadhi yao waliandika majibu kama vile ‘gari nzuri’ na ‘gari lizuri’.

Aidha, uchunguzi ulionyesha kuwa wanafunzi walitatizwa na upatanishaji wa baadhi ya vivumishi na nomino za ngeli ya A/WA.  Kwa mfano, Jedwali 3.1 (a) katika kupatanisha kivumishi 'safi' na nomino 'mtoto', asilimia kubwa ya wanafunzi (96.6) waliandika 'mtoto msafi' huku asilimia 3.33 ikiandika, 'mtoto safi'. 'Safi' ni miongoni mwa vivumishi ambavyo vilikopwa kutoka kwa Kiarabu, ambavyo kimsingi havikuchukua viambishi vya ngeli ila vimeanza kuchukua viambishi hivyo baada ya muda mrefu wa matumizi. Kuna uwezekano kuwa wanafunzi wamejifunza kufanya kosa la kuambisha 'm-' kwa 'safi' kutoka kwa watumizi wengine wa Kiswahili katika mazungumzo yao ya kila siku.  Hivyo basi hili ni kosa la uhamishaji wa mafunzo. Katika Kiswahili 'm' ni mofimu ya umoja na 'wa' (wingi) na huambishwa kwa vivumishi vinapotumika na nomino. Ni wazi kuwa ujumlishaji mno wa sheria za kisarufi kuhusu umoja na wingi wa nomino, ndicho chanzo hasa cha watu wengi kusema, 'msafi'.

Ni bayana kuwa wanafunzi kadha walitatizwa na upatanishaji wa nomino 'ng'ombe' na kivumishi '-eusi'. Walioandika jawabu potofu waliandika 'ng'ombe nyeusi' ambapo kwa jumla walikuwa asilimia 66.6. Hili huenda lilitokana na tofauti iliyoko kati ya Kitaita na Kiswahili ya uainishaji wa ngeli ya nomino 'ngombe'. Katika Kiswahili, nomino hii imo katika ngeli ya 1/2 ilhali katika Kitaita imo katika ngeli ya 9/10.  Katika lugha ya Kiswahili, viumbe wote wenye uhai wamo katika ngeli ya 1/2. Wanafunzi walioandika majibu potofu huenda waliathiriwa na $L_1$ ambapo walifanya kosa la uhamishaji wa kanuni za ngeli

kutoka $L_1$ hadi $L_2$. Upatanishaji wa ngeli ya I/ZI pia uliwatatiza wanafunzi asilimia 53.3 kama tunavyoona katika Jedwali 3.1(d). Wengi waliandika muundo potofu '- kamba mrefu imekatika.'

Insha za wanafunzi zilizokaguliwa pia zilibainisha makosa yaliyohusisha upatanishaji wa nomino na vivumishi vya sifa kama ilivyo katika mifano ifuatayo.

(3.1) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…amechinja ng'ombe kubwa* | *… amechinja ng'ombe mkubwa* |
| *b.* | **…alikuwa na kagari dogo* | *… alikuwa na kigari kidogo* |
| *c.* | **…viti visafi …* | *…viti safi …* |

Vilevile kulikuwa na mifano ifuatayo ya makosa ya kategoria hii katika masimulizi ya wanafunzi;

(3.2) Masimulizi

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Jitu alikuwa ni mkubwa tu* | *Jitu lilikuwa kubwa.* |
| *b.* | **Akachukua kaa leusi* | *Akachukua kaa jeusi* |
| *c.* | **Alikuja na gari leusi lenye alinunua* | *Alikuja na gari jeusi alilonunua.* |
| *d.* | **Jitu lilikuwa na jicho **li**kubwa ajabu* | *Jitu lilikuwa na jicho kubwa ajabu* |

Kwa kuzingatia mifano hii, tatizo la ngeli ya LI/YA limedhihirika katika mifano 3.2 (a) jitu **m**kubwa (d) jicho **li**kubwa. Kwa kawaida, nomino za ngeli hii zikiwa katika umoja haziathiri muundo wa vivumishi vya sifa, jambo ambalo wanafunzi wengi hawakulizingatia. Tatizo hili huenda lilitokana na ujumlishaji mno wa kanuni za sarufi za lugha ya Kiswahili kwani wanafunzi waliambisha viambishi

vya ngeli za nomino pasipostahili.

Mfano 3.1 (a) ulihusu kosa la upatanishaji wa nomino ya ngeli ya A/WA na kivumishi cha sifa. Katika mfano 3.1(b) kuna tatizo la upatanishaji wa nomino ya udogo ‘kigari’ iliyo katika ngeli ya KI/VI, na kivumishi.

### 3.1.1.2 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha kumiliki

Katika hojaji, wanafunzi walipewa sentensi tano wazikamilishe kwa viambishi vifaavyo na Jedwali 3.2 linaonyesha hali halisi ya matokeo ya majibu yao

**Jedwali 3.2: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha kumiliki**

| Ngeli | Kauli | Majibu ya wanafunzi | Kivumishi | idadi ya wanafunzi | % ya wanafunzi | % ya jumla makosa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Mtoto -ake -amelala | Mtoto wake amelala | Wake | 30 | 100 | 0 |
| | b) Ng’ombe -angu -mepotea | Ng’ombe wangu amepotea.<br>*Ng’ombe yangu imepotea . | wangu<br>yangu | 19<br>11 | 63.3<br>36.67 | 36.67 |
| KI/VI | c) kiatu -ake -mepotea | Kiatu chake kimepotea. | chake | 30 | 100 | 0 |
| U/I | d) Miti -ke -mekatwa | Miti yake imekatwa.<br>*Miti zake zimekatwa. | yake<br>zake | 21<br>9 | 70<br>30 | 30 |
| LI/YA | e) Gari -ke ni –zuri | Gari lake ni zuri.<br>*Gari yake ni nzuri. | lake<br>yake | 24<br>6 | 80<br>20 | 20 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Matokeo ya Jedwali 3.2 yanadhihirisha upotofu wa kauli za wanafunzi walipohitajika kupatanisha nomino na vivumishi vimilikishi. Wanafunzi wote hawakutatizwa na upatanishaji wa nomino ya ngeli ya KI/VI na kivumishi kimilikishi kama inavyodhihirika katika Jedwali 3.2 (c). Huenda ngeli hii ni rahisi kwa wanafunzi kwani inafanana katika lugha zote mbili (Taz. Jedwali § 2.2 na Jedwali § 2.7). Aidha, mizizi ya vimilikishi vya nafsi 2 na 3 katika Kiswahili na Kitaita inafanana (Taz. Jedwali §2.3 na §2.9).

Hata hivyo wanafunzi wengi walitatizwa na ngeli za A/WA tunavyoona katika Jedwali 3.2 (b) ambapo asilimia 36.67 walikosea kwa kuandika 'ng'ombe yangu'. Asilimia 30 walishindwa kupatanisha nomino ya ngeli ya U/I na asilimia 20 wakakosea upatanishaji wa ngeli ya LI/YA. Waliokosea waliandika 3.2 (d) 'miti zake' na 3.2 (e) 'gari yake'.

Masimulizi ya wanafunzi hayakudhihirisha makosa ya kategoria hii lakini insha za wanafunzi zilidhihirisha makosa machache yaliyohusisha upatanishaji wa nomino na vimilikishi kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

(3.3) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…gari yangu…* | *…gari langu.* |
| *b.* | **…nichukue mitihani zangu ambazo tulizozifanya.* | *…nichukue matokeo yangu ya mtihanituliokuwa tumeufanya/ambao tulikuwa tumeufanya.* |
| *c.* | **…ngombe zake…* | *…ng'ombe wake...* |

Tatizo la ngeli ya A/WA lilionekana katika mfano 3.3 (c) 'ng'ombe zake. Mifano 3.3 (a) na (b) inaonyesha kuwa wanafunzi walitatizwa na ngeli LI/YA na U/I

mtawalia. Kutatizika kwa wanafunzi na ngeli ya U/I huenda kulitokana na athari za Kitaita. Katika Kitaita kuna viambishi viwili mbadala vinavyotumika katika wingi kwa hivyo huenda wanafunzi walihamisha kanuni hii kwa Kiswahili. Labda walichukulia kuwa pia katika Kiswahili kunaweza kutumika viambishi {u} umoja na {i}/{zi} wingi (Taz. § 2.2.1.2). Athari ya Kitaita pia huenda ndiyo imechangia wanafunzi kufanya kosa katika matumizi ya nomino ’ng’ombe’ ya ngeli ya A/WA. Tatizo hapa ni kuwa wanafunzi walihamisha ufahamu wao wa uainishaji ngeli za nomino kutoka $L_1$ hadi $L_2$. Badala ya kuweka nomino ‘ng’ombe’ kwenye ngeli ya A /WA, wakaiweka katika ngeli ya I/ZI. Kwa mujibu wa nadharia ya UL, huu ni uhamishaji wa kisarufi wa ngeli ya Kitaita hadi lugha ya Kiswahili Sanifu.

#### 3.1.1.3 Upatanishi wa nomino na kivumishi kiashiria

Kauli nne zilitumika kwenye hojaji kuchunguza uwezo wa wanafunzi katika kupatanisha vivumishi viashiria na nomino za ngeli mbalimbali. Matokeo halisi ya majibu yao yameonyeshwa katika Jedwali 3.3.

**Jedwali 3.3: Nomino na Kivumishi kiashiria**

| Ngeli | Kauli | Majibu ya wanafunzi | Kiv. | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Nguku ija ya chilu yafwa. (Kuku yule mweusi amekufa). | Kuku yule mweusi amekufa.<br>*Kuku ile nyeusi imekufa. | yule<br>ile | 19<br>11 | 53.33<br>36.67 |
| KI/VI | b) Viti -vyo vimevunjika. | Viti hivyo vimevunjika.<br>*Viti hivo vimevunjika. | hivyo<br>hivo | 28<br>2 | 93.3<br>6.67 |
| U/I | c) Midi iri rawademwa. | Miti hii inakatwa.<br>*Miti hizi zinakatwa. | hii<br>hizi | 17<br>13 | 56.66<br>43.33 |
| PA/KU /MU | d) Andu aho wangia kwaelie. | Mahali hapo alipoingia ni safi.<br>*Mahali huko alipoingia ni kusafi. | hapo<br>huko | 20<br>10 | 66.66<br>33.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kauli za Jedwali 3.3 (a) na (c) ni za kutafsiri kutoka Kitaita hadi Kiswahili na zile nyingine ni za kukamilisha kauli kwa viambishi mwafaka. Matokeo ya Jedwali 3.3 yanaonyesha kuwa katika kupatanisha nomino ‘kuku’ na kiashiria, asilimia 36.67 ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi. Muundo usio sahihi waliouandika ni ‘kuku ile’. Wanafunzi asilimia 6.67 walikosea upatanishaji wa nomino ‘viti’ na kiashiria na asilimia 43.33 wakashindwa kuoanisha nomino ‘miti’ na kiashiria mwafaka. Majibu potofu yaliyodhihirika ni kwa mfano, Jedwali 3.3 (b) ‘viti hivo’ na (c) ‘miti hizi’, 3.5 (b) ‘hii shamba’, (c) ‘hiyo jitu’.

Aidha, asilimia 33.33 ya wanafunzi waliandika miundo potofu ya upatanishaji wa nomino ya mahali na kiashiria. Waliokosea kama tunavyoona katika Jedwali 3.3 (d) waliandika, ‘mahali huko alipoingia’.

Makosa ya kategoria hii hayakuwa mengi katika insha na masimulizi ya wanafunzi. Mifano ni kama ifuatavyo:

(3.4) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Siku hii sitawahi kuisahau…* | *Sitawahi kuisahau siku hiyo…* |
| *b.* | **Ziara hio …* | *Ziara hiyo…* |

(3.5) Masimulizi

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **alipoingia huko ndani…* | *alipoingia humo ndani…* |
| *b.* | **…hii shamba si yetu* | *…shamba hili si letu* |
| *c.* | **…nyumba ya hiyo jitu* | *…nyumba ya hilo jitu* |
| *d.* | **ule wazimu aliyekuwa mbuzi…* | *yule wazimu aliyekuwa mbuzi…* |

Kutokana na matokeo haya inaonyesha wazi kuwa baadhi ya makosa ya wanafunzi yalitokana na kutotumia viambishi mwafaka vya ngeli za nomino mbalimbali katika uundaji wa viashiria. Aidha, wanafunzi hawakuzingatia matumizi sahihi ya viambishi vya mahali walipoashiria pahali penye sifa fulani kwa mfano, 3.5 (a) 'alipoingia huko ndani'. Hili linaonyesha kuwa wanafunzi wanapuuza dhana mbalimbali za viambishi vya mahali (pa-ku-mu) na kanuni ya kisarufi ya ngeli hii inayohitaji viambishi hivi visichanganywe katika sentensi. Kuna pia kosa la kutumia vipashio visivyo sahihi kimuundo kama katika mifano 3.4 (b) ziara 'hio', mfano 3.5 (e) ule wazimu na Jedwali 3.3 (b) 'viti hivo'.

### 3.1.1.4 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi /Tarakimu

Kauli tano zilitumika kuchunguza uwezo wa wanafunzi wa kupatanisha vivumishi vya idadi (tarakimu) na nomino za ngeli za A/WA, KI/VI na LI/YA. Jedwali 3.4

linaonyesha matokeo ya majibu yao.

**Jedwali 3.4 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi**

| **Ngeli** | **Kauli** | **Majibu ya wanafunzi** | **Idadi ya wanafunzi** | **Asilimia ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Wana warandandu waenda mbuwenyi. (Watoto sita wameenda shambani) | Watoto sita wameenda shambani. | 23 | 76.6 |
| | | *Watoto wasita wameenda shambani. | 7 | 23.33 |
| | b) Watu -kumi wamefika | Watu kumi wamefika. | 21 | 70 |
| | | *Watu wakumi wamefika | 9 | 30 |
| KI/VI | Vitiri vina vachika | Viti vinne vimevunjika. | 29 | 96.66 |
| | | *Viti nne vimevunjika. | 1 | 3.33 |
| | c) Mkonu goka na vala visanu | Mkono una vidole vitano. | 25 | 83.33 |
| | | *Mkono una vidole tano. | 5 | 16.67 |
| LI/YA | d) Amenunua maembe -nane | *Amenunua maembe nane. | 14 | 46.66 |
| | | Amenunua maembe manane. | 16 | 53.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kauli za Jedwali 3.4 (a) na (c) ni za kutafsiri kauli za Kitaita kwa Kiswahili na (b) na (d) ni za kukamilisha kwa viambishi mwafaka. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu, baadhi ya wanafunzi walikosea upatanishaji wa nomino za ngeli ya A/WA na tarakimu sita na kumi kama inavyodhihirika katika kauli za Jedwali 3.4 (a) na (c). Waliokosea waliandika ‘watoto wasita’ (23.33%) na ‘watu wakumi’ (30%) mtawalia.

Wanafunzi wote walipatanisha vizuri nomino‘viti’ ya ngeli ya KI/VI na tarakimu nne. Hata hivyo, asilimia 16.67 ya wanafunzi walishindwa kupatanisha nomino ‘vidole’ na tarakimu ‘tano’. Muundo potofu walioandika ni ‘vidole tano’. Aidha,

asilimia 46.66 ya wanafunzi walikosea upatanishaji wa nomino ya ngeli ya LI/YA na tarakimu nane. Waliokosea waliandika, 'maembe nane'. Tulibainisha mifano ifuatayo ya makosa ya kategoria hii katika tungo na masimulizi ya wanafunzi.

(3.6) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…Mtu moja pekee…* | *…Mtu mmoja pekee…* |
| *b.* | **Magari yalikuwa mingi…* | *Magari yalikuwa mengi…* |
| *c.* | **Familia ya mzee Mwasi ilikuwa na mali mingi sana.* | *Familia ya mzee Mwasi ilikuwa na mali nyingi sana.* |

(3.7) Masimulizi

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…ukisikia kelele mingi ujue simba wamelala…* | *… ukisikia kelele nyingi ujue simba wamelala…* |
| *b.* | **Akachukua mikate mbili akakimbia nazo.* | *Akachukua mikate miwili akakimbia nayo.* |
| *c.* | **Alibaki na ng'ombe chache* | *Alibaki na ng'ombe wachache.* |
| *d.* | **ng'ombe mbili kubwa ziliibwa* | *ng'ombe wawili wakubwa waliibwa.* |

Kulingana na mifano hii, baadhi ya makosa yalitokana na kutotumia viambishi awali mwafaka kwenye vivumishi husika vya idadi kama vile katika mfano 3.6 (b) 'magari mingi', mfano 3.7 (a) kelele mingi na (b) mikate mbili. Pia kuna kosa la kutoambisha kiambishi cha ngeli kwenye kivumishi cha idadi kama ilivyo katika mfano 3.7 (c) ng'ombe chache.

Ufafanuzi wetu wa chanzo cha makosa haya ulionyesha kuwa upatanishaji mbaya wa nomino na tarakimu ulitokana na hali mbili tofauti. Kwanza kwa mujibu wa nadharia ya UL, wanafunzi waliathiriwa na $L_1$. Katika Kitaita, tarakimu 1, 2, 3, 4, 5, na 6 huambishwa kiambishi cha ngeli ilhali katika Kiswahili tarakimu

zinazoambishwa ni 1, 2, 3, 4, 5 na 8 (Taz. § Jedwali 2.5 na § Jedwali §2.13). Hivyo basi kusema ‘watoto wasita’ na ‘maembe nane’ kunatokana na kuhamisha ufahamu wao kuhusu matumizi ya tarakimu hii, kutoka $L_1$ hadi $L_2$.

Ujumuishaji mno wa kanuni za sarufi ya Kiswahili ni chanzo kingine cha matatizo kinachodhihirika bayana. Hili hasa linahusiana na utumizi wa viambishi ngeli kwenye upatanishaji wa kisarufi. Kwa mfano, vile vya wingi vimetumika pasipostahili katika kauli ‘watoto wakumi’, na ‘watoto wasita’.

### 3.1.1.5 Upatanishi wa nomino na kivumishi kiulizi

Kauli tatu zilitumika kwenye hojaji kuchunguza matumizi ya viulizi gani na –pi miongoni mwa wanafunzi na matokeo yamewasilishwa katika Jedwali 3.5 kama ifuatavyo.

**Jedwali 3.5: Upatanishi wa nomino na kiulizi**

| Ngeli | Kauli | Majibu ya wanafunzi | idadi ya wanafunzi | Asilimia ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Ni mtoto -gani ameenda? | Ni mtoto gani ameenda? | 5 | 16.67 |
| | | *Ni mtoto mgani ameenda? | 25 | 83.33 |
| | b) Umeadhibiwa na mwalimu -upi? | Umeadhibiwa na mwalimu yupi? | 26 | 86.67 |
| | | *Umeadhibiwa na mwalimu upi? | 4 | 13.33 |
| KI/VI | c) Mama amepika chakula -gani? | Mama amepika chakula gani? | 5 | 16.67 |
| | | *Mama amepika chakula kigani? | 25 | 83.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Matokeo ya jedwali yanaonyesha kuwa upatanishaji wa kivumishi kiulizi 'gani' uliwatatiza wanafunzi wengi ambapo asilimia 83.33 walishindwa kukipatanisha na nomino za ngeli za A/WA na KI/VI. Waliokosa waliandika, Jedwali 3.5(a) 'mtoto mgani' na (c) 'chakula kigani' mtawalia. Kawaida kivumishi 'gani' hakiambishwi kiambishi awali cha nomino. Kuna uwezekano kuwa wanafunzi waliathiriwa na Kitaita kwani viulizi vyote katika Kitaita huambishwa viambishi vya ngeli (Taz. § 2.2.2.3). Wanafunzi walihamisha kanuni za kisarufi za maumbo ya viulizi vya Kitaita kwa $L_2$. Asilimia 13.33 ya wanafunzi ndio tu walioshindwa kupatanisha ipasavyo nomino 'mwalimu' na kivumishi kiulizi '–pi' kwani waliandika, Jedwali 3.5 (b) 'mwalimu upi'. Hili huenda ni kosa la hijai. Mazoezi yaliyohusisha insha na masimulizi hayakubainisha makosa ya kategoria hii.

**3.1.1.6 Upatanishi wa nomino na vivumishi vya pekee**

Kauli nne zilitumiwa kuchunguza umahiri wa wanafunzi katika kupatanisha vivumishi vya pekee na nomino za ngeli mbalimbali kama ilivyo katika Jedwali 3.6.

**Jedwali 3.6: Nomino na vivumishi vya pekee**

| Ngeli | Kauli | Majibu ya wanafunzi | Idadi ya wanafunzi | asilimia ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Nzi -enyewe –mekufa | Nzi mwenyewe amekufa.<br>*Nzi yenyewe imekufa. | 10<br>20 | 33.33<br>66.67 |
| U/I | b) Miembe –ote –li- mea ni mizuri | Miembe yote iliyomea ni mizuri.<br>*Miembe zote zilizomea ni mizuri. | 16<br>14 | 53.33<br>46.67 |
| I | c) Chai -ote –meisha | Chai yote imeisha.<br>*Chai chote kimeisha. | 13<br>17 | 43.33<br>56.67 |
| KI/VI | d) Viti -ote vimevunjika | Viti vyote vimevunjika.<br>*Viti vote vimevunjika. | 29<br>1 | 96.66<br>3.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Matokeo ya uchunguzi kama yalivyowasilishwa katika Jedwali 3.6, yalionyesha kutatizika kwa wanafunzi kwa kiasi fulani katika kupatanisha ‘-ote’ na ‘-enyewe’ na baadhi ya nomino ijapokuwa hili halikubainika katika masimulizi na insha. Wanafunzi asilimia 66.67 walishindwa kupatanisha nomino (nzi) ya ngeli ya A/WA na kivumishi cha pekee ‘enyewe’ kama inavyobainika katika Jedwali 3.6 (a). Hawa waliandika ‘nzi yenyewe’ ambapo walikosea kwa kuambatanisha kiambishi potofu ‘ye-’ badala ya ‘mw-’.

Upatanishaji wa nomino ya ngeli ya U/I na kivumishi -ote pia ulitatiza asilimia 46.67 ya wanafunzi ambao waliandika ‘miembe zote’. Huenda hili ni kosa la uhamishaji wa kanuni za vipatanishi vya Kitaita kuhusu ngeli ya majina ya miti *(MU/MI)* ambayo ina viambishi viwili vya upatanishi (wingi) ilhali ngeli ya Kiswahili ya U/I, ina kipatanishi kimoja tu cha wingi.

Ngeli ya I/I pia iliwatatiza wanafunzi wengi kwani asilimia 56.67 waliandika muundo potofu wa upatanishaji wa kisarufi inavyodhihirika katika Jedwali 3.6 (d) ‘chai chote’. Hili huenda ni kosa la ujumuishaji mno wa viambishi vipatanishi vya ngeli ya KI/VI ambayo aghalabu hujumisha nomino zenye vianzio vya umoja na wingi: ki-/vi- na ch-/vy-. Upatanishaji wa ngeli ya K/VI haukuwatatiza wanafunzi karibu wote isipokuwa asilimia 3.33 pekee. Aliyekosea aliandika ‘viti vote’ ambalo huenda ni kosa la tahajia.

### 3.1.1.7 Upatanishi wa nomino na kivumishi cha ‘-a’ unganifu

Kivumishi cha ‘-a’ unganifu huambishwa kwa kipatanishi cha kisarufi cha ngeli ya nomino inayomilikiwa. Mifano ya makosa katika kipengele hiki yalidhihirika katika kauli zifuatazo kwenye insha na masimulizi ya wanafunzi.

(3.8) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…bahari la samaki* | *… bahari ya samaki* |
| *b.* | **…kituoni cha polisi* | *… kituo cha polisi* |
| *c.* | **…chai cha jioni* | *…chai ya jioni* |
| *d.* | **Viatu va wasimamizi vilikuwa vizuri* | *Viatu vya wasimamizi vilikuwa vizuri.* |

(3.9) Masimulizi

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Walifanya bidii za mchwa.* | *Walifanya bidii ya mchwa.* |
| *b.* | **Vitu va ndani va mnyama.* | *Viungo vya ndani vya mnyama.* |

Mifano hii inaonyesha vipashio vyenye matumizi ya‘a’-unganifu ambayo si sahihi kama vile katika mifano 3.8 (a) bahari la, (b) kituoni cha (c) chai cha. Tatizo la kusema ‘chai cha’ badala ya ‘chai ya’ ni la ujumuishaji. Katika mfano 3.8 (d) Viatu ‘va’ wasimamizi na mfano 3.9 (b) Vitu ‘va’ ndani, wanafunzi walidondosha kitamkwa ’y’ katika kivumishi. Hili huenda pia lilitokana na athari ya Kitaita ambapo kisarufi kunatumika kipatanishi ‘{va}’ katika ngeli ya KI/VI kwenye kivumishi cha ‘a’ unganifu, ilhali katika Kiswahili ni ‘vy’. Hivyo basi hili ni tatizo la uhamishaji wa miundo ya kisarufi ya $L_1$ hadi $L_2$.

### 3.1.2 Makosa yanayohusu urejeshi wa nomino katika vitenzi

Kirejeshi hutumiwa kuonyesha kuwa nomino iliyotajwa inahusika na kitendo fulani. Katika Kiswahili Sanifu, kiambishi cha urejeshi huwa na upatano na kiima kinachorejelewa. Isitoshe, viambishi hivyo vya urejeshi hutegemea ngeli ya nomino. Katika kategoria hii ya urejeshi wa nomino katika vitenzi, wanafunzi walifanya makosa ya aina mbalimbali kama ilivyodhihirika katika mazoezi ya hojaji, tungo na masimulizi yaliyotumika. Katika hojaji, wanafunzi walipewa kauli tatu zenye mapengo wajaze kwa viambishi mwafaka vya urejeshi. Makosa yaliyofanywa na wanafunzi kuhusu urejeshi wa nomino katika vitenzi yalibainishwa katika Jedwali 3.7.

**Jedwali 3.7: Urejeshi wa nomino katika vitenzi**

| **Ngeli** | **Kauli** | **Majibu ya wanafunzi** | **idadi** | **Asilimia ya wanafunzi** | **% ya jumla ya makosa** |
|---|---|---|---|---|---|
| A/WA | a) Mvulana ali-kuja ni huyu. | Mvulana aliyekuja ni huyu.<br>*Mvulana aliokuja ni huyu. | 12<br>18 | 40<br>60 | 60 |
| U/I | b) Miembe -li-mea ni mizuri | Miembe iliyomea ni mizuri<br>*Miembe zilizomea ni mizuri<br>*Miembe iliomea ni mizuri | 19<br>7<br>4 | 63.33<br>23.33<br>13.33 | 36.67 |
| I | c) Nyumba ina-jengwa ni yangu | Nyumba inayojengwa ni yangu<br>*Nyumba inaojengwa ni yangu | 29<br>1 | 96.66<br>3.33 | 3.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kwa mujibu wa matokeo haya, urejeshi wa nomino katika kitenzi uliwatatiza baadhi ya wanafunzi kama inavyodhihirika katika majibu waliyotoa. Asilimia 60 ya wanafunzi walikosea katika urejeshi wa nomino ‘mvulana’ (ngeli ya A/WA) katika kitenzi ‘kuja’. Muundo potofu uliodhihirika ni ‘mvulana aliokuja ni huyu’. Aidha, urejeshi wa nomino ‘miembe’ (ngeli ya U/I) na ‘nyumba’ (ngeli ya I/ZI) uliwatatiza wanafunzi kwa viwango vya 36.67% na 3.33% mtawalia. Miundo ya majibu yao potofu ni kama inavyodhihirika katika Jedwali 3.7 (b) ‘Miembe iliomea ni mizuri’ na (c) ‘Nyumba inaojengwa ni yangu’.

Tatizo la wanafunzi kuhusiana na urejeshi wa vitenzi katika nomino pia lilidhihirika katika insha na masimulizi yao kama inavyobainika katika mifano

ifuatayo:

(3.10) Insha

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Ndugu yangu alikuwa kidato cha tatu alikuwa akifaulu sana.* | *Ndugu yangu alipokuwa katika kidato cha tatu alikuwa akifaulu sana.* |
| *b.* | **Baba akasema kwamba huoni vyenye tumefanana?* | *Baba akauliza, "huoni tunavyofanana?"* |
| *c.* | **Mama yetu mwenye alikuwa anatusimamia….* | *Mama yetu aliyekuwa akitusimamia….* |
| *d.* | **Walianza kutoa watu walio ndani ya gari ya gari.* | *Walianza kutoa watu waliokuwa ndani/ambao walikuwa ndani ya gari.* |
| *e.* | **Nikafika mahali ambapo nilipoziacha mzigo wangu.* | *Nikafika mahali nilipouacha/ ambapo nilikuwa nimeuacha mzigo wangu.* |
| *f.* | **Miezi iliobaki* | *Miezi iliyobaki* |

(3.11) Masimulizi

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **vyenye alikutananga na yule jitu…* | *Alipokutana na jitu lile…* |
| *b.* | **Vile alipelekwanga kwa nyumba ya yule jitu…* | *Alipopelekwa nyumbani mwa lile jitu…* |
| *c.* | **vyenye walienda shambani…* | *Walipoenda shambani…* |
| *d.* | **vyenye huyu nyanya alikuja…* | *Nyanya huyo alipokuja* |

Baadhi ya makosa haya yanahusisha kutochopeka kiambishi cha urejeshi cha ngeli ya nomino kwenye kitenzi kama vile katika mfano 3.10 (a) ndugu yangu alikuwa kidato cha tatu… (d) Walianza kutoa watu walio ndani ya gari. Pia kuna matumizi yasiyofaa ya '–enye' badala ya kutumia 'amba- 'au 'o' rejeshi kwa mfano, katika mfano 3.10 (c) 'mama yetu mwenye alikuwa anatusimamia….' Mifano 3.11 (c) vyenye walienda shambani na (d) vyenye huyu nyanya alikuja.

Isitoshe, kuna kosa la ukiukaji wa sheria ya kutotumia virejeshi ‘amba’ na ‘o’ kwa wakati mmoja kurejelea kitu kimoja kama vile katika mfano, 3.10 (e) ‘mahali **amba**po nili**po**ziacha’. Virejeshi hivi hutumika kwa ubadalia. Pia, kuna miundo potofu ya kauli zilizotumia kiambishi *{–nga}* mwishoni mwa vitenzi badala ya viambishi sahihi vya urejeshi kama vile mifano 3.11 (a) ‘vyenye *alikutana**nga*** na yule jitu’ na (b) ‘…*alipelekwa**nga*** kwa nyumba ya yule jitu’.

Baadhi ya makosa haya huenda yalitokana na uhamishaji wa ufundishaji unaotokana na athari ya $L_1$ hasa ikiwa mwalimu ana shida ya kimatamshi kuhusu utamkaji wa ‘o’ na ‘yo’. Kwa mfano, 3.10 (f) ‘Miezi ili**o**baki’ badala ya ‘miezi ili**yo**baki’. Wanafunzi huenda pia wamejifunza miundo potofu ya urejeshi kupitia kwa watumizi wengine wa Kiswahili kwani ni kawaida kusikia watu mbalimbali wakichanganya matumizi ya ‘amba’ na ‘o’ rejeshi wanapozungumza hata katika vyombo vya habari. Hiki huenda pia ndicho chanzo cha kuongeza kiambishi tamati {-nga} mwishoni mwa vitenzi visivyo kwa mfano, katika 3.11 (a) alikutana**nga** na (b) alipelekwa**nga** kwa nyumba.

Makosa mengine huenda yalitokana na uhamishaji wa kanuni za kisarufi za urejeshi kutoka Kitaita ambapo tuliona kuna njia mbalimbali za kuonyesha urejeshi (Taz § 2.2.3). Katika Kitaita, kinyume na ilivyo katika Kiswahili, urejeshi unaweza kuhusisha matumizi ya kiashiria cha mbali kinachowekwa kabla ya kitenzi kinachorejeshwa kwa nomino. Tunavyoona ni kuwa hili limewaathiri

wanafunzi kama inavyodhihirika katika mifano ya 3.1.1(a) ‘**Vyenye** alikutana**nga** na yule jitu’ na (c) ‘**vyenye** walienda shambani’.

## 3.2 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa

Kwa mujibu wa Shahim (2011), kiwango cha utokeaji wa makosa hubainishwa katika kuyachunguza na ndicho huzingatiwa katika nadharia ya UM ili kudhihirisha ujuzi wa mwanafunzi wa $L_2$. Kwa kuzingatia data za matokeo ya mazoezi yetu ya uchunguzi, tuliweza kukadiria viwango vya kategoria mbalimbali za makosa kama ifuatavyo.

### 3.2.1 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa katika insha

Uchunguzi uliweza kutubainishia aina mbalimbali za makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wote walioshirikishwa katika utafiti ambao kwa jumla walikuwa 30. Matokeo ya uchunguzi wetu yamewasilishwa katika Jedwali 3.8 ambalo linaonyesha kategoria mbalimbali za makosa ya kisarufi yaliyodhihirika katika insha za wanafunzi, idadi ya wanafunzi waliofanya makosa katika kila kategoria na ni asilimia kiasi gani. Hili lilisaidia kujua ni kategoria ipi inayowatatiza zaidi wanafunzi kwa kuzingatia viwango vyao kiasilimia. Matokeo halisi ya uchunguzi wetu yanaonyeshwa katika Jedwali 3.8.

**Jedwali 3.8: Viwango vya makosa katika insha**

| Kategoria | Idadi ya wanafunzi | asilimia |
|---|---|---|
| vivumishi vya sifa | 2 | 6.67 |
| vivumishi viashiria | 2 | 6.67 |
| vivumishi vya idadi | 3 | 10 |
| vivumishi vya ‘ a –unganifu | 3 | 10 |
| Urejeshi | 14 | 46.7 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kwa kuzingatia data za matokeo zilizomo katika Jedwali 3.8, kategoria ya makosa iliyokuwa ya kiwango cha juu zaidi ni ya urejeshi iliyofanywa na jumla ya wanafunzi 14 ambayo ni asilimia 46.7 ya wanafunzi wote. Hili linaonyesha kuwa wanafunzi Wataita wangetatizika zaidi kujifunza kipengele hiki cha urejeshi katika Kiswahili Sanifu kushinda vipengele vingine vyote. Tofauti zilizoko katika Kitaita na Kiswahili kuhusiana na dhana ya urejeshi huenda zimechangia hali hii kama ilivyobashiriwa na UL (Taz. § 2.3.2).

Makosa yaliyohusisha vivumishi vya ‘a’ unganifu na yale yaliyohusisha tarakimu yote yalifanywa na wanafunzi watatu watatu ambayo ni asilimia 10. Nayo makosa yaliyokuwa ya kiwango cha chini zaidi yalikuwa ya upatanishaji wa nomino na viashiria pamoja na yale yaliyohusisha vivumishi vya sifa ambayo yalichukuwa asilimia 6.67 kila mojawapo na yalifanywa na wanafunzi wawili wawili. Hali hii inaonyesha kuwa wanafunzi Wataita hawatatiziki sana wanapojifunza vipengele hivi.

### 3.2.2 Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa katika masimulizi

Kubainisha viwango vya kategoria za makosa mbalimbali yaliyodhihirishwa katika data zilizokusanywa ilikuwa muhimu ili kutambua ni kategoria gani iliyowatatiza zaidi wanafunzi.Viwango vya kategoria mbalimbali za makosa yaliyoweza kubainishwa katika masimulizi yalionyeshwa katika Jedwali 3.9.

**Jedwali 3.9: Viwango vya makosa ya wanafunzi katika masimulizi**

| **Kategoria** | **Idadi ya wanafunzi** | **Asilimia ya wanafunzi** |
|---|---|---|
| vivumishi vya sifa | 6 | 20 |
| vivumishi viashiria | 8 | 26.67 |
| vivumishi vya idadi | 4 | 13.33 |
| vivumishi vya a –unganifu | 2 | 6.67 |
| Urejeshi | 15 | 50 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Matokeo ya uchunguzi yanaonyesha kuwa wanafunzi walionekana kutatizika zaidi katika urejeshi wa vitenzi katika nomino ambapo wanafunzi 15 walifanya makosa ikiwa ni asilimia 50. Aidha, katika upatanishaji wa nomino na vivumishi viashiria, kulikuwa na jumla ya wanafunzi 8 waliofanya makosa ambayo ni asilimia 26.67. Wanafunzi 6 walifanya makosa yaliyohusisha vivumishi vya sifa ambayo ni asilimia 20. Vilevile kulikuweko na wanafunzi 4 waliofanya makosa ya upatanishaji wa nomino na vivumishi vya idadi ambayo ni asilimia 13.33 ya jumla ya wanafunzi wote. Kategoria ya makosa yaliyohusu kivumishi cha ‘a’

unganifu ndiyo iliyodhihirisha kiwango cha chini zaidi. Haya yalifanywa na wanafunzi 2 ambao ni asilimia 6.67 ya wanafunzi wote.

Kwa jumla, tukilinganisha idadi ya kila kategoria ya makosa yaliyofanywa katika insha na katika masimulizi; ni wazi kuwa wanafunzi wengi walifanya makosa mengi zaidi katika masimulizi. Hili limechangiwa na hali kuwa mtu anapoongea hafikirii sana kabla ya kuongea ilhali anapoandika huweza kuwazia anachosema na hivyo kujikosoa kabla ya kulitumia neno.

Tunaona pia kuwa kwa kila zoezi la uchunguzi, kategoria iliyowatatiza wanafunzi wengi zaidi ni ya urejeshi wa vitenzi katika nomino. Hili huenda linaonyesha ugumu ulioko katika kujifunza kanuni za kisarufi za Kiswahili zinazohusiana na virejeshi. Swala la ugumu wa kujifunza lugha kama jambo linalosababisha wanafunzi kutatizwa na baadhi ya mifumo ya lugha lengwa limezungumziwa pia na Obara (2014). Ugumu huu unatokana na hali kuwa tayari mwanafunzi amezoea sarufi na mifumo ya $L_1$ ambayo inakuwa msingi wa $L_2$. Hivyo basi, anajikuta mara kwa mara akirejelea lugha yake ya kwanza hata akifikiria kwa $L_1$ kisha akabadilisha kauli kwa $L_2$. Wanafunzi Wataita huenda wameathirika na hali hii kwani tulivyoona katika § 2.3.2 ni kuwa kuna tofauti kadha kuhusu dhana ya urejeshi katika Kitaita na Kiswahili Sanifu. Urejeshi katika Kitaita unahusisha viambishi tamati pekee ilhali katika Kiswahili kuna viambishi awali na tamati.

Aidha, katika Kitaita kuna matumizi ya kiashiria cha mbali baada ya nomino inayorejelewa; jambo ambalo haliko katika Kiswahili.

Matokeo kuhusu ugumu wa dhana ya virejeshi kwa wanafunzi Wataita yanaoana na tafiti zingine zilizotangulia kama vile Ntawiyanga (2015). Kwa mujibu wa utafiti wake, tatizo la wanafunzi kuhusu virejeshi lilitokana na kuwepo kwa mifumo tofauti ya dhana ya urejeshi katika Kiswahili na Kinyarwanda. Hali hii pia imedhihirika wazi kati ya Kiswahili na Kitaita katika utafiti wetu. Aidha, Ntawiyanga (2015) anadai kuwa mifumo ya Kiswahili ya kubainisha urejeshi ni changamani zaidi kuliko ya Kinyarwanda. Hili bila shaka linazua ugumu wa aina yake kwa wanafunzi wanapotunga sentensi zenye urejeshi katika Kiswahili.

### 3.3 Aina mbalimbali za Makosa ya kisarufi katika kazi za wanafunzi

Baada ya kuyabainisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi kwa mujibu wa mazoezi mbalimbali ya utafiti walioshiriki kwayo, makosa yaliainishwa kwa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM). Hili lilitekelezwa kwa kuzingatia mhimili wa tatu wa nadharia hii unaoelekeza kuhusu ufafanuzi wa makosa yaliyokwisha kubainishwa (Taz. § 1.8.2.1). Kwa kulinganisha semi za wanafunzi kama zilivyodhihirika katika data tulizokusanya na miundo sahihi inayopaswa kuzingatiwa katika Kiswahili Sanifu; Makosa ya kisarufi yafuatayo yaliweza kubainishwa miongoni mwa wanafunzi (Taz. § 3.3.1 – 3.3.7).

### 3.3.1 Matumizi ya viambishi vipatanishi vya ngeli visivyofaa

Katika Kiswahili Sanifu, mtu anahitaji kuteua kipatanishi kinachowiana na maneno mengine yaliyo katika sentensi. Ukiushi wa kanuni hii unasababisha kosa la kisarufi. Wanafunzi walifanya makosa mbalimbali katika upatanishaji wa kisarufi wa nomino na vitenzi au vivumishi kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

*(3.12)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Muda **zi**lienda haraka….* | *Muda ulienda haraka* |
| *b.* | **Maisha **i**limwendea shwari* | *Maisha yalimwendea shwari.* |
| *c.* | **Nzi **i**kipita inakatwa.* | *Nzi akipita anakatwa* |
| *d.* | **Ukisikia kelele **mi**ngi…* | *Ukisikia kelele nyingi* |
| *e.* | **Ujinga wake **i**lizidi* | *Ujinga wake ulizidi* |
| *f.* | **Yai **i**mepasuka* | *Yai limepasuka* |
| *g.* | **Chai **ki**meisha* | *Chai imeisha* |
| *h.* | **Jitu **a**likuwa ni mkubwa tu* | *Jitu **li**likuwa kubwa tu* |
| *i.* | **…alikuwa na kagari dogo* | *… alikuwa na kigari kidogo* |

Mifano hii inaonyesha vile wanafunzi walivyochanganya viambishi kwa kuambisha viambishi visivyofaa kwenye vitenzi au vivumishi. Kwa kawaida uteuzi wa viambishi hutegemea uainishaji wa nomino inayohusika. Iwapo nomino itaainishwa katika ngeli fulani, basi itatumia viambishi vya ngeli hiyo. Kwa kuzingatia hili, ni wazi kuwa kilichosababisha wanafunzi wengi kutumia vipatanishi visivyofaa ni kuainisha nomino husika katika ngeli zisizo sahihi. Kwa mfano, nomino ‘nzi’ imeainishwa katika ngeli ya I/ZI na ‘chai’ katika ngeli ya KI/VI katika mifano 3.12 (c) na (g).

Katika Kiswahili, nomino huweza kuwa katika hali tatu kuu: hali ya udogo, hali ya wastani (kawaida) na ya ukubwa. Viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya nomino zikiwa katika hali mbalimbali hutofautiana. Nomino zikiwa katika ukubwa huchukua viambishi vya ngeli ya LI/YA na za udogo ile ya KI/VI. Ni makosa kutumia kipatanishi kisichofaa kwa nomino kwa mfano, kutumia cha hali ya wastani kwa nomino ya ukubwa au udogo kama vile katika 3.12 (h) na (i)

Kauli hizi potofu zinadhihirisha wazi kuwa upatanishaji wa nomino za ukubwa na za udogo ulitatiza wanafunzi. Kiambishi ‘a-’ katika 3.12 (h) ni cha kupatanisha nomino ‘mtu’ ambayo ni ya wastani. Nazo nomino za udogo hupatanishwa na ‘ki’ wala si ‘ka’. Lililo wazi hapa ni kuwa mwanafunzi amehamisha kiambishi ‘ka’ cha udogo kutoka Kitaita, hadi Kiswahili.

### 3.3.2 Uongezaji vipashio au sauti pasipostahili

Baadhi ya wanafunzi walifanya kosa la kupachika vipashio/sauti kwenye maneno au sentensi mahali ambapo hapakustahili kama tunavyoona kwenye mifano ifuatayo:

*(3.13)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Alikuwa na gari **n**dogo.* | *Alikuwa na gari dogo* |
| *b.* | **Kituo**ni** cha polisi* | *kituo cha polisi* |
| *c.* | **Mtoto **m**gani ameenda?* | *Mtoto gani ameenda?* |
| *d.* | **Watu **wa**kumi wamefika* | *Watu kumi wamefika* |
| *e.* | ** …Vyenye alikutananga na yule jitu* | *Alipokutana na lile jitu.* |
| *f.* | **Tukaanza kurudi sisi nyumbani* | *Tukaanza kurudi* |

| | |
|---|---|
| *zetu polepole* | *nyumbani polepole* |

Katika mifano hii, wanafunzi walichopeka sehemu ambazo hazikutarajiwa kuwa katika tungo zao. Katika baadhi ya tungo waliongeza viambishi kama vile {–ni} katika (3.13) b. Isitoshe kuna viambishi ambavyo vimeongezwa kwenye vivumishi vya sifa (3.13) a, viulizi (3.13) c na vya idadi (3.13) d, visivyostahili kuchukua viambishi vya ngeli. Kwingineko, wanafunzi walichopeka neno '–enye' na hasa pale ambako walistahili kutumia kirejeshi kama katika (3.13) e. Katika (3.13) f maneno 'sisi' na 'zetu' yamechopekwa kwenye kauli na hayana umuhimu wowote pale.

### 3.3.3 Udondoshaji wa vitamkwa au maneno katika tungo

Makosa ya aina hii yalijitokeza pale ambapo mwanafunzi alikosa kuandika sauti, kiambishi au neno katika nafasi fulani kwenye kauli yake. Hili linafanya kauli husika iwe na upungufu ambao unaweza hata kuathiri ujumbe unaowasilishwa ukakosa kueleweka vizuri. Mfano ufuatao unathibitisha hili:

*(3.14)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **ule wazimu aliyekuwa mbuzi* | *Yule wazimu aliyekuwa mbuzi…* |
| *b.* | **Vitu va ndani va mnyama* | *Viungo vya ndani vya mnyama* |
| *c.* | **Vitu vyote hivo nilivoviona* | *Vitu vyote hivyo nilivyoviona…* |
| *d.* | **Kulikuwa na mtu mmoja anaitwa Majisi.* | *Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa akiitwa Majisi.* |

Katika mfano (3.14) a, b na c kuna makosa ya udondoshaji wa sauti au viambishi katika maneno. Matokeo haya yanaonyesha vile wanafunzi walivyotatizika na

matumizi ya virejeshi katika baadhi ya kauli kama vile (3.14) d kwani ni wazi kuwa wamevidondosha.

### 3.3.4 Mpangilio potofu wa vipashio katika sentensi

Kimuundo, sentensi za Kiswahili zilizo sahihi kisarufi huanza kwa nomino ya mtenda, mtendwa au mtendewa. Maneno yanayotumiwa katika aina fulani ya sentensi yanastahili kufuatanishwa vizuri katika vipashio vyake mbalimbali ili ujumbe usivurugike. Aidha, vipashio kama vile virai vya aina mbalimbali vinastahili kuzingatia muundo fulani. Mifano ya kauli zenye mipangilio potofu zilizodhihirika katika data zilizokusanya ni kama vile:

*(3.15)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Basi sungura ilikuwa usiku akaenda akalala* | *Basi ilipofika usiku, sungura alienda akalala.* |
| *b.* | **huyo ni nani ako kwa mti juu?* | *Ni nani huyo aliye juu ya mti?* |
| *c.* | ** Siku ifuatayo tulimtembelea familia yetu.* | *Familia yetu ilimtembelea siku iliyofuata.* |
| *d.* | **Nikaenda shule alayansi ya wavulana na kufurahi sana.* | *Nilifurahi sana nilipoenda shule ya wavulana ya Alliance.* |
| *e.* | **Hii shamba si yetu* | *Shamba hili si letu* |
| *f.* | ** Ile siku majibu yalitoka* | *Siku ile majibu yalitoka.* |

Sentensi hizi zinakanganya kwa mfano, ni vigumu kubainisha kishazi huru na tegemezi kwenye sentensi changamano, kama vile inavyodhihirika katika mfano (3.15) a na d. Isitoshe, kuna shida ya kauli kutozingatia muundo wa kiima kutangulia kiarifa kwa mfano, katika (3.15) c. Tunaona pia kuna hali ya kategoria

za maneno kubadilishana nafasi visivyo katika baadhi ya kauli kama vile katika mfano (3.15) b, e na f.

### 3.3.5 Kuchanganya vipashio

Wanafunzi walichanganya vipashio vya viwango mbalimbali katika kauli zao. Hii ilihusisha kutumia upatanisho na kategoria za maneno yasiyo mwafaka kama inavyodhihirika katika mfano 3.16 ufuatayo:

*(3.16)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **…bahari la samaki* | *… bahari ya samaki* |
| *b.* | **…chai cha jioni* | *…chai ya jioni* |
| *c.* | **…aliendelea kusoma kwa chuo chake kikuu.* | *…aliendelea na masomo yake katika chuo kikuu.* |
| *d.* | **Vyenye alifungwanga na kamba …* | *Alipofungwa kwa kamba* |
| *e.* | **Akapika chapati na maharagwe.* | *Akapika chapati kwa maharagwe.* |
| *f.* | **Alipata faida nzuri katika mimea yake.* | *Alipata faida nzuri kwa mimea yake.* |

Katika mifano hii, wanafunzi walifanya makosa ya kuambisha viambishi visivyo mwafaka kupatanisha nomino na maneno mengine kwa mfano katika (3.16) a, b. Pia, kuna makosa yaliyohusisha matumizi ya kategoria fulani za maneno visivyo hivyo kuvuruga ujumbe kama vile ‘kwa’ katika (3.16) c, ‘na’ katika (3.16) d, na e.

### 3.3.6 Uakifishaji wenye makosa

Kulingana na Waihiga na Wamitila (2003), kuakifisha ni kutumia alama mbalimbali maalum katika maandishi ili kuweza kuwasiliana na msomaji. Tungo

za wanafunzi zilidhihirisha makosa mengi ya uakifishaji ya aina mbalimbali, kwa mfano:

*(3.17)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Tulipomuuliza yule mama wale wezi ndio wamekuibia akasema ndiyo.* | *Tulimuuliza yule mama, "Wezi wale ndio wamekuibia?" Akajibu, "Ndio",* |
| *b.* | **…mama akaniambia shika mia tano uwende ukalipie feya ya basi nikamwambia asante mama.* | *…Mama akaniambia, "Shika shilingi mia tano utumie kulipia nauli. Nikamwambia, "Asante, mama".* |
| *c.* | **Nikamsalimia shikamoo babu Akaniitikia marahabaa nikamuuliza hapa wakati wa mvua…* | *Nikamsalimia, "Shikamoo babu?" Akanijibu, "Marahabaa. Nikamuuliza ikiwa wakati wa mvua hapo…* |
| *d.* | ** Tulienda tarehe mbili mombasa kwa sababu tukajaribu nguo za harusi kama zinatutosha.* | *Tulienda Mombasa tarehe mbili ili tukajaribu nguo zetu kama zilitutosha.* |
| *e.* | ** Ilikuwa siku ya jumamosi mama akaniambia kesho tulienda shambani mosi.* | *Ilikuwa siku ya Jumamosi mama aliponiambia kuwa siku iliyofuata nilienda shambani huko mosi.* |
| *f.* | **Nikaenda shule alayansi ya wavulana na kufurahi sana.* | *Nilifurahi sana nilipoenda shule ya wavulana ya Alliance.* |

Kutokana na mifano hii, ni wazi kuwa wanafunzi hawajamudu matumizi mwafaka ya viakifishi mbalimbali. Semi ambazo zilinuiwa kuwa maneno halisi ya msemaji hazikufungiwa ipasavyo kwa alama za mtajo. Aidha, kuna mchanganyiko wa sifa za usemi halisi na usemi wa taarifa katika kauli moja, kwa mfano, (3.17) b na c. Pia, kuna matumizi potofu ya herufi ndogo ambapo zinatumika mwanzoni mwa nomino za pekee kama vile katika (3.17) d, e na f. Kukosekana kwa alama za uakifishaji panapostahili kunafanya mwanafunzi

asieleweke vilivyo kwani kauli hazifasiriwi vilivyo. Kwa mfano, kauli ya 3.17 (a) imeandikwa tu kama taarifa ilhali inabeba swali kwani hakuna kiulizi kilichowekwa mahali popote.

### 3.3.7 Urudiaji wa vipashio

Wanafunzi walirudia vipashio isivyostahili kama inavyodhihirika kwenye sehemu zilizokolezwa wino katika mifano ifuatayo:

*(3.18)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Nikachukua mitihani zangu* ***ambazo*** *tuli**zo**zifanya.* | *Nikachukua matokeo ya mitihani ambayo tulifanya.* |
| *b.* | **Nikafika mahali* ***ambapo*** *nili**po**ziacha mzigo wangu.* | *Nikafika mahali nilipouacha mzigo wangu.* |
| *c.* | **Nimezihesabu ng'ombe na ako na* ***ng'ombe*** *ishirini* | *Nimewahesabu ng'ombe wake ni ishirini.* |
| *d.* | **Baba yangu na mama* ***yangu*** *walinipea pesa mia mbili hamsini.* | *Baba na mama yangu walinipa shilingi mia hamsini.* |

Katika mifano hii, shida ya uradidi inasababishwa na utumizi wa 'amba' na 'o' rejeshi katika sentensi moja kurejelea kitu kimoja kama vile katika mifano (3.18) *a* na *b*. Aidha, katika mfano (3.18c) kosa limetokana na kutaja nomino 'ng'ombe' mara mbili badala ya kutumia kirejeshi. Pia, kuna urudiaji usio muhimu wa neno 'yangu' katika (3.18d).

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii tuliweza kubainisha, kufafanua na kuainisha makosa ya wanafunzi kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya UM na UL kama inavyozungumziwa katika §1.8. Kwa kuzingatia mazoezi yote matatu yaliyopewa wanafunzi, kategoria mbalimbali za kisarufi ambazo ziliathirika zilichunguzwa kwa kuzingatia viwango vya utokeaji wake kiasilimia. Hili lilisaidia kufahamu ikiwa tatizo kuhusu kategoria fulani liliathiri wanafunzi au la. Uchunguzi ulidhihirisha kuwa kategoria ya urejeshi wa nomino katika vitenzi ndio huathiri wanafunzi wengi zaidi.  Aidha, ufafanuzi wa makosa yaliyobainishwa uliwezesha kutambua aina mbalimbali za makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi.

Mazoezi yote yaliyohusishwa yalishughulikiwa kwa pamoja ili kubainisha kategoria mbalimbali za makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Zoezi la kukamilisha hojaji hasa lilisaidia kuona vile wanafunzi hutatizwa na upatanishaji wa kisarufi wa ngeli mbalimbali. Nalo zoezi la insha liliwezesha kung'amua matatizo yanayowakumba wanafunzi katika kujieleza kimaandishi; hasa katika kujitungia kauli zilizo sahihi. Aidha, masimulizi ya hadithi yalisaidia kutathmini uwezo wao wa kutunga kauli zilizo sahihi wanapozungumza na kuona matatizo yanayowakumba. Katika sura inayofuata vyanzo vya makosa halisi ya kisarufi ya wanafunzi vilijadiliwa huku uhusiano wao na yale yaliyobashiriwa na nadharia ya UL ukiangaziwa.Vilevile mikakati ya kuyakabili matatizo yanayowakumba wanafunzi ilijadiliwa.

# SURA YA NNE

# CHANZO CHA MAKOSA YA KISARUFI YA WANAFUNZI NA MIKAKATI YA KUYASHUGHULIKIA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunabainisha chanzo cha makosa ya kisarufi ya wanafunzi yaliyobainishwa katika sura ya tatu ili kuonyesha jinsi yanavyohusiana na ubashiri uliofanywa na nadharia ya UL katika sura ya pili. Uchunguzi ulifanywa kuonyesha namna vipengele vilivyobashiriwa kuwa vingesababisha ugumu au urahisi wa ujifunzaji kwa wanafunzi vilithibitishwa au kutothibitishwa kwa mujibu wa uchanganuzi uliofanywa. Haya yalielekezwa na tofauti za kiisimu kati ya $L_1$ na $L_2$ ambazo zinasistizwa katika nadharia ya UL.

Pia, mikakati inayoweza kuzingatiwa kupunguza makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi ilijadiliwa. Juhudi hizi zilielekezwa na mbinu za uchunguzaji wa lugha ya mwanafunzi zinazozungumziwa katika nadharia yetu ya pili ya Uchanganuzi Makosa (UM).

## 4.1 Chanzo cha makosa ya kisarufi ya wanafunzi

Mbaabu (1995) anabainisha kuwa makosa ya kisarufi katika ujifunzaji wa $L_2$ yanaweza kusababishwa na uvunjaji wa kanuni za kisarufi zinazohusiana na vipengele mbalimbali yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Matokeo ya uchunguzi wa data umedhihirisha kuwa makosa ya kisarufi yaliyofanywa na

wanafunzi waliochunguzwa yalikuwa na vyanzo tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu ya $L_1$ hadi $L_2$, ujumuishaji mno wa kanuni za $L_1$, kutojua mipaka ya kaida au sheria za lugha anayojifunza, tafsiri, uhamishaji wa ufundishaji na kutomakinika au kutojali kwa wanafunzi.

### 4.1.1 Uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu

Kwa mujibu wa utafiti huu, wanafunzi Wataita wameathiriwa na mifumo ya lugha yao ya kwanza katika ujifunzaji wao wa Kiswahili Sanifu. Mifano ifuatayo ya kauli za wanafunzi katika Jedwali 4.1, inathibitisha uhamishaji wa vipengele vya kisarufi kutoka lugha ya Kitaita hadi Kiswahili Sanifu.

**Jedwali 4.1: Kauli potofu za wanafunzi zilizotokana na uhamishaji wa vipengele vya kisarufi**

| Kauli za wanafunzi | Tafsiri katika kitaita | Kauli sahihi ya Kiswahili |
|---|---|---|
| a) *Nzi ikipita inakatwa | Izi ikaida yedemwa | Nzi akipita anakatwa |
| b) *…ng'ombe zake… | …ng'ombe rake … | …ng'ombe wake … |
| c) *…kuku ile nyeusi imekufa. | …nguku ija ya chilu yafwa. | …kuku yule mweusi amekufa. |
| d)* Alikuwa na kagari dogo. | Odeka na kaigare katinieri. | Alikuwa na kigari kidogo. |
| e) *Miembe zote zilizomea ni mizuri. | Miembe rose irija ribukie rapoie / Miembe yose ija ibukie yapoie. | Miembe yote iliyomea ni mizuri. |
| f) *Miti zake zimekatwa. | Midi rake redemwa/ Midi yake yedemwa. | Miti yake imekatwa. |
| g) *Chai chote kimeisha. | Chai chose chasia. | Chai yote imeisha. |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Katika Jedwali 4.1, kauli (a, b na c) zinaonyesha wanafunzi walikosea kutumia viambishi {*i-zi*} vya ngeli za 9 na 10 za Kitaita kwa sentensi za Kiswahili zilizotumia majina ya viumbe wenye uhai. Hii ni wazi kuwa walizingatia miundo ya viambishi vya ngeli za Kitaita ambapo nomino za wanyama, ndege na wadudu huainishwa katika ngeli za 9 na 10 (N/N). Nomino za watu pekee ndizo huainishwa katika ngeli ya MU / βA (WA). Katika Kiswahili majina ya viumbe wote wenye uhai yamo katika ngeli moja ya A/WA. Viambishi vipatanishi vya ngeli hii vikiwa ni '*a*-' (umoja) na '*wa*-' (wingi). Tofauti hizi zilibashiriwa na UL kuwa zingeweza kuwatatiza wanafunzi kupitia uhamishaji wa kiisimu hasa kuhusiana na nomino zisizo na vianzio {*m*-} (umoja) na {*wa*-} (wingi).

Ngeli ya U/I pia iliwatatiza wanafunzi, jambo ambalo huenda lililotokana na kuwepo kwa viambishi viwili vya wingi {*ya*} / {*ra*} katika Kitaita kinyume na ilivyo katika Kiswahili. Baadhi ya wanafunzi walitumia miundo ya viambishi vya Kitaita vya ngeli hii katika sentensi zao za Kiswahili kama inavyodhihirika katika Jedwali 4.1; kauli (e) na (f). Kiambishi 'zi' ni tafsiri ya '*ra*' katika Kitaita.

Uhamishaji wa kiisimu kutoka Kitaita hadi Kiswahili pia unadhihirika katika udogo wa nomino. Kauli ya (d) katika Jedwali 4.1, inathibitisha hili ambapo muundo wa kiambishi *{ka-}* cha udogo katika Kitaita umetumiwa mwanzoni mwa udogo wa nomino ya Kiswahili. Nomino za Kiswahili zikiwa katika udogo hutumia viambishi {ki-} au {kiji-} katika umoja na {vi-} au {viji-} katika wingi.

Katika Jedwali 4.1 kauli ya (g) *'chai chote kimeisha', inadhihirisha kosa la uhamishaji wa kiisimu. Tatizo hapa linatokana na mwingiliano wa mofu 'chai' katika Kitaita na Kiswahili. Chai ni mojawapo wa misamiati mingi katika lugha hizi mbili ambayo inafanana kimaumbo na kisemantiki. Hili linakuwa tatizo kwa wanafunzi wanapotumia maneno haya katika kauli za lugha ya Kiswahili kwani wanajikuta wakitumia kanuni za kisarufi za lugha yao ya kwanza. Hii ndiyo sababu ya wao kusema 'chai kimeisha' badala ya 'chai imeisha' kwani katika Kitaita nomino zote zenye vianzio '*ch*' zinapatanishwa kwa kiambishi (*ch*-) ambapo katika Kiswahili kisawe chake ni (ki).

Kwa mujibu wa Richards (1974), uhamishaji ni mojawapo wa mbinu anazotumia mwanafunzi katika ujifunzaji wake wa $L_2$ na hutokea mara kwa mara katika tungo za mwanafunzi huyo. Hii inasababishwa na hali kuwa wakati ambapo mwanafunzi anajieleza katika lugha lengwa, yeye hurejelea lugha ambayo anaimudu vizuri na ambayo ni $L_1$. Hivyo basi, atahamisha kanuni za lugha ya kwanza na kwa hivyo makosa mengine atakayofanya yatakuwa ni tafsiri ya moja kwa moja kutoka $L_1$. Hivyo mitindo ya $L_1$ huwa muhimu kwani ndiyo msingi wa sarufi ya $L_2$.

Katika sura ya pili ilibashiriwa kuwa kushabihiana na kutofautiana kati ya Kiswahili na Kitaita kungeweza kusababisha baadhi ya makosa ya kisarufi. (Taz. § 2.3 na §2.4).

### 4.1.2 Ujumuishaji mno

Kwa mujibu wa Norrish (1983), ujumuishaji unatokana na tajriba aliyo nayo mwanafunzi katika matumizi yake ya $L_2$. Mwanafunzi hufanya kosa la ujumuishaji mno anapotumia kanuni za kisarufi za dhana fulani katika lugha anayojifunza pasipotarajiwa. Hili hasa hutokana na wao kutojua kuwa kanuni husika zina mipaka yao ya matumizi. Tatizo hili limedhihirika katika kazi za wanafunzi waliochunguzwa kama vile inavyobainika katika mifano ifuatayo.

*(4.1)*

| | ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
|---|---|---|
| *a.* | **Mama amepika chakula kigani?* | *Mama amepika chakula gani?* |
| *b.* | **Ni mtoto mgani ameenda?* | *Ni mtoto gani ameenda?* |
| *c.* | **Ngombe yangu imepotea.* | *Ng'ombe wangu amepotea.* |
| *d.* | **Mtoto msafi atatuzwa.* | *Mtoto safi atatuzwa.* |
| *e.* | **Watu wakumi wamefika.* | *Watu kumi wamefika.* |
| *f.* | **Watoto wasita wameenda shambani.* | *Watoto sita wameenda shambani.* |

Mifano 4.1 (a, b na d), inahusiana na kanuni ya vivumishi kuchukua kiambishi cha ngeli aghalabu silabi ya kwanza, kama kipatanishi. Baadhi ya wanafunzi wamefanya kosa la kuchopeka kiambishi cha ngeli hata kwenye vile vivumishi ambavyo havihitajiki kutumiwa na viambishi hivyo. Vivumishi 'gani' na 'safi' havipaswi kuchukua kiambishi awali cha nomino husika.

Nayo mifano 4.1 (e na f) inaonyesha vile wanafunzi walivyokosea kwa kutanguliza kiambishi 'wa-' cha wingi wa nomino kwenye tarakimu zisizostahili kuchukua viambishi. Tatizo hili pia ni la ujumuishaji wa kanuni ya kuambisha

viambishi awali vya nomino kwenye vivumishi. Aidha, katika mfano 4.1 (f) huenda wanafunzi waliathiriwa na Kitaita ambapo tarakimu 6 huchukua kiambishi awali cha nomino kinyume na ilivyo katika Kiswahili. Ubashiri uliofanywa na UL, uliangazia kuwa tarakimu hii ingeweza kuwatatiza wanafunzi (Taz. § 2.3.2).

### 4.1.3 Uhamishaji wa ufundishaji

Selinker (1972) anasema kuwa mwanafunzi anaweza akafanya makosa kutokana na vile anavyofunzwa. Hii inamaanisha kuwa ufundishaji mbaya wa mwalimu utaakisiwa katika utendaji wa wanafunzi kimaandishi au kimaongezi. Nao Amando na wengine (2007), wanasema kuwa utendaji mdogo wa mwanafunzi wa kile anachofundishwa aghalabu hutokana na uwezo mdogo wa mwalimu au vifaa vya kufundishia. Uchunguzi ulionyesha kuwa walimu wote wa shule zote sita zilizoshirikishwa katika uchunguzi, walikuwa wamejifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Kwa sababu hii huenda pia wao wameathiriwa na $L_1$ zao na wanapowafunza wanafunzi wao, kuna uwezekano kupitisha athari walizo nazo kwa wao bila kukusudia. Kwa njia hii, makosa yao katika Kiswahili Sanifu yanahamishwa kwa mwanafunzi ambaye kwa kawaida huchukulia kuwa kila afundishacho mwalimu ni sahihi. Isitoshe, wakati mwingine mwanafunzi na mwalimu huwa na $L_1$ zinazotofautiana hivyo basi inakuwa vigumu kwa mwalimu kuelewa ugumu alio nao mwanafunzi wake katika kujifunza Kiswahili Sanifu.

Matokeo ya uchunguzi yaliweza kubainisha uhamishaji wa ufundishaji kama tatizo jingine ambalo huenda lilichangia katika makosa ya kisarufi ya wanafunzi. Zoezi la ukaguzi wa tungo za wanafunzi lilionyesha vile walimu walisahihisha kazi hizo na maelekezi waliyowapa wanafunzi. Baadhi ya tungo, zilibainisha makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi ambayo mwalimu hakuwa ameyaangazia alipokuwa akisahihisha kama inavyodhihirika katika data ifuatayo:

**Jedwali 4.2: Makosa ya kisarufi yaliyokosa kuangaziwa katika usahihishaji**

| **Shule** | **Idadi ya wanafunzi waliokuwa na makosa** | **Aina za makosa yaliyohusika** | **Idadi ya makosa** |
|---|---|---|---|
| A | 0 | - | - |
| B | 4 | Urejeshi | 4 |
| C | 3 | urejeshi<br>uakifishaji | 2<br>1 |
| D | 3 | urejeshi<br>uakifishaji | 2<br>1 |
| E | 0 | - | - |
| F | 2 | Urejeshi | 2 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Katika matokeo yaliyo kwenye Jedwali 4.2, tunaona kuwa katika shule mbili (A na E) hakukuwa na kosa lolote katika tungo za wanafunzi ambalo halikuwa limeangaziwa na mwalimu wakati wa usahihishaji. Katika shule nyingine ya B, kulikuwa na wanafunzi wanne waliofanya makosa ya urejeshi lakini mwalimu hakuwa ameyaangazia. Vilevile katika shule nyingine mbili (C na D) kulikuwa na wanafunzi watatu watatu kwa kila mojawapo ambao walifanya makosa lakini hayakuwa yameangaziwa na walimu husika. Makosa haya yalikuwa 2 (urejeshi)

na 1 (uakifishaji). Katika shule ya sita (F), kulikuwa na wanafunzi wawili waliofanya makosa ya urejeshi ambayo hayakuwa yameangaziwa.

Jambo hili la makosa ya aina fulani kutoangaziwa na mwalimu kwa zaidi ya mwanafunzi mmoja lilifanya iafikiwe kuwa huenda kwa mwalimu husika, hayo hayakuwa makosa na hivyo ndivyo alivyowafunza wanafunzi wake. Makosa haya yaliangazia udhaifu wa mwalimu katika vipengele vya kisarufi vilivyohusika ambao huenda uliakisiwa katika makosa waliyoyafanya wanafunzi wake; yaani, wanafunzi walikuwa wakiandika kulingana na vile walivyofunzwa.

Isitoshe, upungufu wa usahihishaji wa walimu ulidhihirika wazi kwani katika insha zote tulizokagua alama iliyotumika kuashiria kuwepo kwa kosa ilikuwa ya aina moja tu - kupiga mstari chini ya neno au kauli yenye tatizo. Ijapokuwa walimu wengi walifuatiliza kwa kurekebisha kosa walililoliangazia, kuna wale ambao walikuwa wanapiga tu mstari bila kurekebisha kosa lililomo. Pia, aghalabu hakukuwa na maelezo ya kuonyesha mwanafunzi ikiwa kosa husika ni la kisarufi, kihijai au kimsamiati. Ingekuwa vyema ikiwa mwanafunzi angebainishiwa makosa aliyoyafanya ndio ajue ni wapi alistahili kujitahidi zaidi. Kwa kuzingatia matokeo haya tuliona wazi kuwa mbinu za ufundishaji wa baadhi ya walimu zilichangia kwa kiwango fulani yale makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi.

### 4.1.4 Tafsiri

Kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi, ni bayana kuwa kuna makosa mengine ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi ambayo yalitokana na wanafunzi kutafsiri kauli na misamiati ya Kitaita kiholela. Katika hali hii mwanafunzi anafikiria kwa $L_1$ (Kitaita), kisha anajaribu kujiundia kauli za Kiswahili lakini anajikuta akifanya makosa kama vile ya upatanishi wa kisarufi au kuunda sentensi yenye muundo potofu. Mifano ifuatayo inathibitisha hili:

**Jedwali 4.3: Kauli za wanafunzi zilizotafsiriwa kutoka $L_1$**

| **Kauli potofu** | **Kauli sahihi ya Kiswahili** | **Tafsiri katika Kitaita** |
|---|---|---|
| a. *Mama yetu mwenye alikuwa anatusimamia. | Mama mlezi wetu aliyetusimamia. | Mka uja odisimamiagha. |
| b. *vyenye walienda shambani | walipoenda shambani... | Iji weendieghe mbuwenyi... |
| c. *Mtoto mgani ameenda? | Mtoto gani ameenda? | Mwana **u**ao waenda |
| d. *Ule wazimu aliyekuwa... | Yule wazimu aliyekuwa mbuzi... | Uja wazimu orekoghe mburi ... |
| e. *Vitu va ndani va mnyama. | Viungo vya ndani vya mnyama. | Vilambo va ndenyi va nyamandu. |
| f. *Huyo ni nani ako kwa mti juu? | Ni nani huyo aliye juu ya mti? | Uo ni ani uko kwa mudi aighu? |
| g. *vyenye alikutananga na yule jitu... | alipokutana na lile jitu... | iji okwaneghe na ijija ijumu... |
| h. *Watoto **wa**sita wameenda shambani. | Watoto sita wameenda shambani. | Wana warandadu waenda mbuwenyi. |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kutokana na mifano ya Jedwali 4.3 tunaona kuwa tafsiri ya kauli kutoka Kitaita hadi Kiswahili Sanifu ilikuwa chanzo cha baadhi ya makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi. Mwanafunzi alitumia vibaya mzizi '–enye' kama vile katika Jedwali 4.3 (a), (b) na (g). Katika Jedwali 4.3 (a) ametumia 'mwenye',

kuwakilisha urejeshi wa kiima huku Jedwali 4.3 (b) na (g) ametumia ‘vyenye’ katika kuwakilisha urejeshi wa mahali.

Aidha, kutafsiri kutoka Kitaita hadi Kiswahili kumesababisha matumizi mabaya ya viambishi vipatanishi kwani fikra ya mwanafunzi ilikuwa inawaza kauli za Kitaita. Katika Jedwali 4.3 (e), mwanafunzi alitumia kipatanishi ‘va’ badala ya ‘vya’ kwani kauli nzima ni tafsiri sisisi ya maneno ya Kitaita.

Kutokana na mwanafunzi kufikiria kwanza kwa Kitaita anajikuta akifanya kosa la kuongeza kiambishi pasipostahili. Hili tunaliona katika Jedwali 4.3 (h) ambapo kumeongezwa kiambishi ‘wa’ cha wingi wa nomino kwenye tarakimu sita, ilhali haistahili kuwa hivyo. Tarakimu sita huchukua kiambishi cha ngeli katika Kitaita wala sio katika Kiswahili.

Pia katika Jedwali 4.3 (c), kivumishi ‘gani’, hakistahili kuchukua kiambishi awali cha nomino. Kwa hivyo ni makosa kusema, ‘Mtoto **m**gani’. Huenda athari ya viulizi vya lugha ya Kitaita vimechangia kama ilivyobashiriwa na UL.Viulizi vyote katika Kitaita huchukua kiambishi awali cha nomino ilhali katika Kiswahili sio vyote vinavyochukua viambishi awali vya viulizi (Taz. § 2.1.2.3 na 2.2.2.3). Isitoshe, udondoshaji wa sauti unaodhihirika katika Jedwali 4.3 (d) ambapo mwanafunzi anasema ‘ule’ badala ya ’yule’; ulitokana na mchakato wa kisaikolojia wa wanafunzi kutafsiri maneno katika $L_2$. Hili hapa ni tatizo la tafsiri sisisi ya neno.

### 4.1.5 Kutomakinika kwa wanafunzi

Matokeo ya uchunguzi yaliweza kudhihirishia kuwepo kwa hali ya kutomakinika miongoni mwa wanafunzi kama tatizo jingine lililochangia makosa mengi ya kisarufi hasa yanayohusiana na uakifishaji. Hili hasa lilibainika katika kazi zao za uandishi wa insha ambapo wengi hawakuweza kuweka alama zifaazo za uakifishi katika kauli zao ili kutoa maana aliyokusudia kwa msomaji. Kwa sababu hii ilikuwa vigumu kwao kueleweka kwa urahisi na hata kwingineko, ujumbe ulivurugika kabisa.

Katika maandishi, matumizi ya viakifishi mwafaka husaidia kutofautisha kauli zenye maana mbalimbali kama vile swali, ombi, amri, mshangao na taarifa. Aidha, kwa kuakifisha ipasavyo, tunaweza kutofautisha usemi halisi na usemi wa taarifa. Makosa yaliyohusiana na uakifishaji yalienea katika tungo za wanafunzi mbalimbali, kama inavyodhihirika katika Jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.4: Wanafunzi waliofanya makosa ya uakifishaji**

| **Shule** | **Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa ya uakifishaji** | **asilimia** |
|---|---|---|
| A | 4 | 80 |
| B | 4 | 80 |
| C | 5 | 100 |
| D | 5 | 100 |
| E | 3 | 60 |
| F | 4 | 80 |
| Jumla | 25 | 83.33 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Tunapozingatia Jedwali hili tunaona kuwa katika shule A, B na F kulikuwa na wanafunzi wanne wanne kwa kila mojawapo waliofanya makosa ya uakifishaji ambayo inawakilisha asilimia 80 ya wanafunzi wote waliotafitiwa. Hii inamaanisha kuwa ni mwanafunzi mmoja kwa kila shule ambayo ni asilimia 20 ambaye hakuwa na kosa la uakifishaji. Aidha, tunaona kuwa katika shule A, wanafunzi watatu walifanya makosa ya uakifishaji wakiwakilisha asilimia 60 huku katika shule C na D wanafunzi wote watano yaani, asilimia 100 walifanya makosa. Kwa jumla wanafunzi 25 kati ya 30 walioshirikishwa katika utafiti, walifanya makosa ya uakifishaji. Hii inawakilisha asilimia 83.33 ya wanafunzi wote.  Walimu walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu chanzo cha makosa ya wanafunzi ya uakifishaji. Kulingana nao, wanafunzi wa darasa la saba walifunzwa uakifishaji na walitarajiwa kuakifisha ipasavyo ila wengi hawakuwa na umakinifu wa kuzingatia waliyofunzwa. Mifano ya kauli zilizohusisha uakifishaji mbaya ni kama ilivyoorodheshwa katika mfano ufuatao wa 4.2:

*(4.2)*

| ***Kauli za wanafunzi*** | ***Kauli sahihi*** |
| --- | --- |
| *a.*Tulipomuuliza yule mama wale wezi ndio wamekuibia akasema ndiyo.* | *Tulimuuliza yule mama, "Wale wezi ndio wamekuibia?" Akajibu, "Ndio".* |
| *b.*…mama akaniambia shika mia tano uwende ukalipie feya nikamwambia asante mama.* | *…Mama akaniambia, "Shika shilingi mia tano utumie kulipa nauli ya basi." Nikamwambia,"Asante,mama".* |
| **Tulienda tarehe mbili **Mombasa** kwa sababu tukajaribu nguo zetu za harusi kama zinatutosha.* | *Tulienda **M**ombasa tarehe mbili ili tukajaribu nguo zetu za harusi kama  zingetutosha.* |
| *c.   *Ilikuwa siku ya **j**umamosi mama akaniambia kesho utaenda shamba huko mosi.* | *Ilikuwa siku ya **J**umamosi mama aliponiambia kuwa siku iliyofuata ningeenda shambani* |

*huko **M**osi.*

d. **Nikafika mahali ambapo nilipoziacha mzigo wangu.* | *Nikafika mahali nilikouacha mzigo wangu.*

Tunavyoona katika mifano 4.2 (a) na (b), wanafunzi husika walikosa kuakifisha semi walizonuia zifasiriwe kama semi halisi. Kauli walizoandika zimechanganya sifa za usemi halisi na usemi wa taarifa. Nayo mifano 4.2 (c) na (d) inahusisha kosa la kuanzia nomino za pekee - Mombasa, Jumamosi na Mosi, kwa herufi ndogo. Kulikuwa pia na urudiaji wa vipashio mathalani katika mfano 4.2 (e) ambapo virejeshi ‘amba’ na ‘o’ vimetumika pamoja katika sentensi moja kurejelea kitu kimoja, ‘mzigo’. Kauli hizi zinatudhihirishia wazi kutokuwepo kwa umakinifu miongoni mwa wanafunzi kama tulivyoelezwa na walimu wao.

## 4.2 Mikakati ya kuyashughulikia makosa ya kisarufi ya wanafunzi

Kwa mujibu wa UM, kutathmini makosa ya wanafunzi ni muhimu kwani kunawezesha kutambua namna ya kushughulikia makosa hayo. Kulingana na Ellis (1994), kuchunguza makosa ya mwanafunzi humsaidia mwalimu kutathmini ufundishaji wake na kufanya matayarisho ya masomo ya baadaye. Ili kuweza kutambua mbinu za kupunguza makosa ya wanafunzi, vyanzo vyao vilizingatiwa kama vilivyodhihirika katika sehemu ya kwanza. Hatua zifuatazo zinaweza kuzingatiwa katika kupunguza makosa mbalimbali yaliyofanywa na wanafunzi.

### 4.2.1 Utangamano wa mwalimu na wanafunzi

Ellis (1985) anasistiza utangamano kati ya mwalimu na wanafunzi ambapo mwanafunzi hupewa wakati wa kutosha wa kufanya mazoezi yanayohusu stadi tofauti tofauti za kimazungumzo na za kimaandishi. Mwanafunzi anaposhiriki katika mazoezi mengi ataendelea kujirekebisha pale anapokosea kwa uelekezi wa mwalimu. Kwa mfano, mazoezi ya utumizi wa viambishi mwafaka vya ngeli za nomino utamwezesha kupunguza kosa la uhamishaji wa kanuni kutoka $L_1$ hadi $L_2$. Tunavyoona katika mifano iliyoorodheshwa hapa chini (Jedwali 4.5), kuna baadhi ya makosa ambayo ijapokuwa kwa muundo wa nje yanakaa kama ya hijai, ukweli ni kwamba yametokana na athari za maumbo ya vipengele vya kisarufi vya $L_1$ kukaribiana kufanana na vya $L_2$. Vipengele hivi humchanganya mwanafunzi asiweze kuvitofautisha kimatumizi. Tatizo hili tumeliona hasa katika viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya KI/VI kama inavyodhihirika katika kauli zifuatazo.

**Jedwali 4.5: Upotofu wa kisarufi unaotokana na athari za kukaribiana kimaumbo kwa vipengele vya kisarufi vya $L_1$ na $L_2$**

| **Kauli za wanafunzi** | **kauli sahihi** | **Kauli ya Kitaita** |
|---|---|---|
| i) *Viti **hivo** vimevunjika. | Viti **hivyo** vimevunjika. | Vitiri **ivo** vebarika. |
| ii) Viatu **va** wasimamizi | Viatu **vya** wasimamizi | Vadu **va** wasimamizi |
| iii) Vitu **va** ndani **va** wanyama. | Viungo **vya** ndani vya mnyama. | Vilambo **va** ndenyi va nyamandu. |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Katika kauli hizi tatu zinazoangaziwa katika Jedwali 4.5, maneno ’hivo’ na ’va’ yanaweza kumfanya msomaji adhanie mwanafunzi amefanya kosa la kiundelezaji; ila tunavyoona ametatizwa na vivumishi vya Kitaita. Kwa hivyo bila kutanabahi anajipata ametumia neno la Kitaita badala ya la Kiswahili kama katika ‘va’. Hili limechangiwa na kukaribiana kufanana kwa maneno haya kimaumbo na hata kimatamshi.

### 4.2.2 Wanafunzi kushirikishwa katika kukosoana

Mwalimu anaweza kurahisisha swala la wanafunzi kujirekebisha kwa kuzingatia asemayo Amando na wengine (2007) kuhusu kuwaweka wanafunzi katika makundi ambapo kila mwanafunzi atalitambua kosa la mwenzake na kulisahihisha au kila kundi kutambua makosa ya kundi lingine na kuyasahihisha. Kwa njia hii, wanafunzi watajifunza kutokana na makosa yanayofanywa na wengine na kuchukua tahadhari ya kutoyarudia pia wao.

### 4.2.3 Mwalimu kutambua chanzo cha kosa la mwanafunzi na kumwelekeza

Itakuwa muhimu kwa mwalimu kutambua chanzo cha makosa yanayofanywa na wanafunzi wake ndio aweze kuyashughulikia vilivyo. Kulingana na Ellis (1994) kuchunguza makosa wayafanyayo wanafunzi humwezesha mwalimu kuwakosoa na kuwahimiza wasiyarudie.

Katika ukaguzi wa insha za wanafunzi zilizochunguzwa ilibainika wazi kuwa walimu wote hawakuwa wakiwabainishia wanafunzi aina za makosa yaliyodhihirika katika kazi zao. Mahali popote kulikotokea kosa, walimu walitumia mtindo mmoja wa kupigia maneno yote yenye makosa kistari kimoja bila kujali ikiwa ni kosa la kisarufi, kimsamiati au kihijai. Ni vizuri ikiwa alama mbalimbali zitatumika kuashiria aina hizi tofauti za makosa na wanafunzi waelezwe zinavyomaanisha. Alama zifuatazo zinaweza kutumika:

______ makosa ya hijai

====== makosa ya kisarufi

× makosa ya kimsamiati

Hili litasaidia mwanafuzi kujirekebisha anapoandikiwa mwishoni mwa insha yake kauli za kijumla kama vile, ‘rekebisha makosa ya kisarufi’, ‘rekebisha makosa ya hijai’ au ‘tumia msamiati mwafaka’.

### 4.2.4 Mwalimu kujitayarisha vilivyo kabla ya somo

Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa baadhi ya walimu walikuwa na changamoto katika maandalizi yao kwani wengine walikuwa na aina moja tu ya kitabu cha kusomeshea kama inavyodhihirika katika data ifuatayo:

**Jedwali 4.6: Aina za vitabu vilivyotumiwa na walimu katika maandalizi yao ya ufundishaji wa sarufi**

| **Shule** | **Idadi ya aina za vitabu vya kufundishia** |
|---|---|
| A | 2 |
| B | 2 |
| C | 1 |
| D | 1 |
| E | 3 |
| F | 2 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kulingana na data ya Jedwali 4.6, walimu wa shule mbili walikuwa na kitabu cha aina moja tu, wa shule tatu wakawa na vitabu vya aina mbili na wa shule moja akawa na vitabu vitatu. Kitabu cha *Kiswahili kwa Darasa la Saba* kilichochapishwa na KLB, kilipatikana katika shule zote kwa hivyo hiki ndicho kitabu cha pekee kilichotumiwa na wale walimu wawili ambao hawakuwa na kitabu chochote cha ziada. Kitabu hiki kimesambazwa na Serikali katika shule zote za umma katika juhudi zake za kufanikisha mradi wake wa kutoa elimu ya bure na kila mwanafunzi alikuwa na nakala yake.

Shule ambapo mwalimu alikuwa na vitabu vya aina tatu ilikuwa ya kibinafsi iliyokuwa miongoni mwa zilizotafitiwa. Utafiti ulibainisha kuwa viongozi wa shule za umma hawawajibiki kuwanunulia walimu wao vitabu vya ziada kuongezea kile kinachosambazwa na serikali, bali walimu wenyewe hujukumika kujinunulia. Kwa hivyo, wale walimu wa shule tatu za umma waliokuwa na aina

mbili za vitabu; walijinunulia wenyewe nakala zao za ziada. Kuhusu utoshelevu wa kitabu hiki cha *Kiswahili kwa Darasa la Saba* katika ufunzaji wa sarufi, walimu husika walitoa maoni yaliyo katika Jedwali 4.7

**Jedwali 4.7: Maoni ya walimu kuhusu Kitabu cha *Kiswahili kwa Darasa la Saba***

| **Maoni ya walimu** | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Yaliyomo yanaoana na silabasi | 6 | 100 |
| Yaliyomo hayaoani na silabasi | 0 | 0 |
| Kitabu hiki ni toshelevu | 1 | 16.7 |
| Kitabu hiki si toshelevu | 5 | 83.33 |
| Baadhi ya mada zake za sarufi zina kasoro | 4 | 66.7 |
| Hakuna mada yoyote ya sarufi yenye kasoro. | 2 | 33.3 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kwa mujibu wa matokeo ya Jedwali 4.7, walimu wote 6 (asilimia 100); walisema kuwa yaliyomo katika kitabu hiki yanaoana na mahitaji ya silabasi. Kuhusu ikiwa kitabu hiki kinamtosheleza mwalimu au la, mwalimu mmoja alisema ni toshelevu ilhali watano wakasema si toshelevu. Aidha, walimu wanne walisema kulikuwa na kasoro katika baadhi ya mada zake za sarufi, huku wawili wakisema hakukuwa na kasoro yoyote. Uchunguzi ulithibitisha kuoana kwa mahitaji ya silabasi na yaliyomo katika kitabu hiki. Hata hivyo baadhi ya mada zina upungufu kiasi na hivyo kuna haja ya mwalimu kurejelea pia vitabu vingine ili kujitosheleza kimaandalizi.

Katika uchanganuzi wa chanzo cha makosa ya wanafunzi ya kisarufi ilibainika kuwa baadhi ya makosa hutokana na uhamishaji wa ufundishaji. Hivyo basi, ni vyema kwa mwalimu kuhakikisha kuwa amejiandaa vilivyo kabla ya kuenda darasani ili asichangie ufunzaji potofu wa vipengele mbalimbali vya sarufi. Anastahili aweze kupitia barabara vipengele mbalimbali vya kisarufi ili asije akakwama anapofundisha au akatoa habari zisizo sahihi kwani tulivyoona mwanafunzi huchukulia kila asemalo mwalimu kuwa ni sahihi. Ili kufanikisha maandalizi mwafaka kwa mwalimu, ni vyema kurejelea vitabu zaidi ya kimoja ili viweze kukamilishana pale ambapo kimoja kinaweza kuwa na upungufu kuhusiana na kipengele fulani cha kisarufi

Aidha, walimu walioathirika na lugha yao ya kwanza wanastahili pia wajitambue ili wawe makini wanapofunza ndio wasihamishe athari za lugha yao ya kwanza kwa wanafunzi ambao huenda hawatatambua kuwa ni kosa. Isitoshe, walimu wanaofunza Kiswahili wanaweza wakasaidiana katika kurekebishana kwa kuendesha ukaguzi mmoja kwa mwengine mara kwa mara wakati wanaposomesha. Ukaguzi huu hautalenga hasa kukosoana, bali kuelekezana kwa lengo la kuboreshana katika ufundishaji.

### 4.2.5 Matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa

Utafiti ulionyesha kuwa kulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa na vitabu ambavyo havikuwa miongoni mwa vile vilivyoidhinishwa kutumika na Taasisi ya

Ukuzaji wa Mitaala ya *Kenya Institute of Curriculum Development* (KICD). Hivi hasa ni vile vitabu vya ziada walivyonunuliwa na wazazi wao. Walimu walipoulizwa ikiwa walikuwa na uelekezi wowote kwa wazazi kuhusu vitabu vya ziada ambavyo walifaa kununulia wanawe, wote walisema huwaelekeza. Hata hivyo, baadhi ya walimu walikiri kuwa walikuwa hawashughuliki kufuatilia kukagua ni vitabu vya aina gani watoto walinunuliwa kama inavyobainika katika Jedwali lifuatalo la 4.8.

**Jedwali 4.8: Mchango wa walimu kwa vitabu vya wanafunzi vya ziada**

| **Mchango wa walimu** | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ninawaelekeza wazazi kuhusu vitabu vya kununua | 6 | 100 |
| Siwaelekezi wazazi kuhusu vitabu vya kununua | 0 | 0 |
| Hukagua ni vitabu gani vya ziada vinavyotumiwa na wanafunzi wangu | 4 | 66.7 |
| Sikagui ni vitabu gani vya ziada vinavyotumiwa na wanafunzi | 2 | 33.3 |

Asili: Utafiti wetu (2018)

Kwa mujibu wa yaliyomo katika Jedwali 4.8, Walimu wote 6 walikiri kuwa waliwaelekeza wazazi kuhusu vile vitabu vya ziada walivyopaswa kuwanunulia wanawe ikiwa ni asilimia 100. Hata hivyo ni walimu 4 pekee waliojitahidi kukagua ni vitabu gani vya ziada vilivyotumiwa na wanafunzi wao, huku walimu wawili wakikosa kufanya hivyo.

Ili kupunguza makosa ya uhamishaji wa ufundishaji, ni vizuri ikiwa vitabu vya kufunzia sarufi ya Kiswahili vinavyotumiwa na walimu pamoja na wanafunzi

vitakuwa vile vilivyoidhinishwa ili kuepuka kutumia vitabu potofu. Kuhusiana na hili wanafunzi na wazazi /walezi wanastahili watahadharishwe dhidi ya kununua vitabu bila kuzingatia maongozo ya walimu.

### 4.2.6 Ufundishaji wa Kiswahili kwa mwelekeo wa Uchanganuzi Linganuzi

Ni jambo mwafaka kwa mwalimu anayefunza wanafunzi Kiswahili Sanifu kujaribu kuelewa vipengele vya kisarufi vinavyofanana na vinavyotofautiana katika $L_1$ ya mwanafunzi na Kiswahili sanifu. Kwa kufanya hivi ataweza kujua mbinu iliyo mwafaka zaidi ya kutumia kuvifunza. Aidha, atawatahadharisha wanafunzi dhidi ya kutohamisha sheria na maumbo ya kisarufi kutoka $L_1$ hadi Kiswahili kwa mfano, maumbo ya ngeli ya U/I katika Kitaita.

### 4.2.7 Kutahadharisha wanafunzi dhidi ya tafsiri sisisi kutoka $L_1$ hadi $L_2$

Kama tulivyoona, hili hutokana na kufikiria semi kwanza kwa lugha moja kabla ya kuzigeuza katika Kiswahili. Kutokana na hili kunakuwa na tafsiri sisisi ya maneno au semi ambazo mara nyingi mbali na kuwa zinazua utata wa kisemantiki, huleta pia tatizo la kisarufi. Ni vyema wanafunzi wahimizwe kuepuka kufikiria kwa lugha nyingine wanapowasiliana kwa Kiswahili ili wasije wakapotoka.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura, hii vyanzo mbalimbali vya makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi vimejadiliwa huku uhusiano kati yao na ubashiri uliofanywa na nadharia ya UL katika sura ya pili ukiangaziwa. Ufafanuzi wa vyanzo hivi mbalimbali umethibitisha kuwa kuna makosa yaliyotokana na tofauti za kiisimu kati ya lugha ya Kitaita na Kiswahili Sanifu au ubia wa baadhi ya sifa zao. Haya ni pamoja na uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu kutoka $L_1$ hadi $L_2$ na ya tafsiri potofu. Aidha, makosa mengine yalitokana na uhamishaji wa ufundishaji, ujumuishaji mno na tabia ya wanafunzi ya kutomakinika au mapuuza hasa katika maandishi yao ya Kiswahili Sanifu kama ilivyodhihirika katika tungo zao. Katika sura hii pia, kwa kuzingatia nadharia ya UM, mikakati mbalimbali ambayo inaweza kuzingatiwa ili kuyashughulikia matatizo ya kisarufi yanayowakabili wanafunzi imeshughulikiwa.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inahitimisha uchunguzi kuhusu makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi wanapojifunza Kiswahili Sanifu kama lugha yao ya pili. Hitimisho hili linajumuisha muhtasari wa tasnifu nzima, matokeo ya utafiti na changamoto zilizoshuhudiwa katika kutekeleza uchunguzi huu. Vilevile mapendekezo kwa wadau mbalimbali na kuhusu utafiti zaidi yanajadiliwa.

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Lengo la utafiti lilikuwa ni kuchunguza makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi wanaojifunza Kiswahili Sanifu katika kaunti ya Taita /Taveta nchini Kenya. Utafiti huu ulijumuisha sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada, swala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti ambazo zimetumiwa katika kuendesha utafiti wetu. Madhumuni yaliyoelekeza kazi hii yalikuwa ni pamoja na: kubainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi katika kujifunza Kiswahili Sanifu; kuainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi; kuchunguza uhusiano uliopo kati ya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita na

yaliyobashiriwa na UL na mwisho kubaini na kutambua mbinu mwafaka za kuyakabili makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita katika utendaji wao wa Kiswahili Sanifu.

Sura ya pili iliangazia vipengele vya kisarufi vya lugha ya Kiswahili na Kitaita vilivyojumuisha ngeli, upatanishaji wa nomino na aina mbalimbali za vivumishi na dhana ya urejeshi. Aidha, ubashiri wa vipengele vya kisarufi ambavyo vingeweza kuwatatiza wanafunzi katika kujifunza Kiswahili Sanifu kama lugha yao ya pili ulifanywa kwa kuzingatia nadharia ya UL.

Sura ya tatu ilihusisha uchanagnuzi wa data iliyokusanywa kwa kuzingatia nadharia ya UM. Data hii ilikusanywa kupitia kwa zoezi la maswali ya hojaji, masimulizi na insha. Uchunguzi huu ulijikita katika makosa yaliyohusiana na nomino, vivumishi na virejeshi kulingana na upeo na mipaka ya utafiti wetu. Aina saba za makosa yalibainishwa.

Nayo sura ya nne ilitathmini makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi tuliochunguza. Hapa vyanzo vitano vya makosa haya ya kisarufi vilibainishwa. Aidha, mikakati mbalimbali ya kuyashughulikia ilijadiliwa kwa uelekezi wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM).

Katika sura ya tano, uchunguzi unatamatishwa. Hii inashirikisha muhtasari wa sura zilizotangulia, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na mapendekezo kwa wadau mbalimbali kuhusu utafiti zaidi.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Uchunguzi huu ulidhihirisha kuwa kategoria ya urejeshi wa nomino katika vitenzi ndiyo huathiri wanafunzi wengi zaidi. Aidha, ufafanuzi wa makosa yaliyobainishwa umewezesha kutambua aina saba za makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi: Makosa ya mpangilio potofu wa vipashio katika sentensi, matumizi ya viambishi vipatanishi vya ngeli visivyofaa, kuongeza vipashio au sauti pasipostahili, udondoshaji wa maneno au vitamkwa katika tungo, kuchanganya vipashio, uakifishaji mbaya, na urudiaji wa vipashio.

Pia, athari za lugha ya Kitaita kwa wanafunzi Wataita walio katika shule za msingi wanapojifunza Kiswahili Sanifu zimebainishwa. Baadhi ya matatizo ya wanafunzi hawa katika kujifunza Kiswahili Sanifu, yanachangiwa na kutofautiana au ubia wa baadhi ya vipengele vya kisarufi katika Kitaita na Kiswahili Sanifu. Imebainika wazi kuwa uhamishaji wa dhana za mifumo ya kiisimu za lugha ya Kitaita kwa Kiswahili Sanifu miongoni mwa wanafunzi Wataita, ni mojawapo wa vyanzo vya makosa yao ya kisarufi. Hili linaeleza ni kwa nini wanafunzi hawa licha ya kwamba wengi huongea Kiswahili na Kitaita hata kabla hawajaenda shule, bado wanafanya makosa ya kisarufi katika Kiswahili Sanifu kama $L_2$.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti, uhusiano uliopo kati ya chanzo cha makosa ya kisarufi ya wanafunzi kama yalivyodhihirika na ubashiri uliofanywa na UL katika sura ya pili ulibainishwa. Kufanana kwa vipengele kadha vya lugha hizi mbili kwa kiasi fulani kunawafanya wanafunzi wasimakinike kutambua zile tofauti finyu zilizomo na hivyo wanatatizwa na baadhi ya ngeli mathalan KI/VI na U/I. Aidha, majina ya ngeli ya A/WA yasiyoanza kwa viambishi m (umoja) na wa (wingi) yanawakanganya wanafunzi. Mifano ya majina haya ni kipofu, ng'ombe na kuku. Ngeli zingine zilizowatatiza wanafunzi ni zile zilizojumuisha majina yasiyoonyesha kiambishi chochote cha ngeli kama vile chai (ngeli ya I/I) na gari (ngeli ya LI/YA).

Vilevile, utafiti umedhihirisha kutatizika kwa wanafunzi kuhusiana na upatanishaji wa nomino na vivumishi vya sifa visivyochukua viambishi vya ngeli kama vile 'safi'. Isitoshe, upatanishaji wa nomino na tarakimu 'sita' umezua changamoto kwa wanafunzi. Hili limechangiwa na tofauti za kisarufi kuhusiana na tarakimu hii katika Kitaita na Kiswahili Sanifu. Kwa jumla, tumebainisha vyanzo vifuatavyo vya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu: uhamishaji wa dhana na mifumo ya kiisimu kutoka $L_1$ hadi $L_2$, tafsiri potofu, uhamishaji wa ufundishaji, ujumuishaji mno na tabia ya wanafunzi ya kutomakinika au mapuuza hasa katika maandishi yao ya Kiswahili Sanifu kama ilivyodhihirika katika tungo zao. Baadhi ya mikakati ya kuyashughulikia makosa haya tuliyoweza kuibainisha ni pamoja na utangamano

wa mwalimu na wanafunzi, wanafunzi kushirikiana katika kukosoana, mwalimu kutambua chanzo cha kosa la mwanafunzi na kumuelekeza, mwalimu kujitayarisha vilivyo kabla ya somo, matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa, ufundishaji wa Kiswahili kwa kuzingatia mwelekeo wa Uchanganuzi Linganuzi na kutahadharisha wanafunzi dhidi ya tafsiri sisisi.

## 5.3 Changamoto za utafiti

Ijapokuwa malengo ya utafiti huu yaliafikiwa kwa kiasi kikubwa, utafiti ulikumbwa na changamoto fulani. Kwanza, ukusanyaji wa habari nyanjani haukuwa rahisi kwani baadhi ya wanafunzi hawakuwa wanaelewa maagizo yaliyohitajika kuzingatiwa kwa haraka. Ilibidi kutumia muda mwingi kuwaelekeza kwanza ndio tuendelee. Aidha, wengine hawakuwa na ujasiri wa kuongea mbele ya wenzao kwa hivyo haikuwa rahisi kujitolea kusimulia hadithi. Ilibidi mtafiti kuwachochea zaidi kwa kuwabembeleza kwa zawadi ndio wajitokeze.

Isitoshe, ilikuwa vigumu kubainisha chanzo cha kosa kwani ilibainika kuwa kosa laweza kuwa na vyanzo zaidi ya kimoja. Hivyo basi, ilibidi kupitia data mara kadha ili kuchunguza vyema makosa hayo. Kwa mfano, kosa la upatanishaji wa nomino na vivumishi vya sifa linaweza kuwa la ujumuishaji mno, la uhamishaji wa vipengele vya kiisimu au la uhamishaji wa ufundishaji. Vilevile kumekuwa na changamoto ya kukatiziwa mawasiliano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na

wasimamizi kwa sababu ya maradhi ya Korona. Mawasiliano katika kipindi hiki yalifanyika kupita simu na mtandao. Ijapokuwa kulikuwa na changamoto hizi, matokeo ya utafiti huu yana mshabihiano mkubwa na tafiti zingine za awali mathalan, Musau (1993), Mudhune (1994), Onyango (1997), Chepkwony (2011) na Ntawiyanga (2015). Hata hivyo kuna upekee wa miundo kati ya Kiswahili na kila $L_1$ kwa waliotafitiwa.

## 5.4 Mapendekezo

Walimu wanapendekezewa kuzingatia ile mikakati mbalimbali iliyojadiliwa katika kazi hii kuhusu njia za kushughulikia makosa mbalimbali ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi (Taz. § 4.2.1 - 4.2.7). Hata kama utafiti ulihusisha wanafunzi Wataita, mikakati hii inaweza kutumika hata kwa wanafunzi wenye asili tofauti. Aidha, wakuza mitaala wanapendekezewa kutoa maelekezo kwa walimu kuhusu tofauti za kiisimu zilizoko baina ya lugha asilia na athari zao katika ujifunzaji lugha. Ilivyo kwa sasa ni kuwa wanachukulia kama wanaojifunza lugha wote hutatizika kwa jinsi sawa.

Kwa upande wa wanafunzi, tungependekeza wahimizwe kuongea Kiswahili Sanifu katika mawasiliano yao kwani lugha yao ya mazungumzo huathiri maandishi yao. Aidha, wanafaa kuelewa kuwa lugha hutofautiana kiisimu ndio waepuke kutafsiri au kuhamisha vipengele vya $L_1$ kwa $L_2$. Katika kutekeleza uchunguzi, mtafiti alikumbana na makosa mengine yasiyohusiana na kategoria

zetu za utafiti kulingana na mipaka yetu ya utafiti. Kwa hivyo, ni vyema ikiwa tafiti zaidi zitafanywa kuhusu makosa ya wanafunzi Wataita yanayohusiana na vipengele vingine vya lugha kama vile fonolojia, semantiki na hata msamiati.

## 5.5 Hitimisho

Sura hii imeonyesha muhtasari wa yaliyomo katika ripoti nzima. Aidha, imeeleza namna sura mbalimbali za utafiti zilivyochangia kufanikisha uchunguzi, kuanzia sura ya kwanza hadi ya tano. Matokeo ya uchunguzi yamelinganishwa na malengo na imethibitika kuwa Kitaita kinachangia baadhi ya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu kama $L_{2.}$ Aidha, ubashiri wa UL kuhusu mchango wa $L_1$ kwa wanaojifunza $L_2$ ulidhihirika kwa kiasi fulani miongoni mwa wanafunzi Wataita wanaojifunza Kiswahili Sanifu. Vilevile, sura hii imeshughulikia changamoto alizokabiliana nazo mtafiti na kujadili mapendekezo ya tafiti zingine.

## Marejeleo

Amando, L, Eduardo E. F, Arburim 1. na Christopher P. C. (2007). Teachers' attitudes towards correcting students' written errors and mistakes, Porta Linguarum. 10. Universi.dad de Murcia. 21-30.

Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar Including intonation*. London. Longman.

Chepkwony, C. L. (2011). *Matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kipsigis wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu.* Tasnifu ya Uzamili. Nairobi, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Corder, S.P. (1971). Idiosyncratic dialects and errors analysis. In Richards J.e. (ed). *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. London: Longman. 158 - 171.

Corder, S.P. (1974). The Significance of Learner's Errors. In Richards J.e. (ed). *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. London: Longman. 19-27.

Corder, S.P. (1981). *Error Analysis and Interlanguage.* Oxford: Oxford University Press.

Ellis, R. (1985). *Understanding Second Language Acquisition.* Oxford: Oxford University Press.

Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Aquisation.* Oxford: Oxford University Press.

Guthrie, M. (1948). *Classification of Bantu Languages.* London: Dawsons of Pall Mall.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi Ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

James, C. (1971). *An Exculpation of Contrastive Linguistics.* In Nickel G. (ed). Papers Kanezja Publisher.

James, C. (1980). *Contrastive Analysis.* Longman: London

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam. TUKI.

Karingi B .W (2012). *Ufunzaji na ujifunzaji na vibainishi katika shule za upili wilayani Kirinyaga: Mtazamo wa sintaksia Finyizi*, M.A Thesis, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. New York: Palygrave.

Krapf, J. L. (1850). *Outline of the Elements of the Kisuaheli Language with Special Reference to the Kinika Dialect.* L, F.Fues. Tubingen.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures*. Michigan: The University of Michigan Press.

Littlewood, W. (1984). *Foreign and Second Language Learning.* Cambridge: Cambridge University Press. London: Longman.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, 1. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, 1. (1985). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, 1. (1995). *Usahihishaji wa Mokosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Kenya Limited.

Mgullu, R. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publisher.

Mohamed, A. M. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Publishers.

Mudhune, E.S. (1994*). A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners*. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mugenda, O.M. & Mugenda, A.G. (2012). *Research Methods Dictionary*. Nairobi: Applied Research & Training Services.

Musau, P.M. (1993*). Aspects of Interphonology: The Study of Kenyan Learners of Swahili.* Tasnifu ya Uzamifu. Bayreuth: Bayreuth African Studies.

Mwaliwa, H. C (2000). *Ulinganishi wa Mofololojia ya Kiswahili na Kitaita*. M.A Thesis, U.O.N.

Myachina, E.N. (1981). *The Swahili Language: A Descriptive Grammar.* London: Routledge & Kegan Paul.

Norrish, J. (1983). *Language Learners and their Errors.* London: The Macmillan Press Limited.

Ntawiyanga, S. (2015). *Changamoto za Kimofosintaksia miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii*. M.A Thesis. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Odeo I.I. na Maina G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*, Nairobi: Oxford University Press.

Onyango, J. (1997). *Uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi linganuzi*. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Orodho, J.A. (2009). *Elements of Education and Social Research Methods.* Nairobi: Kanezja Publisher.

Orodho, J.A, & Kombo, D.K. (2002). *Research Methods*. Nairobi: Kenyatta University, Institute of open Learning.

Polome, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook.* Washngton D.C: Center for Applied Linguistics.

Richards, J.C. (1974). *Error analysys: Perspectives on Second language Acquisition.* London: Longman.

Selinker, L. (1972). *Interlanguage*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).

Shahim, N. (2011). Error Treatment in TESOL Classrooms. *Jordan Journal of Applied Science "Humanities Series*" .13 (1). 207 - 206.

Steere, E. (1865). *A Handbook of Swahili Language (as Spoken at Zanzibar).* London: The Sheldon Press.

Steere, E. (1969). *Swahili Exercises. Revised and partly re-written by Hellier A.B.* London: The sheldon Press.

TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI.

Van Els, T, Bongaerts , T., Extra. G. na Charles, V.O (1984). *Applied Linguistics and the Learning and teaching of Foreign* Languages, London: Edward Arnold.

Waihiga, G na Wamitila, K.W. (2003). *Chemchemi za Kiswahili, Kidato cha Kwanza*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Watuha, A (2015). *Kiswahili kwa Darasa la Saba*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

**Kiambatisho 1: Hojaji ya wanafunzi**

**Maagizo:**

1. Usiandike jina lako
2. Jibu maswali yote

Shule ________________________________

Darasa _______________________________

Umri _______________________________

1. Lugha yako ya kwanza ni gani? ________________

2. Ni lugha ipi mnayoongea nyumbani kwenu? (a) Kitaita pekee (b) Kiswahili na Kitaita

3. Ulianza kuongea Kiswahili wakati gani?

   i. Kabla niingie shule

   ii. Nilipojiunga na shule

4. Umewahi kuishi mahali kwingine mbali na Taita? i) Ndiyo ii) La

   Ikiwa ndiyo,

   i. Mahali penyewe panaitwaje? ____________________

   ii. Uliishi huko kwa muda gani? ____________________

**Kambatisho 2: Jaribio la wanafunzi**

**Maagizo**

i. Usiandike jina lako
ii. Andika majibu kwenye nafasi zilizoachwa.
iii. Jibu maswali yote.

**Sehemu 1**

**Andika sentensi zifuatazo kwa Kiswahili**

1. Mao waenda mbuwenyi.
2. Ngombe ija ya chilu yawakamwa
3. Kikapu chalagaya
4. Midi iri rawademwa.
5. Chai chose chasia.
6. Mtaro gwawakotwa sena
7. Moda ghooma
8. Andu aho wangia kwaelie sana.
9. Akaja kanguwo kagokie sana.
10. Ako kamoda keoma.
11. Wana warandadu waenda idukenyi.
12. Mkonu goka na  vala visanu.
13. Lumi lulacha.
14. Kubora  kwake kwapoie
15. Vindo ivija vadekwa vasia.

16. Mwana uja uendieghe wawuya.

17. Mwana upoie ni uja usikiraga wavi wake.

18. Kamba ndacha yadumbuka.

**SEHEMU 2**

Jaza nafasi zilizoachwa kwa kiambishi mwafaka pale panapostahili.

1. Mtoto ___ake -melala.

2. Ng'ombe –ngu amepotea.

3. Kiatu chake __ mepotea.

4. Miti __ake ___ote __nakatwa.

5. Mkoba __angu __mebwa.

6. Gari ___ke ni __zuri.

7. Inzi ___enyewe __mekufa.

8. Kiguo ___meraruka.

9. Mtoto ___o__ote aliye ___safi atatuzwa.

10. Amenunua nguo ___pya.

11. Guo __lilonunuliwa ___napendeza.

12. Amenunua maembe __nane.

13. Viti hivyo __ote ____nne vimevunjika.

14. Watu ___ote ___kumi wamefika.

15. Ni mtoto ___gani ameenda?

16. Umeadhibiwa na mwalimu __pi?

17. Mama amepika chakula ___gani?

18. Meza __mevunjika.

19. Chai __ote __meisha.

(Tumia 'o' rejeshi, 19-21)

20. Nyumba ina___jengwa ni yangu

21. Miembe -ote ili-mea ni mizuri.

22. Mvulana ali-kuja ni huyu.

**Kiambatisho 3: Kiongozi cha mahojiano ya wanafunzi**

Simulia hadithi yoyote uliyowahi kuisikia.

1. Je, hadithi hii inatufunza nini?
2. Wahusika wa hadithi hii ni nani?
3. Wahusika wa hadithi hii wana sifa gani?

**Kiambatisho 4: Kiongozi cha mahojiano na walimu**

Shule ____________________________________

1. Kiwango chako cha elimu ni gani?

2. Umefunza Kiswahili kwa miaka mingapi?

3. Ni vitabu gani vinavyotumiwa na wanafunzi wako kujifunzia?

4. Unatumia vitabu gani kufundishia sarufi?

5. Vitabu hivyo vinakidhi mahitaji ya malengo yako unapojiandaa kufundisha mada mbalimbali za sarufi zilizo katika silabasi?

6. Ni vipengele gani vya kisarufi vinavyowatatiza wanafunzi wako?

7. Ni aina gani za makosa ya kisarufi wanayofanya wanafunzi wako?


8. Unafikiri makosa haya ya kisarufi yanasababishwa na nini?

9. Ni hatua gani unazochukua ili kupunguza makosa haya ya kisarufi?

10. Je , unawaambia wazazi ni vitabu gani vya ziada vya kununulia wanawe?

11. Huwa unahakikisha vitabu vya ziada vinavyotumiwa na wanafunzi ni vile vilivyopendekezwa?

**Kiambatisho 5: Barua ya shule ya kuidhinisha utafiti**



KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/CE/28176/2013

DATE: 5th May, 2017

Director General,
National Commission for Science, Technology
& Innovation
P.O. Box 30623-00100,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MARTINA ZIGHE – REG. NO. C50/CE/28176/2013

I write to introduce Mr. Martina Zighe who is a Postgraduate Student of this University. He is registered for M.A degree programme in the Department of Kiswahili and African Languages.

Mr. Zighe intends to conduct research for an M.A Proposal entitled, **"Makosa ya Kisarufi Yanayofanywa na Wanafunzi Wataita wa Shule za Msingi Wanaojifunza Kiswahili Sanifu Katika Kaunti ya Taita/Taveta Nchini Kenya"**.

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

MRS. LUCY N. MBAABU

**Kiambatisho 6: Kibali cha NACOSTI**



THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MS. MWAWUGANGA MARTINA ZIGHE*
of KENYATTA UNIVERSITY, 0-1020
Kenol,has been permitted to conduct
research in *Taita-Taveta County*

on the topic: *MAKOSA YA KISARUFI YANAYOFANYWA NA WANAFUNZI WATAITA WA SHULE ZA MSINGI WANAOJIFUNZA KISWAHILI SANIFU KATIKA KAUNTI YA TAITA /TAVETA NCHINI KENYA.*

for the period ending:
*6th December,2018*

*Applicant's Signature*

Permit No : NACOSTI/P/17/63372/20491
Date Of Issue : 6th December,2017
Fee Recieved :Ksh 1000

*Director General*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*